# "MCHANGO WA SITIARI ZA KISWAHILI KATIKA KAULI ZA KICHOCHEZI KWENYE DISKOSI YA KISIASA NCHINI KENYA"

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

NA

VICTOR OCHIENG MENYA

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (MA) KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI

*1701960*
UoN Thesis
2018

DISEMBA, 2017

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

.............................................................................. Tarehe 14.12.2017

Victor Ochieng Menya

Tasnifu hii imetolewa kwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa mtahiniwa waliotolewa na chuo kikuu cha Nairobi:

.............................................................................. Tarehe 14.12.2017

Dr. Hezron Mogambi

(Msimamizi)

.............................................................................. Tarehe 14/12/17

Dr. Jefwa Mweri

(Msimamizi)

# TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia kwanza kabisa bibi yangu mpendwa Evaline Akinyi kwa kunisaidia kwa hali na mali wakati nilipokuwa ninasoma. Pia kwa kunipa moyo wa kuendelea na kazi yangu ya utafiti pamoja na kunipa utulivu wa moyo na akili. Pia watoto wangu Viola Esther na Vincent Junior kwa kunivumilia sana nikiwa masomoni. Hata hivyo sitasahau kuwashukuru ndugu zangu Martin, Phelix, Ronald, Erick, Mariet, Lilian, na Irene kwa kunisaidia kwa njia moja au nyingine katika masomo yangu ya awali Mungu awabariki nyote.

## SHUKRANI

Kwa kweli kazi hii imekuwa na panda shuka nyingi sana lakini kwa usaidizi wa watu mbalimbali niliweza kuikamilisha. Kwanza ningependa kumshukuru muumba wangu Mungu aishiye milele, kwa kunipa siha njema na akili timamu, pamoja na hekima, ili kufanikisha malengo yangu ya kiusomi. Ni kupitia kwa nguvu na uwezo wake, ambapo nimeweza kuitimiza ndoto yangu, ya kupata shahada ya uzamili, katika somo la Kiswahili. Shukrani zingine nazitolea wasimamizi wangu; Dkt. Hezron Mogambi na Dkt. Jefwa Mweri kwa kunielekeza hatua kwa hatua, kunikosoa na kunirekebishia kazi yangu pamoja na kunivumulia. Ni kupitia kwa juhudi zao ambapo kazi yangu iliweza kukamilika na kuwa ya kutamanika. Shukrani zingine ziwaendee wahadhiri wangu wapenzi walionifunza. Prof. John Habwe, Prof. Kineene Wa Mutiso, Dkt. Zaja Omboga Prof. Iribe Mwangi, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Jefwa Mweri, Prof, Mwenda Mbatiah, Dkt. Prisca Jerono na Bw. Sanja Leonard.

Vilevile wahadhiri wote wa Chuo Kikuu cha Nairobi ambao wengi pia walinifunza na kunisaidia kwa njia moja au nyingine. Mungu awabariki nyote na awape hekima na siku nyingi ili msaidie wengine kama mimi. Ninawashukuru pia wasomi wenzangu tulioshirikiana na kushauriana pamoja na kuhimizana na kuchukuliana mizigo. Sanasana sitasahau mahubiri na maombi tuliyokuwa tukianza nayo kila asubuhi. Wao ni Raymond, Oiro, Domnic, Peter, Shem, Githinji, Okello, Silas, Lilian, Rose, Florence, Jackline, Nancy, Veronica, Chaniro, Christine, na Pauline. Asanteni kwa ushirikiano wenu.

Ninawashukuru wafanyi kazi wa Tume ya Muungano na Ushirikiano (NCIC) kwa ushirikiano wao. Mwisho ningependa kutoa shukrani za kipekee kwa babangu Bw. Vincent Menya kwa ufadhili wake katika masomo yangu, ushauri wake na kunielewa kila nilipohitaji ruhusa ya kuhudhuria shughuli zangu za kimasomo. Wengine ni marafiki zangu wa dhati Raymond Owala kwa kunipa moyo na msaada niliohitaji pamoja na Peter Mwita. Sitasahau kumshukuru Samwel Nyamai kwa kujitolea kunipigia chapa kazi zangu zote za kiusomi pamoja na kupanga na kurekebisha makosa yaliyojitokeza. Barikiwa sana. Kwenu nyote ambao sikuwataja kwa majina na ambao mlinifaa kwa njia moja au nyingine, ninawashukuru sana na Mungu awamiminie baraka zisizo na kikomo.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza jinsi sitiari za Kiswahili hujitokeza katika kauli za wanasiasa na jinsi wanasiasa huweza kuzitumia kueneza kauli za kichochezi nchini Kenya. Vile vile, jinsi lugha ya Kiswahili ijapokuwa ni lugha rasmi na ya kitaifa inayotakikana kuunganisha wananchi huchangia kueneza kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya, jinsi lugha ya Kiswahili huweza kutumiwa kama chombo cha kuleta uwiano wa kijamii nchini Kenya. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchambua matumizi ya sitiari za Kiswahili katika kauli ya kichochezi kwenye diskosi ya kisiasa nchini ili kubaini na kuchunguza michango yao katika kueneza kauli za kichochezi katika siasa za Kenya. Utafiti huu ulinuia kuchangia pakubwa katika tafiti zilizopo, na kuongeza maarifa mapya katika pengo la kiusomi katika eneo la mchango wa sitiari za Kiswahili katika kauli za kichochezi kwenye diskosi ya kisiasa nchini Kenya. Njia ya utafiti ya mtandao wa *Youtube*, maktabani na data kutoka kwa tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano (NCIC) ilitumika kuleta maelezo ya mada chini ya uchunguzi kwa kutumia nadharia ya vitendo usemi. Data ilichambuliwa kwa kuzihusisha na malengo ya utafiti. Utafiti huu umebaini kuwa, sitiari ina mchango mkubwa katika semi zozote, inachangia pakubwa katika kueneza kauli ya chuki katika siasa nchini Kenya kwa kuwagawanya na kuwadunisha jamii lengwa. Wanasiasa mara nyingi hutumia sitiari kwenye matamshi yao kwenye kampeni kwa njia ya kushawishi wafuasi wao na pia kuwachochea dhidi ya jamii pinzani. Lugha ya Kiswahili ijapokuwa ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya ina mchango katika kueneza kauli ya chuki siasani kwa kutumia msamiati ambao wanasiasa hutumia kama matusi dhidi ya jamii nyingine. Vile vile, lugha ya Kiswahili inaweza kutumika kuleta uwiano wa kijamii nchini Kenya. Hata hivyo, licha ya kubuniwa kwa sheria na sera za kukabili hotuba na matamshi ya chuki nchini Kenya, bado kuna changamoto zinazozuia makabiliano dhidi ya kauli ya chuki katika siasa.

## YALIYOMO


**UNGAMO** .......... ii

**TABARUKU** .......... iii

**SHUKRANI** .......... iv

**IKISIRI** .......... v

**YALIYOMO** .......... vi

**ISTILAHI NA VIFUPISHO** .......... ix

**ISTILAHI** .......... x

**SURA YA KWANZA** .......... 1

1.0 Utangulizi .......... 1

1.1 Usuli wa mada .......... 1

1.2 Tatizo la utafiti .......... 4

1.3 Sababu za kuchagua mada .......... 5

1.4 Malengo ya utafiti .......... 5

1.5 Nadharia tete .......... 6

1.6 Upeo na mipaka .......... 6

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada .......... 6

1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu viathiriwa huru vinavyochangia kauli za kichochezi katika siasa... 7

1.7.2. Sitiari .......... 7

1.7.3 Lugha ya Kiswahili .......... 12

1.7.4 Vyama na viongozi wa kisiasa .......... 13

1.7.5 Vyombo Vya Habari .......... 14

1.7.6 Wananchi .......... 14

1.8. Nadharia ya utafiti .......... 15

1.8.1 Nadharia ya Vitendo usemi (VU) .......... 15

1.9 Misingi ya nadharia .......... 18

1.10 Muhtasari wa yaliyoandikwa kuhusu mada hii .......... 18

1.11 Njia za utafiti .......... 19

1.11.1 Uteuzi wa sampuli .......... 19

1.11.2 Eneo la utafiti .......... 19

1.11.3 Idadi ya watu inayolengwa....20
1.11.4 Mbinu za ukusanyaji wa data....20
1.11.5 Mbinu za uchanganuzi wa data....20
1.11.6 Uwasilishaji wa data....21
1.11.7 Uhalali wa kuaminika....21
1.11.8 Maadili ya utafiti yanayohitajika....22
**SURA YA PILI**....23
**AINA MBALIMBALI ZA SITIARI NA DHANA MUHIMU KATIKA NADHARIA YA VITENDO USEMI**....23
2.0 Utangulizi....23
2.1 Maana ya sitiari....23
2.2. Aina ya vitendo usemi....27
2.2.1. Lokusheni....27
2.2.2. Ilokusheni....27
2.2.3. Vitendo Usemi Elekezi (VUE)....29
2.2.4. Vitendo Usemi Ahadi (VUA)....29
2.2.5. Vitendo Usemi Taarifa (VUT)....30
2.2.6. Vitendo Usemi Hisia (VUH)....30
2.2.7. (Vitendo Usemi Maamuzi (VUM)....30
2.2.8. Palokusheni....32
2.3. Kanuni za ufasaha....33
2.3.1. Kanuni ya maana ya kiproposisheni....34
2.3.2. Kanuni za matayarisho....34
2.3.3. Kanuni za uaminifu....35
2.3.4. Kanuni za msingi....35
2.4. Kitenda na kitaarifu....35
2.5 Proposisheni....36
2.6. Nguvu ilokusheni....39
2.7 Hitimisho....41

**SURA YA TATU** ........ 42
**VITENDO USEMI KATIKA SITIARI ZA KISWAHILI ZINAZOTUMIKA KATIKA** ........ 42
**SIASA NCHINI KENYA** ........ 42
3.0 Utangulizi ........ 42
3.1 Hitimisho ........ 56
**SURA YA NNE** ........ 57
**JINSI LUGHA YA KISWAHILI NA MATUMIZI YA SITIARI ZA KISWAHILI YANAVYOCHANGIA KUENEA KWA KAULI YA CHUKI KATIKA SIASA NCHINI KENYA** ........ 57
4.0 Utangulizi ........ 57
4.1 Jinsi lugha ya Kiswahili inachangia kuenea kwa kauli ya chuki katika siasa nchini Kenya ........ 57
4.2 Mchango wa sitiari za Kiswahili katika kuenea kwa kauli za chuki katika siasa nchini Kenya59
4.3 Jinsi lugha ya Kiswahili inaweza kutumika kama chombo katika kuleta umoja wa kijamii nchini Kenya ........ 61
4.4 Hitimisho ........ 64
**SURA YA TANO** ........ 66
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 66
5.0 Utangulizi ........ 66
5.1 Muhtasari ........ 66
5.2 Hitimisho ........ 67
5.3 Mapendekezo ........ 68
5.4. Mapendekezo ya utafiti zaidi ........ 70
**MAREJELEO** ........ 71
KIAMBATISHO 1: Mpangilio wa muda uliotumika ........ 74
KIAMBATISHO 2: Bajeti ........ 75
KIAMBATISHO 3: Sitiari zingine ........ 76
KIAMBATISHO 4: Aina Mbalimbali ya Uainishaji wa Vitendo Usemi ........ 77
KIAMBATISHO 5: Kauli za kichochezi zilizochambuliwa ........ 78

## ISTILAHI NA VIFUPISHO

## VIFUPISHO

**AP**------------------------------------Athari ya Kipalokusheni

**MP**-----------------------------------Maana ya Kiproposisheni

**NI**------------------------------------Nguvu Ilokusheni

**Taz**----------------------------------Tazama

**VU**-----------------------------------Vitendo Usemi

**VUA**--------------------------------Vitendo Usemi vya Ahadi

**VUE**--------------------------------Vitendo Usemi vya Vielekezi

**VUH**--------------------------------Vitendo Usemi vya Hisia

**VUI**---------------------------------Vitendo Usemi vya Ilokusheni

**VUL**--------------------------------Vitendo Usemi vya Lokusheni

**VUM**-------------------------------Vitendo Usemi vya Maamuzi

**VUP**--------------------------------Vitendo Usemi vya Palokusheni

**VUT**--------------------------------Vitendo Usemi vya Taarifa

**USHMM**---------------------------United States Holocaust Memorial Museum

## ISTILAHI

| | |
|---|---|
| **Ilokusheni** | Nia ya kimawasiliano aliyonayo msemaji. |
| **Kauli ya kichochezi**. | Ni matumizi yanayomshambulia mtu au kikundi cha watu kulingana na vipengele kama jinsia, kabila, dini, rangi, ulemavu au mahusiano ya kimapenzi. |
| **Kitaarifu** | Tamko ambalo hutolewa linaloweza kuthibitishwa kuwa ama la ukweli au uwongo. |
| **Kitenda** | Tamko ambalo kwalo msemaji hufanya jambo fulani kwa kusema pekee. |
| **Kitendo usemi** | Tamko lichukuliwalo kama kitendo ambalo kwalo msemaji hutenda jambo. |
| **Lokusheni** | Kitendo cha kutoa tamko lolote. Dhana hii pia tumeiita unatiki kurejelea usemaji |
| **Lugha chafu** | Ni lugha ya matusi na yenye chuki ambayo inamshambulia mtu au kikundi na huweza kuwa na au isiwe na nia ya kusababishaVurugu |
| **Nguvu ilokusheni** | Ni nguvu ambazo tamko huwa nazo pindi tu linapotamkwa. |
| **Palokusheni** | Kitendo cha msemewa kutokana na athari ya kitendo hicho kwa tabia, imani na hisia. |
| **Propaganda** | Ni habari au maandiko yaliyotiwa chumvi sana yenye madhumuni yakushawishi watu ili wabidili mawazo yao. |
| **Proposisheni** | Ni kiini cha kisemantiki cha sentensi kinachoamua kanuni za ukweli za sentensi hiyo pasi kuzingatia muundo wake wa kisintaksia. |
| **Sitiari** | Ni tamathali ya usemi ya kuhusisha kitu kimoja na kingine chenye sifa zinazofanana. |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

### 1.1 Usuli wa mada

Lugha imekuwa chombo cha kutumiwa na wanasiasa katika kila mamlaka ya kutafuta kura na ushawishi wa uchaguzi kwa njia moja au nyingine. Wanasiasa hutumia lugha na sitiari katika mikutano ya kampeni, vipindi katika redio na runinga, matangazo katika vyombo vya habari, kwenye mtandao kama vile *twitter, facebook, blogs, youtube, na istagram* miongoni mwa mitandao mingine ya jamii (Kalmoe, 2014). Kwa mujibu wa Umar (2015), Lugha ni chombo muhimu zaidi katika kushawishi ambayo mtu anaweza kutumia ili kudhibiti na kuathiri tabia ya mwingine. Kwa upana, lugha inaweza kurejelea elementi kama vile mawasiliano ya maongezi, lugha shara au ishara za mwili, muonekano na mienendo inayoashiriwa. Hivyo basi, matumizi ya sitiari za Kiswahili yanaweza kujitokeza wazi wakati mwanasiasa anawahutubia wapiga kura ana kwa ana au kwa kutumia mwakilishi wake. Kenya ina zaidi ya makabila arubaini na mawili ambayo huzungumza kwa lugha tofauti. Mara nyingi, wagombea hutumia sababu hizi za kuwepo kwa lugha tofauti tofauti zinazozungumzwa na makabila tofauti kuwagawanya wananchi kwa kutumia kauli za kichochezi ili kuwachochea jamii zao dhidi ya wapinzani wao kutoka kwa makabila mengine (Oddsdottir, 2014).

Vile vile, sitiari ni neno linalojitokeza katika maandishi ambayo hufahamisha na hutoa ufahamu wa ziada kwenye kauli ya kichochezi na siasa. Kwa mujibu wa Landau et. al (2010), sitiari haizidishi utamu wa hotuba pekee, bali pia huboresha zaidi jinsi watu hufanya maamuzi baina yao na kufikiria kuhusu mwingiliano wa kijamii. Sitiari zinaweza kufaa kama hekima ambayo huwasaidia watu kuelewa na kuwasilisha mawazo mazito na ya kidhahania kwa kurejelea vitu halisi zaidi na michakato mbalimbali (Bougher, 2012). Kwa hivyo, watu wengi hutumia sitiari katika siasa ili kuwezesha uelewa kutokana na utata, ukosefu wa utamu na hali isiyotabirika ya siasa. Aghalabu, sitiari za kichochezi zinazotumika katika siasa hugeuka kuwa kauli za kichochezi, ambayo baadaye huchochea vita vinavyojitokeza baina ya makabila mbalimbali, husababisha mauaji na vita baina ya mataifa (Hartman, 2012).

Isitoshe, maana ya usemi hutegemea muktadha ambamo usemi huo umo, na kuna sababu kadhaa ambazo zinaweza kuiathiri au kuibadilisha. Uchambuzi wa maneno yenyewe, hayafafanui habari nzima. Ni muhimu kuzingatia anayezungumza, nia yake na uhusiano wake kwa hadhira. Pia, ni muhimu kuzingatia mahitaji ya hadhira na uelewa wao wa ujumbe (USHMM, 2015). Kauli ya kichochezi ni matamshi yanayomshambulia mtu au kikundi cha watu kulingana na vipengele kama jinsia, kabila, dini, rangi, ulemavu, au mahusiano ya kimapenzi. Katika sheria za baadhi ya nchi, kauli ya kichochezi inaelezwa kama matamshi, ishara, au tabia, maandishi, au maonyesho ambayo ni haramu kwa sababu yanaendeleza uhasama au hatua ya kudhuru ulinzi wa mtu binafsi au kikundi kwa sababu inatishia usalama wa aliyelindwa au kikundi cha watu (Bell, 2009). Sheria inaweza kutambua kikundi kinachopokea ulinzi kutokana na sifa fulani. Katika sheria za nchi nyingine kama Marekani na India, kauli ya kichochezi si msamiati wa kisheria. Vilevile, katika baadhi za nchi kama vile Rwanda, mwathiriwa wa kauli ya kichochezi anaweza kutafuta haki chini ya sheria za kiraia na sheria za makosa ya jinai (Kinney, 2008). Baadhi ya visababishi vya kauli ya kichochezi katika siasa ni pamoja na kuwepo kwa lugha tofauti za kikabila, siasa za ukabila, matumizi ya sitiari, lugha chafu, na kubaguliwa kwa baadhi ya makabila katika nchi katika masuala ya maendeleo na utawala (Bell, 2009)

Kulingana na United States Holocaust Memorial Museum (USHMM,2010), vita vya Bosnia-Herzegovina kutoka mwaka wa 1992-1995 vilisababisha mauaji ya baadhi ya raia 100,000, ikiwa asilimia 83% vikiwa vifo vya waislamu wa Bosnia. Kutokana na kusambaratika kwa Srebrenica, wanajeshi wa Bosnia walitekeleza mauaji makubwa kule Ulaya tangu mauaji ya wanaume na wavulana 8,000 kule nchini Ujerumani kitendo ambacho mahakama kuu ya ulimwengu ya Yugoslavia ya zamani yaliita mauaji ya kikatili. Vita vya Bosnia vilitendeka katika mazingira ya kusambaratika kwa Yugoslavia ya zamani, wakati viongozi watukufu, kutoka Serbia walipobadilisha kiini cha ujumbe wa vyombo vya habari vya taifa kutoka kwa umoja na undugu hadi kwa chuki za kale za kikabila. Mnamo mwaka wa 1994, idadi ya wakazi 7,000,000 huko Rwanda ilijumuisha makabila matatu; Hutu (85%), Tutsi (14%) na Twa (1%). Kati ya Aprili na Julai mwaka huo, angalau watutsi 500,000 waliuawa wakati mkereketwa wa kiserikali wa kihutu alizindua mpango ulioongozwa na serikali wa kuua watutsi wote nchini na wengine waliopinga sera za serikali. Wahusika wa mauaji hayo walitumia propaganda ambazo zilijazwa na kauli za kichochezi katika kampeni kwa redio, magazeti na kufanya mashauri ya moja kwa moja kwa

makabila wakiwahimiza kushiriki katika vita kabla na baada ya mauaji ya kikatili (Herz & Peter, 2012).

Vita vya kiraia nchini Guatemala vilifanyika kuanzia mwaka wa 1960-1996, vikazidisha kuwa uhasama wa kikatili kuanzia mwaka wa 1981-1983. Zaida ya watu 200,000 wa Mayan waliuawa na wanajeshi wa Guatemala walifanya watu zaidi ya 1,500,000 kuhamishwa kutoka kwa makazi yao kama njia ya kupambana na waasi. Wanajeshi hao waliandaliwa kweli kweli ili kushiriki katika kampeni za kuwakandamiza wenyeji, lakini hawakufaulu kueneza propaganda kwa umma. Nchini Kenya, kauli za kichochezi zimesababisha madhara mabaya kwa zaidi ya makabila 42 yanayopakana. Uchaguzi wa rais wa mwaka wa 2007 nchini Kenya ulikuwa umezungukwa na utata na unachukuliwa kuwa ulisababishwa na serikali. Vyama vya kisiasa nchini Kenya vimegawanyika kwa kiasi kikubwa katika msingi ya kikabila, na hasira kuhusu matokeo ya uchaguzi zilibadilika zikawa ghasia za kisiasa pamoja na ndimi za chuki za kikabila (Bell, 2009). Vyombo vya habari, hasa stesheni za redio za lugha za kienyeji, zilieneza kauli za kichochezi kabla na wakati vurugu zilipotokea. Arafa mbali mbali zilizotumwa pia zilichangia pakubwa katika usambazaji wa ujumbe kwa njia chanya na hasi (Sharon, 2013). Kutokana na madhara mabaya ya ghasia za baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007-2008, taifa la Kenya liliidhinisha katiba mpya mwaka wa 2010 ili kukabiliana na kauli za kichochezi miongoni mwa ukosefu wa haki nyinginezo.

Kwa mujibu wa Tume ya Venice (2008), Albania, Austria, Ubelgiji, Denmark, Ufaransa, Ugiriki, Ireland, Uholanzi, Poland, Romania, Uturuki, na Uingereza, miongoni mwa nchi nyingine zimepitisha sheria za ndani ili kukabiliana na kauli za kichochezi. Vilevile, katiba ya Kenya (2010) inatoa uhuru wa kujieleza na kutangamana. Ibara ya 33(1) na (3) ya katiba ya Kenya inatoa masharti ya uhuru wa kujieleza; ibara 34(1) na (4) inashughulikia masuala mbali mbali yanayokabiliana na uhuru wa vyombo vya habari; ibara 35(1) na (3) inahusika na masuala ya kupata ujumbe na ibara 36(1) na (3) inatoa masharti ya masuala yanayohusiana na uhuru wa kutangamana. Ibara ya 33(1) inaeleza kwamba kila mtu ana haki ya uhuru wa kujieleza ambao ni pamoja na; Uhuru wa kutafuta, kupokea na kutoa habari au mawazo, uhuru wa ubunifu wa kisanaa na uhuru wa kitaaluma na uhuru wa utafiti wa kisayansi.

Bila kujali masharti haya, ibara ya 33(2) inasema kwamba haki ya uhuru wa kujieleza haipaswi kuenda mipaka na yafuatayo; propaganda kwa ajili ya vita, kuchochea vurugu, kauli ya kichochezi au na kueneza chuki ambayo inaweza kuimarisha uhasama baina ya makabila na kusababisha madhara au uchochezi katika msingi wa ubaguzi ambao unakiuka ibara 27(4).

Aidha, sheria za vyombo vya habari (2007), sheria ya tume ya kitaifa ya Uwiano na Utangamano (2008) na kanuni za maadili kwa mazoezi ya uandishi wa habari nchini Kenya inaelezea wazi yanayohusu kauli za kichochezi. Kutokana na maelezo haya ni bayana kuwa lugha ni chombo kinachoweza kutumika kuunganisha watu na pia kujenga uhasama baina ya watu. Kwa mantiki hii, tuliazimia kuchunguza mchango wa sitiari katika kauli za kichochezi kwenye diskosi ya kisiasa nchini Kenya.

## 1.2 Tatizo la utafiti

Sitiari ni tamathali ya usemi muhimu ambayo hufahamisha na hutoa ufahamu wa ziada katika matamshi. Kwa mujibu wa Landau et. al., (2010), sitiari haizidishi utamu wa hotuba pekee, bali pia huboresha zaidi jinsi watu hufanya maamuzi baina yao na kufikiria kuhusu mwingiliano wa kijamii. Sitiari zinaweza kufaa kama hekima ambayo huwasaidia watu kuelewa na kuwasilisha mawazo mazito na ya kidhahania kwa kurejelea vitu halisi zaidi na michakato mbalimbali (Bougher, 2012). Kwa hivyo, watu wengi hutumia sitiari katika siasa ili kuwezesha uelewa kutokana na utata, ukosefu wa utamu na hali isiyotabirika ya siasa. Matumizi haya ya sitiari za Kiswahili hasa katika diskosi ya siasa nchini Kenya pia hupelekea baadhi ya wanasiasa kutumia sitiari kwa njia ya kiuchochezi.

Licha ya taifa la Kenya kuwa na tume ya kitaifa ya Uwiano na Utangamano (NCIC) na kuwatia mbaroni wanasiasa kama njia ya kukabiliana na kauli za kichochezi, bado kunatokea kauli nyingi za kichochezi zinazoenezwa na wanasiasa na wananchi tofauti tofauti kutumia sitiari.

Utafiti huu utachunguza jinsi sitiari za Kiswahili hujitokeza katika kauli za wanasiasa na jinsi wanasiasa huweza kuzitumia kueneza kauli za kichochezi nchini Kenya, mchango wa Kiswahili katika kueneza kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya ijapokuwa ni lugha rasmi na ya taifa inayotakikana kuunganisha wananchi, jinsi lugha ya Kiswahili huweza kutumiwa kama chombo cha kuleta uwiano wa kijamii nchini Kenya na changamoto zinazoibuka katika

utekelezaji wa sera za uwiano wa kijamii nchini Kenya. Isitoshe, utafiti haba pia umefanywa kuhusu mchango wa sitiari za Kiswahili katika kauli za kichochezi kwenye diskosi za kisiasa nchini Kenya. Hivyo basi utafiti huu ulilenga kulipunguza ikiwa si kuliziba pengo hilo la kiusomi.

### 1.3 Sababu za kuchagua mada

Utafiti huu unanuiwa kuchangia pakubwa katika tafiti zilizopo, na kuongeza maarifa mapya katika pengo la kiusomi katika eneo la mchango wa sitiari katika kauli za kichochezi kwenye diskosi ya kisiasa nchini Kenya. Matokeo ya utafiti huu yataipa msaada serikali na Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano (NCIC) kuboresha sheria na sera zilizopo kuhusiana na kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya. Inadhamiriwa kuwa matokeo ya utafiti huu yatatumiwa kuboresha maendeleo ya mfumo mzuri wa utekelezaji wa sheria kuhusu kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya.

Matokeo ya Utafiti huu pia yatawezesha serikali ya Kenya kubadilisha mikakati na mienendo yao ya kukomesha kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya. Pia inatarajiwa kwamba matokeo ya utafiti huu yatakuza ushirikiano kati ya wafanyakazi watakaopewa mamlaka ya kushughulikia tatizo la kauli ya kichochezi nchini Kenya.

### 1.4 Malengo ya utafiti

Lengo pana la utafiti huu ni: kuchambua matumizi ya sitiari za Kiswahili katika kauli ya kichochezi kwenye diskosi ya kisiasa nchini Kenya.

Utafiti huu una madhumuni yafuatayo;

i. Kubainisha jinsi lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha rasmi na lugha ya taifa huchangia kueneza kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya,

ii. Kuchunguza mchango wa sitiari za Kiswahili katika kueneza kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya,

iii. Kuchunguza jinsi lugha ya Kiswahili inaweza kutumiwa kama chombo cha kuleta uwiano wa kijamii nchini Kenya

## 1.5 Nadharia tete

Katika utafiti huu tulikisia yafuatayo:

i) Ijapokuwa Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi huchangia kugawanya na kudunisha kwa kueneza kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya?

ii) Sitiari za Kiswahili zina mchango mkubwa katika kueneza kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya ni gani?

iii) Lugha ya Kiswahili inaweza kutumiwa kama chombo cha kuleta uwiano wa kijamii nchini Kenya?

## 1.6 Upeo na mipaka

Utafiti huu ulichunguza sitiari za Kiswahili zilizotumika na wanasiasa nchini Kenya kueneza kauli za kichochezi kuanzia Januari hadi Julai mwaka wa 2017. Hii ni kwa sababu kati ya mwezi wa Januari hadi Julai 2017 kulikuwa na ndimi kadhaa za chuki zilizotumiwa na wanasiasa kulenga jamii zilizodunishwa au kudharauliwa. Vilevile hiki kilikuwa kipindi cha kampeni za kisiasa za kuchagua wawakilishi tofauti tofauti wa wananchi akiwemo rais. Utafiti ulichunguza hotuba zao zilizotumia lugha ya Kiswahili na ambazo zilitumia sitiari za Kiswahili ili kubainisha sitiari za kichochezi zilizotumika. Mtafiti aliweka msingi wa uchambuzi wake katika mambo halisi ya kihistoria kuhusu sitiari katika siasa na jinsi imechangia kuendeleza kauli ya kichochezi nchini Kenya.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Sehemu hii tulijadili mada kama vile lugha ya Kiswahili, Sitiari, Vyombo vya habari, vyama vya kisiasa, na wananchi kama viathiriwa huru vinavyochangia kauli za kichochezi katika siasa. Kila mada tumeonyesha umuhimu wake kwa utafiti wetu. Sehemu hii pia itatoa muhtasari wa yaliyoandikwa kuhusu mada hii.

### 1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu viathiriwa huru vinavyochangia kauli za kichochezi katika siasa

### 1.7.2. Sitiari

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo haizidishi utamu wa usemi pekee, bali pia huboresha zaidi jinsi watu hufanya maamuzi baina yao na kufikiria kuhusu mwingiliano wa kijamii. Sitiari zinaweza kufaa kama hekima ambayo huwasaidia watu kuelewa na kuwasilisha mawazo mazito na ya kidhahania kwa kurejelea vitu halisi zaidi na michakato mbali mbali (USHMM, 2013). Kulingana na Kalmoe (2014), kuibuka kwa nguvu za sitiari katika maandishi hutoa ufahamu wa ziada katika lugha za vurugu za kisiasa. Katika jamii nyingi na kwa watu wengi, siasa huonekana mbali, isiyopendeza na tata inayohitaji maarifa makubwa ya kuboresha uelewa. Sitiari za kichochezi hutoa njia rahisi kwa wasomi wa kisiasa na wananchi wa kawaida kurejelea utata wa siasa katika simulizi zinazoeleweka za migogoro na uchokozi (wananchi kwa urahisi wanaweza kuwa na fikra za vita vya masumbwi au hata vita vya bunduki kati ya viongozi wa kisiasa kwa sababu wanaonekana mara kwa mara wakibishana katika taarifa za habari kwenye vyombo vya habari na burudani.

Wakati sitiari nyingi zina nafasi ndogo katika hali halisi ya dunia, sitiari za kichochezi huongeza tishio la vurugu halisi kwa njia ya mauaji, mapigano ya kiraia, mauaji ya kikatili ya kundi la watu na vita kati ya mataifa. Hotuba za kisiasa zisizotabirika pia huongeza athari zake, kama ilivyo katika vipimo vya vyombo vya habari vinavyoonyesha wazi udanganyifu wa vurugu kwenye vyombo vya habari, wakati lugha zenye nia za uchochezi huchukuliwa kama sitiari (Landau, et. al., 2010).

Maoni haya yataufaidi utafiti wangu pakubwa kwa sababu ni bayana kuwa wanasiasa mashuhuri nchini Kenya hutumia sitiari kuchochea jamii zao dhidi ya jamii nyingine wanakotoka wapinzani wao wa kisiasa. Kwa mfano ghasia za baada ya uchaguzi wa mwaka 2007, zilijitokeza kutokana na sitiari zenye chuki zilizoenezwa kupitia vyombo vya habari, wanasiasa na wananchi vilevile.

Kwa mujibu wa Mulokozi na Kahigi (1979), sitiari ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana zingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum iliyokusudiwa

na mtumizi au mzungumzaji. Sitiari kama tanzu zingine za fasihi simulizi ni chombo cha kutolea mawazo ya jamii; kuibua hisia zao na kukuza ari yao ya kisiasa. Wanasiasa walioko katika upinzani aghalabu wametumia tamathali za usemi kama vile vitendawili na mafumbo kuhamasisha na kuwachochea wananchi na kuwaonyesha namna wanavyoendelea kunyonywa na kunyanyaswa na serikali iliyo mamlakani. Waama, upinzani unajitwika jukumu la kuwafumbua wananchi macho na kuikosoa serikali. Ukosoaji huu hujidhihirisha zaidi, punde baada ya uchaguzi ambapo chama kinachopoteza uchaguzi na kukosa fursa ya kuunda serikali, kinajifariji kwa wimbo: 'Mapambano...mapambano... bado mapambano...' Kupitia kwa sitiari, viongozi wanaounda serikali nao kwa upande wao wanauambia upinzani usubiri chaguzi zijazo. Aidha, wanashinikiza wananchi kudai haki zao za kutawaliwa na kuongozwa na viongozi waliowachagua wala si wale waliowakataa kupitia kwa uchaguzi.

Mbali na vitendawili na mafumbo, wanasiasa wametumia sitiari kuwasilisha ujumbe wao wa kisiasa. Wanasiasa wametambua kuwa huu ni utanzu mwafaka wa kutolea ujumbe wao na kuhamasisha umma kuwaunga mkono. Wairagu (2001) anasema kuwa baadhi ya maoni na mawazo, hasa yale yanayolenga hisia za hadhira hufaa zaidi yakitolewa kwa njia ya sitiari na jazanda. Mojawapo ya sitiari inayotumiwa sana katika kumbi za siasa ni: Nyani haoni kundule. Aghalabu methali hii hutumiwa kuashiria ukweli kwamba baadhi ya viongozi ambao daima huwashutumu wenzao kwa uozo huu ama ule; wao wenyewe wanaendeleza au wamewahi kuhusika na uozo ule ule. Tamathali za ufananisho kama vile tashbihi, sitiari, jazanda na tabaini zimetumika kwa mapana na marefu katika kumbi za siasa. Katika matumizi haya, tabia za baadhi ya viongozi zimelinganishwa na wanyama. Kwa mfano, nguruwe ama fisi wametumiwa kudhihirisha ulafi wa baadhi ya viongozi. Baadhi ya viongozi wamelinganishwa na ngiri-mnyama ambaye husahau haraka sana. Neno kinyonga hutumiwa kuashiria viongozi ambao hawana msimamo dhabiti wa kisiasa. Wengine huwaita tikitimaji (water-melon). Hili ni dhihirisho la misimamo ya kuyumbayumba ya baadhi ya viongozi ambayo, aghalabu huwapotosha wafuasi wao. Hali hii imewafanya baadhi yao kulinganishwa na panya vipofu ambao hawatoi mwelekeo ufaao kwa wale wanaowafuata.

Siasa katika nchi mbalimbali, hasua Kenya, hushuhudia malumbano kila mara. Malumbano ya kitamathali yameibuka katika kumbi mbalimbali popote panapopatikana nafasi ya viongozi na

wananchi kutoa rai zao za kisiasa. Baadhi ya kumbi hizo zimekuwa vyombo vya habari kama vile runinga, redio na magazeti. Vile vile majukwaa ya mikutano ya hadhara na hata kwenye mazishi havikuachwa nyuma. Inadaiwa kwamba malumbano ya kitamathali yalichangia pakubwa kutokea kwa machafuko yaliyotishia kuliangamiza taifa hili baada ya uchaguzi wa 2007. Inasemekana matumizi ya maneno kama vile 'kwekwe' na 'madoadoa' miongoni mwa tamathali nyingine, yalichangia pakubwa katika kufurushwa kwa baadhi ya jamii kutoka maeneo fulani ya Kenya. Mchanganuzi mmoja wa maswala ya kisiasa anasema: 'Kwa bahati mbaya, machafuko haya yalibadilisha mwelekeo; mkondo mzima wa kisiasa; maingiliano na mahusiano ya Wakenya na kuacha taathira itakayodumu kwa muda mrefu, hususan kwa watoto walioshuhudia yaliyotokea'. Shida ni kwamba uhasama miongoni mwa viongozi husambaa na kuota mizizi miongoni mwa wafuasi/mashabiki wao ambao hufuata na kuwaamini viongozi wao kama waumini waaminivyo ukweli uliomo kwenye misahafu. Wananchi wanapaswa kuelimishwa kisiasa ili wakatae katakata kuchochewa kisiasa. Elimu hii itawawezesha kukagua maswala ya kisiasa kwa umakinifu, hivyo kuondokewa na upofu wa kuchukulia yote yasemwayo na wanasiasa kama ukweli kutoka juu.

Takwimu zinaonyesha kwamba wasemaji wa lugha za kienyeji, kwa msamiati wao, wana seti ya maandiko ya msamiati yaliyohifadhiwa kwa jamii wanayochukia. Kwa mfano, uchunguzi uliopita unasema kwamba kila wakati jamii inapotaka kuhimiza wenyeji kutatua changamoto fulani au kufikia matarajio ya jamii, wao huwaita kwa kutumia maneno ya dharau kwa jamii lengwa. Jedwali hapa chini linaonyesha baadhi ya misamiati ya chuki ambayo baadhi ya jamii hutumia, ambayo hutumiwa mara nyingi na wanasiasa wakati wa kampeni.

| Jamii | Msamiati ya chuki | Maana yake | Jamii lengwa |
|---|---|---|---|
| Wanga | Omurende | | Watu wote wasiozungumza lugha ya waluhya |
| Maragoli | Omukivala | | Wasioongea kimaragoli |
| Maragoli | Ababo | | Luo |
| Maragoli | Bidugudi | Wale wasioongea vizuri au wasioeleweka wakiongea | Kalenjin |
| Kisa | Abasebe | | Kikuyu |
| Pokot | Kaure | Walafi- wanaopenda kula sana | Luhya |
| Keiyo | Lamindet/Cheplamindet | | Wasioongea Kikalenjin |
| Keiyo | Lemek | | Lugha chafu ya kutaja wasio wakalenjin |
| Bukusu | Omusinde | Wasiotahiriwa | Luo |
| Kikuyu | Kihii | Wasiotahiriwa | Luo |
| Luo | Jo Rabuon | Wakulima wa viazi | Kikuyu |
| Bukusu | Banyolo | Waoga- wasiotahiri | Luo |
| Luo | Jo Got | Wanaoishi mlimani | Kissi |
| Kikuyu | Mode wa Nyuba | Mtu kutoka kabila letu | Wasioongea Kikuyu |
| Luo | Ja Dhot | Mtu kutoka kabila letu | Luo |
| Luo | Ja Tol | Mwenye Kamba | Kamba |
| Luo | Bimbe | Nyani | Kikuyu |
| Kissi | Ekenyambi | Magugu makaidi | Wasioongea kwa lugha ya Ekegusi |
| Swahili | Madoadoa | Alama ambazo hazitakikani na zinapaswa kuondolewa | Wale wasiotoka kwenye jamii iliyoanza kuishi mahali kitambo au wanaotoka kwa kabila lingine. |
| Kalenjin | Kekoyok | Ukoo au jamaa wa mbali | Kikuyu |
| Luo | Onagi | Waliong'olea meno | Luo |
| Kalenjin | Kaamama | Kazaliwa na mjomba | Kikuyu |
| Meru | Kiiji | Mvulana ambaye hajatahiri | Luo |

Kwa mujibu wa Odiwuor (2002), lugha za kiasili na hasa utumiaji wa sitiari ni silaha yenye nguvu ambayo inaweza kutumiwa na kikundi kimoja ili kuonyesha ubabe wao au kuendeleza mitindo ya uongozi fulani kwa nia ya kuimarisha umaarufu wao. Uteuzi wa maneno unaweza kutumika kwa ufasaha kuibadilisha tabia, matendo na mtazamo wa watu. Kwa kufanya hivyo, misamiati hiyo inaweza kutumika kudhalilisha au kuboresha hali ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Viongozi wa kisiasa wana ushawishi mkubwa kwa jamii na wengi wa wafuasi wao wanaamini kile wanachosema. Hii inaonekana wazi kwenye matokeo ya vitendo fulani vinavyotokana na maneno fulani yanayohusiana nao na ambayo huunda msingi wa imani yao ya kisiasa ambayo hayabadiliki.

Baadhi ya maneno yaliyotumiwa na jamii mbalimbali kwa kutaja mambo na ambayo yamekuwa yakitumiwa katika hotuba ya kisiasa katika kufanya hotuba ya chuki ni kama yafuatayo: Katika lugha ya Wanga, *Omurende* hutumiwa katika hotuba ya kisiasa kwa maana ya watu wote wasioongea kiluhya. Katika Maragoli, neno *Omukivala* linatumika kuelezea wasemaji wote wasiokuwa Maragoli, neno *Ababo* linatumika kuelezea jamii ya Luo, wakati neno *Bidugudi*, ambalo linamaanisha wale wasiozungumza kwa usahihi, hutumiwa kuelezea Kalenjin. Katika kabila la Kisa, neno *Abasebe*, linatumiwa kumaanisha wakikuyu wakati jamii ya Pokot hutumia neno *Kaure*, ambalo lina maana ya watu wenye tamaa au wale wanaopenda kula, kutaja waluhya. Katika Keiyo, neno *Lamindet/Cheplamindet* linamaanisha wote wasio wakalenjin wakati huo huo *Lemek* hutumiwa kidharau kutaja wasio wakalenjin.

Vivyo hivyo, Bukusu hutumia *Omusinde*, ambalo lina maana ya kutahiriwa na *Banyolo*, ambalo lina maana ya woga au wale ambao hawajatahiriwa, kuelezea wajaluo. Jamii ya Luo hutumia *Jo Rabuon*, maana yake wale wanaopanda viazi, kuelezea wakikuyu; *Jo Got*, kumaanisha wale wanaoishi milimani, kutaja Wakisii; *Ja Dhot*, ambalo lina maana ya mtu kutoka kabila letu kuelezea wajaluo; *Jo Tol*, kumaanisha watu walio na kamba, kuashiria wakamba; *Bimbe*, ambalo linamaanisha nyani kuelezea wakikuyu; na *Onagi*, maana wale ambao meno yao ya chini yameng'olewa ili kuashiria wajaluo. Jamii ya Kikuyu kwa upande mwingine hutumia neno *Kihii* katika lugha yao, ambalo lina maana kwamba wasiotahiriwa kuelezea wajaluo na wakati wanapotumia *Mode wa Nyuba*, ambalo lina maana mtu kutoka kabila au nyumbani, kuelezea wakikuyu. Wakisii hutumia *Ekenyambi* ambalo lina maana ya magugu makaidi, kuelezea jamii

zote zisizokuwa Ekegusi. Jina la Kiswahili *'Madoadoa',* ambalo linamaanisha alama zisizohitajika ambazo zinahitaji kuondolewa, limetumiwa na wanasiasa kuhamasisha jamii zao dhidi ya watu wengine wasio wa asili au wale ambao sio wa jamii yao. Jamii ya Kalenjin inatumia *Kekoyok,* ambalo linamaanisha uhusiano wa mbali kuashiria wakikuyu; *Kaamama,* ambalo lina maana ya kuzaliwa na mjomba wake pia kutaja wakikuyu. Hatimaye, Wameru wanatumia neno *Kiiji,* ambalo linamaanisha kijana asiyetahiriwa, kuelezea wajaluo.

### 1.7.3 Lugha ya Kiswahili

Nchini Kenya, lugha ya Kiswahili hutumika kama lugha rasmi na lugha ya kitaifa. Hii ina maana ya kuwa Kiswahili kinachangia pakubwa katika mawasiliano ya kila siku nchini Kenya. Katika jamii ambazo zimeundwa kwa vikundi vingi vidogo vya kikabila kama vile Kenya, wanasiasa wana mazoea ya kutumia lugha ya Kiswahili kama mojawapo za lugha ambazo zinaeleweka na watu wengi nchini kuwavutia jamii zao kuwapigia kura au kusaidia ajenda zao za kisiasa. Mara nyingi, wanasiasa hutumia hali ya kuwepo kwa lugha ya kiswahili kuongoza na kuelekeza jamii ya kabila moja dhidi ya mpinzani mwingine ambaye huweza kuwa anatoka katika kundi la kabila tofauti. Misingi mingine ya kimuktadha ambayo ni muhimu ni mazingira ya kawaida ambayo hotuba hutolewa. Kauli ya kichochezi, propaganda na uchochezi mara nyingi hutegemea ishara, lugha ya Kiswahili na lugha zilizokopwa ambazo misingi yao imo ndani ya miktadha ya kihistoria na kiutamaduni ya eneo maalum. Vyama vinavyofanya uchunguzi kwa nje kuhusu hotuba za hatari vyaweza kupuuza ishara hizi za onyo ikiwa havielewi eneo hilo vyema (Oyeniyi, 2011)

Mfumo wa tahadhari wa mapema hauwezi kutegemea kuchambua hotuba peke yake. Kuna baadhi ya mambo ya mazingira na miundo ndani ya jamii- kama vile historia ya vurugu, kubaguliwa kwa makundi fulani na chuki ambayo inaweza kuunda masharti ya kufanya kauli ya kichochezi kuwa na uwezekano wa kusababisha vurugu katika jamii zilizopangika kutokana na uwezo wa kiuchumi, uongozi uliotawalwa na sheria duni, vurugu zilizofadhiliwa na serikali, ufidhuli au ufisadi ulioenea. Ni hatari hasa wakati ambapo maoni ya wananchi hayatakikani na hakuna maoni badala yanayopendekezwa (Kalmoe, 2014).

Mawazo ya (Oyeniyi, 2011) na (Kalmoe, 2014) yanafaa kwa utafiti wangu kwa sababu nchini Kenya wanasiasa karibu wote hutumia lugha ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na lugha zao za kiasili wakiwaomba watu wao kura. Kwa mfano kampeni za Urais za mwaka huu katika mrengo wa Nasa na Jubilee zinaendeleza matumizi ya lugha za Kiswahili katika maeneo yao. Mara nyingi lugha ya Kiswahili na lugha zingine wanazotumia huwa na kauli za kichochezi zinazoshambulia wapinzani wao na jamii zao.

### 1.7.4 Vyama na viongozi wa kisiasa

Katika demokrasia zinazopendwa duniani kote, vyama vya kisiasa na viongozi wa kisiasa mara kwa mara hushiriki katika matamshi ambayo mara nyingi huchukuliwa kama kauli za kichochezi kwa sababu ya uchaguzi wa maneno na tamathali za usemi. Kwa mujibu wa Kalmoe (2014), viongozi wa kisiasa kwa kawaida hutumia maneno ya "mapigano" katika siasa; kwa mfano, akiahidi "kupambana" kwa ajili ya maadili, kutangaza "vita" kwa matatizo mengi ya kijamii na "kupambana" na matatizo katika jamii yanayohitajika kushughulikiwa kwa haraka. Sitiari hizi zenye kauli za kichochezi hutumika katika uwanja mkubwa wa kisiasa kutoa matangazo ya kampeni na hotuba ya rais, katika barua pepe za wanamapinduzi na kutangaza habari za kisiasa. Mifano mbali mbali inapatikana katika hotuba mashuhuri ya kisiasa kule Marekani pamoja na FDR`S fireside chats, LBJ`S "Great Society", Bryan`s "Cross of Gold", na Lincoln`s "House Divided" (Bougher, 2012). Mifano hii inaonyesha kiwango cha ushawishi na mchango ambao vyama vya kisiasa huwa navyo kwa kauli ya kichochezi katika siasa duniani kote.

Mawazo haya ya (Bougher, 2012) na (Kalmoe, 2014), yanafaa utafiti wangu kwa sababu nchini Kenya vyama na viongozi wa kisiasa, hutumia maneno yanayoweza kuleta vurugu nchini. Kwa mfano, Johnstone Muthama, Moses Kuria, Junet Mohammed na wengine wa Pangani sita walipatwa na hatia ya kauli ya kichochezi na kutiwa mbaroni. Hata hivyo walitetewa na viongozi wa vyama vyao ili wasihukumiwe. Hii inaonyesha kwamba vyama na viongozi wa kisiasa huwa tayari kila wakati kutetea na kupigania mmoja wao hasa apatikanapo kwenye hatia ya uchochezi. Hii ndio sababu kauli za kichochezi huendelezwa kila uchao.

### 1.7.5 Vyombo Vya Habari

Vyombo vyote vya habari vya kitaifa na kimataifa ni nguvu za uzalishaji wa matukio ambayo vinasimulia; jinsi matokeo huelezwa, wakati yanapojitokeza, na sauti za kina nani zapaswa kujumuishwa huweza kubadilisha mkondo wa vurugu. Zaidi ya hayo, teknolojia mpya imewezesha sauti mbali mbali kuibuka na kuboresha usambazaji wa ujumbe ambao umetoa changamoto zote pamoja na nafasi za ajira. Kuipa lugha kipaumbele ni muhimu sio tu kwa ajili ya uelewa wakati vyombo vya habari vinapopiga chuku maelezo yao kimakusudi ili kuzidisha uhasama, lakini pia kwa kuelewa jinsi vyombo vya habari vinaweza kuathiri matukio katika mwendo wa mara kwa mara kazini (Tulkens, 2013). Mara nyingi vyombo vya habari havichunguzi tu bali pia huathiri sana mienendo ya vita, na athari yenyewe huweza kuwa nzuri au mbaya. Katika utafiti wa kila hali uliowasilishwa katika kongamano, kulikuwa na mifano ya waandishi wa habari shupavu ambao walihatarisha maisha yao, na katika matukio mengine, walipoteza maisha yao katika harakati zao za kuripoti kwa utaalamu mkubwa. Kwa upande mwingine, tafiti hizi pia zilibaini kwamba ukosefu wa uwajibikaji au uchunguzi hasi wa habari kutoka kwa vyombo vya habari vya ndani na vya nje vinaweza kuongeza vurugu. Hii inaweza kuwa hatari hasa wakati kauli za kichochezi zinahusika (Sharon, 2013).

Mawazo ya (Tulkens, 2013) na (Sharon, 2013) ni muhimu kwa utafiti wangu kwa kuwa, nchini Kenya, vyombo vya habari huchangia pakubwa kueneza kauli za kichochezi. Hii hutokana na kuripoti kauli za kichochezi punde tu zinapotamkwa na wanasiasa. Vyombo vya habari hasa za lugha za kiasili huweza kutetea kiongozi kwa kushikilia msimamo wa kiongozi husika hata ikiwa mawazo yake yana nia ya kuleta vurugu.

### 1.7.6 Wananchi

Wananchi wana nafasi muhimu wa kutoa mchango wao kuhusu kauli za kichochezi katika siasa. Wananchi walio katika chama chochote cha kisiasa au wanamfuata mgombea fulani wa kisiasa huwa na uwezekano mkubwa wa kupongeza na kupokea kauli yoyote ya kichochezi inayoenezwa na mgombea wao kutoka chama chao cha kisiasa, hasa ikiwa wanahisi kwamba watu wengine au jamii ya makabila fulani imewanyanyasa kisiasa kupitia kwa njia ya kubaguliwa kiuchumi au uteuzi wa nyadhifa za kisiasa. Maoni ya wananchi mara nyingi

huongozwa na maoni ya viongozi. Isitoshe, wananchi hufuata vyanzo vya habari vya kuaminika, katika kudhibiti ushawishi wa mawasiliano wa kisiasa. Kwa mujibu wa Bekoe (2010), vurugu za uchaguzi zinazojitokeza mara kwa mara barani Afrika zinahusu masuala ambayo misingi yao imo ndani ya malalamiko na matatizo kuhusu jinsi jamii ilivyopangwa kutokana na uwezo wa kiuchumi ambayo yanajitokeza kupitia mivutano juu ya haki za kumiliki ardhi, ajira na kubaguliwa kijamii. Wakati wananchi wanachangia kuendeleza ghasia za kisiasa na kukubali kauli za kichochezi katika siasa, wanaweza kujenga mazingira hatari ya kisiasa ambayo huweza kuwaruhusu wengine kusababisha vurugu. Hata wakati wananchi wengine hawataki vita, wananchi ambao hufurahia hali hiyo ya vita huweza kuhimizwa na mazingira yanayoruhusu vita na kusababisha ghasia ili kukubiliana na matokeo ya kisiasa yasiyopendeza. Demokrasia hutegemea kupata suluhu ya migogoro kwa njia ya amani na huzuiliwa wakati viongozi na wananchi wameshindwa kukana vurugu (Kalmoe, 2014).

Haya mawazo ya Bekoe na Kalmoe yalisaidia utafiti huu sana kwa sababu wananchi hufuata tu wanayoambiwa na wanasiasa kutoka jamii zao. Isitoshe, wananchi huwa tayari kukabiliana na serikali kwa njia ya maandamano ikiwa kiongozi kutoka jamii yao apatikane na hatia ya kueneza kauli ya kichochezi na kutiwa mbaroni. Kwao, hii ni ishara ya unyanyasaji kwa jamii yao.

## 1.8. Nadharia ya utafiti

Utafiti huu ulitumia nadharia ya vitendo usemi. Hili limechochewa na imani kuwa kipengele muhimu katika mawasiliano ni vitendo usemi (Austin, 1962; Searle,1975).

### 1.8.1 Nadharia ya Vitendo usemi (VU)

Hii nadharia huchunguza jukumu la matamko kwa kuyahusisha na tabia ya msemaji na msemewa. Iliasisiwa na Austin (1962) kuonesha kwamba lengo la lugha si tu kuwasilisha taarifa ya mambo yalivyo, bali pia kutenda. Ifuatayo ni mihimili ya nadharia hii tuliyotumia kwenye utafiti wetu. Katika kuchunguza mchango wa sitiari kwenye kauli za kichochezi kwa mkabala wa VU, nia ya msemaji huwa ni jambo muhimu. Kila msemaji huanza kwa kuzingatia mada aliyo nayo akilini ambayo angependa hadhira iielewe. Pasi kuielewa nia ya msemaji, kipashio cha kiisimu hakina maana yoyote ya kudumu (taz. Patte 1988:98)

Kuvielewa VU huhusisha ufahamu wa muktadha. Muktadha wa tamko hudokeza msingi wa maana ya tamko lenyewe. Austin anaashiria jambo hili anaposema "kitendo usemi kamilifu kwenye muktadha kamilifu wa usemi". (1962:147). Muktadha ni jumla ya kanuni zinazoathiri uelewa na uzalishaji wa utendaji wa kiisimu (Bunt 2000:81-82), ama miduara mzunguko ya athari kwenye hali fulani ya mambo (Dijk 2008:4). Bunt (2000:100) anataja mikabala mitano ya muktadha: kiisimu, kisemantiki, kitambuzi, kijamii na kihalisi. Kwenye mchakato wa mawasiliano, inafaa msikilizaji kuelewa mikabala yote ya kimuktadha inayoathiri VU.


VU ni akisiko la mwonoulimwengu. Ingawa muktadha ni muhimu katika kuelewa kitendo usemi, tamko huundwa kwa kuzingatia mwonoulimwengu. Isitoshe, VU huundwa kijamii na ni vya utoano. Kwa kuchunguza VU vya jamii maalum, zipo ruwaza zinazojitokeza kubainisha maelezo, marekebisho au udhibiti baina ya wanajamii wake. La muhimu ni matamko ambayo jamii huyatumia kueleza uhalisia wauonao kama jamii wala si uhalisia wenyewe (Petrey 1990:40-41; Esterhammer 1993:288). Kanuni za kijamii huwezesha VU kufanyika (Briggs, 2001:63-67). Nadharia hii hudhihirisha kuwa jamii ni ya kifasiri na inakomazwa kwa lugha (VU) kushughulikia kuwepo kwake duniani na kwenye dunia yake (Verhey 2007:22-23).

Jukumu la msemewa hupewa kipaumbele kwa kuwa VU huwa na msemaji na msemewa. Lengo la kimsingi la kusema ni kuwasilisha nia (Bach na Harnish, 1979:3). Katika nadharia ya VU, msisitizo mkubwa umekuwa kwa msemaji. Hali hii ni ya kusikitisha kwa kuwa, jukumu la msemewa hudunishwa hadi anapewa tu dhima ya kuwa kama kifaa cha kuitikia (Gorman 1999:102-103; Masaki 2004:34-36). Kwa kuchunguza mawasiliano kisafu, msemaji hudhibiti matamko, msemewa akiwa tu kupokea jinsi inavyojitokeza katika kielelezo 1.1

Msemaji ——→ tamko ——→ msikilizaji

Upo utegemeanno baina ya msemaji, msemewa na tamko. Ni muhimu kuzingatia lengo la kutamka. Hili huwa ni msemewa kufasiri na kutekeleza vilivyo tamko (Holdcroft, 1978:70-71; Bach na Harnish, 1979:17; Gu 1993:422; Masaki 2004:35). Watu hutumia lugha wakiwazia hadhira yao (Clark na Carlson 1982:342). Ilokusheni ni sehemu tu ya hali jumla ya usemi, ambamo msemewa huhusishwa kikamilifu kwa sababu ya kutambuliwa kutokana na lugha na muktadha katika huo wavu wa mahusiano (Petrey 1990:89). Ili ilokusheni kufanikiwa, sharti


pawe na kukubaliana baina ya pande zinazohusika (Hornsby, 1994:198-207). Ingawa msemaji ndiye chanzo cha tamko, msemewa ana jukumu kwa tamko na kwa msemaji katika muktadha wa kitendo usemi. Ikiwa atatambua NI, yeye ndiye chanzo cha kufasiri tamko kudhihirisha kuelewana (Kissine, 2009:128-134). Kwenye kielelezo hiki tunaonesha utegemeano huu;




Nilitumia nadharia hii katika kutambua na kuainisha VU mbalimbali vilivyomo kwenye sitiari za Kiswahili zilizotumika na wanasiasa katika kampeni zao kabla ya kuonyesha jinsi zinavyoendeleza kauli ya kichochezi nchini Kenya.

## 1.9 Misingi ya nadharia

**Kielelezo 1.1: Misingi ya nadharia**




Misingi hii ya nadharia inaeleza uhusiano baina ya viathiriwa vinavyojisimamia kama vile sitiari ya Kiswahili, lugha ya kiswahilina viathiriwa tegemezi, yaani kauli ya kichochezi katika siasa. Matumizi ya sitiari, hasa zile za kivita na wanasiasa wakati wa kampeni huchangia pakubwa katika kauli za kichochezi. Kulingana na asili ya kisiasa nchini Kenya, ambayo aghalabu huchukua msingi wa kikabila, matumizi ya lugha yaKiswahili na wanasiasa katika harakati zao za kuomba kura kwenye maeneo yao dhidi ya wapinzani wao, huchangia pakubwa katika kauli ya kichochezi kwa sababu baadhi ya maneno yakitafsiriwa, huweza kuonekana kama matusi kwa jamii nyingine. Vile vile, lugha chafu zinazotumika na wanasiasa kudunisha au kuwapuuza wapinzani wao wakati wa kampeni pia zina mchango mkubwa kwenye kauli ya kichochezi. Hii inaonyesha kwamba viathiriwa hivi vitatu vinavyojisimamia vina mchango kwenye kauli ya kichochezi, hasa nchini Kenya. Isitoshe, vyombo vya habari, vyama vya kisiasa, wanasiasa, na wananchi, pia wanachangia sana kuzidisha kauli ya kichochezi katika siasa nchini Kenya kwa kuwa vyombo vya habari huripoti kauli za kichochezi punde tu zinazotamkwa na wanasiasa, vyama vya kisiasa huunga mkono wanasiasa katika vyama vyao, na wananchi pia hukubali na kuamini wanayoambiwa na wanasiasa dhidi ya watu wengine au jamii nyingine.

## 1.10 Muhtasari wa yaliyoandikwa kuhusu mada hii

Yaliyoandikwa kuhusu mada hii yamebainisha kwamba sitiari ya Kiswahili pamoja na sababu nyingine kama vile lugha ya Kiswahili inachangia katika kauli ya kichochezi katika siasa. Hata

hivyo, uchambuzi wa yaliyoandikwa kuhusu mada hii umedhihirisha kwamba uchambuzi haba umefanywa katika muktadha wa mazingira ya kisiasa nchini Kenya. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kulipunguza ikiwa si kuliziba pengo hilo la kiusomi kwa kuchambua mchango wa sitiari za Kiswahili na sababu nyingine katika siasa nchini Kenya. Hivyo basi, utafiti huu ulikuwa tofauti na tafiti za awali kwa sababu ulichunguza malengo ya ziada huku pia ukichambua kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya.

### 1.11 Njia za utafiti

#### 1.11.1 Uteuzi wa sampuli

Utafiti huu ulinuia kuchunguza matamshi ya wanasiasa ili kuteua sitiari za Kiswahili zilizotumika kwa njia ya kiuchochezi. Matamshi yaliyolengwa ni yale yaliyotolewa katika mikutano ya kampeni za kisiasa na kunadi sera kwa wananchi. Sampuli hii ya kuteua sitiari za Kiswahili hasa ililenga sana maeneo ambayo wanasiasa walio na ushawishi na ufuasi mkubwa kama ilivyo katika maeneo wanakoungwa mkono. Niliteua matamshi ya wanasiasa kuanzia Januari hadi Julai mwaka wa 2017. Hii ni kwa sababu kati ya mwezi wa Januari hadi Julai 2017 kulikuwa na hali ya juu ya kisiasa na ndimi kadhaa za chuki zilizotumiwa na wanasiasa kulenga jamii zilizodunishwa au kudharauliwa. Vilevile hiki kilikuwa kipindi cha kampeni za kisiasa za kuchagua wawakilishi tofauti tofauti wa wananchi akiwemo rais. Sampuli yangu pia ilijikita katika maeneo mbalimbali kote nchini. Uteuzi wangu ulitegemea vikundi viwili yaani kundi jaribiwa na kundi la kudhibiti. Kundi jaribiwa ndilo ambalo hupokea athari, ilhali kundi la udhibiti halipokei athari. Hii iliniwezesha kukusanya data na kufanya uamuzi kuhusu athari husika.

#### 1.11.2 Eneo la utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika muktadha wa kauli ya kichochezi katika siasa nchini Kenya. Majarida ya kiakademia kama Mwanga wa Lugha zilizochapishwa hivi karibuni zinazoangazia sitiari za Kiswahili na michango yao katika kauli ya kichochezi katika siasa, hasa katika muktadha wa Kenya zilikuwa nyenzo muhimu kwa ajili ya data ya sekondari kwa ajili ya uchambuzi wa kimaelezo katika utafiti huu. Mtafiti aliteua Kenya kama sehemu mwafaka wa

utafiti huu kwa sababu anaishi na kusoma nchini Kenya, na hii ina maana kwamba anaelewa mienendo na matendo ya kauli za kichochezi nchini Kenya.

### 1.11.3 Idadi ya watu inayolengwa

Mchango wa sitiari za Kiswahili kwenye kauli za kichochezi nchini jinsi zilivyoangaziwa katika tafiti zilizotangulia pamoja na maandishi muhimu na yanayohusiana na mchango wa sitiari za Kiswahili katika kauli ya kichochezi katika siasa ambayo yamepitishwa hivi karibuni yalitumika. Kenya imepitisha sheria zinazofafanua kauli za kichochezi na kulinda sera na mienendo inayotumiwa na wanasiasa katika kampeni zao. Kenya pia iliunda taasisi mbalimabali kama vile Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano (NCIC), na Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano ili kuendeleza amani, uponyaji wa kitaifa na maridhiano kati ya watu wa Kenya. Mtafiti alichunguza jinsi sitiari za Kiswahili hutumiwa na wanasiasa kueneza kauli za kichochezi nchini Kenya.

### 1.11.4 Mbinu za ukusanyaji wa data

Mtafiti alitumia data za sekondari zinazopatikana kwenye vitabu, ikiwa ni pamoja na majarida ya kitaaluma kama Mwanga wa Lugha ambalo lilichapisha makala kuhusu mchango wa sitiari za Kiswahili katika kauli ya kichochezi kwenye siasa nchini Kenya. Data za sekondari zilizokusanywa zilitegemea malengo mahususi ya utafiti ambayo yalitilia mkazo vifaa vyenyewe vinavyolenga makisio ya utafiti. Mtafiti pia alilenga kutumia data za sekondari zilizochapishwa katika siku za hivi karibuni kama Mwanga wa Lugha ili kupata mawazo mapya kuhusu mada iliyotafitiwa. Hii ilihakikisha kwamba data za sekondari zilizokusanywa si za zamani na zinafaa utafiti wetu. Isitoshe, mtafiti alitazama video kama njia ya kukusanya data msingi. Mbinu niliyotumia kukusanya data ni kutazama video kutoka kwa mtandao wa youtube pamoja na kusoma vitabu na majarida kama Mwanga wa Lugha yaliyochapisha makala kuhusu jinsi sitiari za Kiswahili hueneza kauli ya kichochezi.

### 1.11.5 Mbinu za uchanganuzi wa data

Data zilichanganuliwa kwa kutumia njia ya takwimu elezi iliyohusu kutoa mifano, kufafanua na kutoa maelezo kwa kuyahusisha na malengo ya utafiti na nadharia ya vitendo usemi. Kwa kila nadharia tete, mtafiti alitumia njia tofauti katika uchanganuzi wa viathiriwa na mahusiano yao.

Muhtasari wa uainishaji wa data ulitokana na malengo ya utafiti. Uchanganuzi zaidi wa data uliimarishwa kwa kuweka data zilizokusanywa pamoja. Mtafiti aliihakiki data ili kuepuka makosa, kuhakikisha usahihi, ukamilifu, ubora, na kuhakikisha mfululizo wa data zilizokusanywa. Takwimu za kiuelezi zilitumika katika uchambuzi, ili kusaidia katika kutoa matokeo ya malengo ya utafiti huu.

### 1.11.6 Uwasilishaji wa data

Data ziliwasilishwa kwa kutumia takwimu elezi za uhusiano. Nilitumia uchunguzi wa kimantiki kutambua kama kuna uhusiano baina ya vijaribiwa vinavyofanyiwa uchunguzi. Kwa muhtasari, sura ya kwanza ilishughulikia usuli wa mada, tatizo la utafiti, mbinu za ukusanyaji wa data pamoja na kuwasilishwa kwao. Sura ya pili, tatu, nne na tano pia zilitumika katika kuwasilisha data. Sura ya pili ilishughulikia aina mbalimbali za sitiari pamoja na dhana muhimu katika nadharia ya VU ambazo zilikuwa na umuhimu kwenye utafiti huu na sura ya tatu imechanganua data zilizoteuliwa kwa kutumia nadharia ya VU. Sura ya nne imetoa matokeo kutoka kwa data zilizochanganuliwa. Hatimaye, sura ya tano imejumuisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

### 1.11.7 Uhalali wa kuaminika

Ili kufikia maudhui ya kihalali, mtafiti alihakikisha kwamba data za sekondari zilizokusanywa zilitoa taarifa muhimu zinazopimika kuhusu mchango wa sitiari za Kiswahili katika kauli ya kichochezi katika siasa. Ili kupima uhalali wa maudhui, mtafiti alihakikisha kwamba hakukuwa na tofauti katika kulinganisha data mbalimbali zilizokusanywa, na data hizo za sekondari zilikuwa katika hali ambayo inakubalika kwa ajili ya utafiti. Ili kupima uhalali wa ndani, mtafiti alihakikisha kwamba viathiriwa huru ni thabiti katika kuonyesha matokeo yao kuhusu mchango wa sitiari za Kiswahili katika kauli ya kichochezi kwenye siasa jinsi ilivyotolewa na data za sekondari zilizokusanywa nchini Kenya. Ili kuonyesha kiwango cha uhalali, Mtafiti alilinganisha usahihi wa utafiti huu na matokeo mengine yaliyohalalishwa na uthabiti katika mbinu ya mapito ya maandishi yaliyochunguzwa. Mtafiti alipima uaminifu wa mbinu ya mapito ya maandishi katika chuo kikuu kwa kuiwasilisha mbele ya jopo la wahadhiri wa chuo, na wasimamizi wa utafiti ambao waliihalalisha kabla ya utafiti halisi. Aidha, mtafiti alihakikisha uaminifu kwa kuhakikisha kwamba data za sekondari zilikusanywa kutoka kwa machapisho yaliyohalalishwa,

majarida ya kitaaluma na karatasi za utafiti zilizofanywa katika kipindi hiki cha kisasa kisichozidi miaka kumi kuanzia sasa na kwamba hakukukuwa na mabadiliko makubwa katika matokeo haya kuhusu mchango wa sitiari za Kiswahili katika kauli ya kichochezi kwenye siasa.

### 1.11.8 Maadili ya utafiti yanayohitajika

Mtafiti alipata kibali kutoka kwa chuo kikuu kabla ya kuanzisha uchunguzi wa ukusanyaji wa data kwa kujaza na kuwasilisha fomu ya maombi ili kupata idhini ya kufanya utafiti ulioandaliwa na kamati ya maadili ya lugha chuoni. Data zote za sekondari zilizokusanywa kwa ajili ya utafiti huu utapatikana kwa urahisi katika mtandao wa youtube, vitabu, majarida ya kitaaluma na maandishi mengine. Ni mtafiti mwenyewe ndiye alikuwa na uwezo wa kufikia data zilizokusanywa, mahali pa kuhifadhi, na uchambuzi wa data. Mtafiti hakuhifadhi data zisizofaa kwa ajili ya utafiti huu. Data zilizofaa kukusanywa kwa ajili ya utafiti huu zilichunguzwa kwa njia na haki zilizofaa kwani mtafiti alizitumia kwa madhumuni yaliyolengwa. Mtafiti alizingatia maadili yote yanayohitajika kwa ajili ya kufanya utafiti huu jinsi ilivyoidhinishwa na wasimamizi na chuo.

# SURA YA PILI

# AINA MBALIMBALI ZA SITIARI NA DHANA MUHIMU KATIKA NADHARIA YA VITENDO USEMI

## 2.0 Utangulizi

Kwenye sura hii nilishughulikia aina mbalimbali za sitiari pamoja na dhana muhimu katika nadharia ya VU ambazo zina umuhimu kwenye utafiti huu. Nilianza mjadala wangu kwa kuangazia maana ya sitiari.

## 2.1 Maana ya sitiari

Hii ni tamathali ya usemi ambayo kwayo neno ambalo mara nyingi huhusishwa na kitu fulani hutumiwa kufafanua kitu kingine tofauti (Abrams, 1999). Wasemavyo Lakoff na Mark Johnson (1980) katika (Elhindi, 2009), sitiari huwa zimesimikwa sawasawa kwenye akili na matendo yetu pamoja na lugha ya kila siku.

Ni wazi kwamba maana ya kisitiari hutegemea vipengele vya kipragmatiki pamoja na kukisia kwamba fenomena za kisitiari zinakubalika katika nadharia ya kipragmatiki kwa urahisi. Ni kwa sababu hii nadharia ya VU, imewachochea wataalamu wengi kuchunguza sitiari kama tamathali ya usemi katika fasihi ambayo inadhihirisha matumaini makubwa ya ufanisi. Rybarkiewicz (2002) anaiona sitiari kama mojawapo ya vitendo usemi vya ilokusheni. Rybarkiewicz (2002) akimnukuu Warner (1973) anasema mradi tu sitiari iko hai, huwa na nguvu fulani za kisitiari ambazo sharti zichukuliwe kuwa ni za kiilokisheni. Vilevile anawataja Cormac na Earl (1990) kama waitifaki wa Vu vya kisitiari. Kulingana na Cormac na Earl, inafaa nadharia hii ipambanue aina ya kitendo usemi ambacho sitiari inayohusika hukitenda. Kwa mtazamo wa VU, sitiari ni vitendo ambavyo huibua mshtuko, kuzalisha utata wa kisemantiki na kujenga hisia mbalimbali ndani yetu. Ni (nguvu ilokusheni) za sitiari huwa “kile sitiari hutenda” wala si kile wasemaji hutenda. Hii ina maana kwamba, inafaa msikilizaji azingatie Vu vya kisitiari kwenye tafsiri. Matendo ya sitiari kwenye usemi huwa ni kumtazamisha msikilizaji kwenye usemi unaohusika kuzingatia ulinganishi wa hali au muktadha fulani. Kwa mfano mvua kwa kawaida huashiria kitu kinachorutubisha hivyo kuhusiana moja kwa moja na uhai na maji. Vile vile mvua huhusishwa na usufi kwa imani kuwa mvua hupusa kutoka mbinguni. Wakati mwingine, vigezo vya mvua

ambavyo hutumiwa sanasana na wanasiasa vinahusu athari zake; mvua kama mateso au bahati mbaya. Mvua huwa aina ya sinekidoki ya aina mbaya ya hali ya anga hivyo basi kuashiria matukio yoyote hasi maishani (Ferber, 2007).

Kwa mujibu wa Mulokozi na Kahigi (1979), sitiari ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana zingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum iliyokusudiwa na mtumizi au mzungumzaji.

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo haizidishi utamu wa usemi pekee, bali pia huboresha zaidi jinsi watui hufanya maamuzi baina yao na kufikiria kuhusu mwingiliano wa kijamii. Sitiari zinaweza kufaa kama hekima ambayo huwasaidia watu kuelewa na kuwasilisha mawazo mazito na ya kidhahania kwa kurejelea viti halisi zaidi na michakato mbalimbali (USHMM, 2013).

Kulingana na wasomi mbalimbali, kuna aina nyingi za sitiari ambazo aghalabu hutumika kwenye usemi. Baadhi zao ni kama zifuatazo; Kwanza, Sitiari kuu. Hii ni aina ya sitiari ambayo hutawala kazi ya kifasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Sitiari ya aina hii hurudiwarudiwa au kurejelewa na mtunzi kila mara na hujitokeza kuwa motifu. Jukumu la sitiari kuu ni kuwasilisha dhamira na maudhui ya kazi ya kifasihi. Kwa hali hii, sitiari ya aina hii huwa muhimu katika kuifasiri kazi inayohusika. Sitiari za aina hii ni nyingi katika tenzi za kiswahili. Mfano mzuri katika siasa ni sitiari ya simba wakati wanasiasa wengine wanajisifu kwa kusema 'ndimi simba maarufu' kumaanisha wao ni wakali na jasiri kama simba. Mifano mingine inapatikana katika mashairi huru ya Kithaka wa Mberia, Bara Jingine mfano, neno nyuki limetumiwa kama sitiari ya waafrika ambao waliungana na kujikomboa lakini baadaye wakapoteza umoja wao na hivyo kuzuia kupatikana kwa maendeleo barani Afrika (Lugwiri 2009).

Aina ya pili ni Sitiari Sahili. Aina hii ya sitiari huwa nyepesi na rahisi kueleweka na hadhira. Hii ni kwa sababu ulinganishi wake ni wa moja kwa moja. Mfano tuliotoa wa 'Ndumbu ni Yesu' ni aina ya sitiari sahili na ambayo ni rahisi kueleweka kutokana na sifa za Yesu kuwa mkombozi, mwenye utu, mpole na mpenda amani. Mifano zaidi ni kama ujana ni moshi, yeye ni 'sungura', mimi ni 'kinyonga' kumaanisha tabia ni kama za mnyama anayetajwa. Katika siasa za Kenya kuna viongozi mbalimbali ambao hujisifu kwa lakabu kama vile 'Agwambo' kumaanisha mtu

wa ajabu, 'Tinga' kumaanisha mtu mwenye nguvu au bidii kwenye kazi yake, 'Nyundo' kumaanisha mtu mwenye hufichua ukiukaji wa sera za kijamii na uongozi mbaya wa serikali bila woga.

Aina ya tatu ni Sitiari Chakavu. Kulingana na Murray (1978:85), uchunguzi wa sitiari chakavu katika lugha unaweza kutueleza kuhusu maisha ya kijamii na ya kihistoria ya jamii fulani. Naye Abrahams (1957:64) anaeleza kuwa sitairi chakavu imetumiwa sana katika lugha kwa kiasi cha kuifanya kutoonekana kama sitairi tena. Sitiari za aina hii huwa zimefungamana sana na matumizi ya kawaida ya lugha na hivyo kupoteza ubunifu wake. Aina hii ya sitiari itumiwapo, huwa haina athari zozote za kisanii kwa hadhira katika lugha ya Kiswahili, mifano mizuri ya sitiari za aina hii inapatikana katika misemo na nahau. Mifano ni kama kiuno cha nyingu, shingo ya upanga, mdomo wa chupa, meno ya msumeno, mkono wa birika, kichwa cha nyoka na kadhalika. Kwenye siasa, wanasiasa wengi hutumia sitiari chakavu kujisifu, kueleza jinsi makabila yao yamepuuzwa au kudunishwa kwa muda mrefu katika ugavi wa rasilimali pamoja na uteuzi wa nyadhifa mbalimbali ya serikali. Vilevile, wanasiasa wengine hutumia sitiari chakavu kudunisha wapinzani wao. Kwa mfano, mara nyingi wanasiasa nchini Kenya wametumia sitiari chakavu; 'Nyani haoni kundule' kueleza wanaowakosoa kwamba hao pia wana dosari zaidi.

Aina ya nne ni sitiari ya usuli. Sitiari za aina hii zinapatikana katika lugha nyingi ulimwenguni. Wamitila (2008:423) anaeleza kuwa sitiari ya usuli ni ''...sitiari ambayo imefungamanishwa na lugha kiasi kwamba watu au wazungumzaji na watumiaji wa lugha hawaiangalii tena kama sitiari au hawafikirii tena kama ni sitiari''. Nyingi ya sitiari za usuli zinapatikana katika utamaduni mahsusi ilhali zingine ni bia, kwa mfano, ''mtihani huu ni 'mboga'' kumaanisha ni rahisi. Akili ni nywele, shilingi ya ua, maisha ni safari, pesa ni maua na kadhalika. Kwa mfano, upinzani nchini Kenya umekosoa serikali kwa utumizi mbaya wa fedha na kuendeleza ufisadi kwa kuita rais 'fisi', 'kichwa maji' na kadhalika.

Tano, sitiari radidifu. Aina hii ya sitiari si rahisi kueleweka kwani kilinganishi, kilinganishwa au msingi haviwekwi wazi bali ni kutokana na maelezo yake ndipo maana ya sitiari hiyo huweza kufasiriwa na kueleweka. Mfano mzuri unapatikana katika Utenzi wa mwana Munga ambapo kulingana na maelezo ya mwandishi, mtunzi alishiriki ngono na mwana Munga kwa

kulinganisha na shughuli za baharini. Pia katika riwaya ya Bin-adamu mbinu hii imetumika kwa wingi. Aina ya sita ni Sitiari ya Kikaida. Kwa kuwa kazi ya fasihi ni zao la jamii, sitiari hii hufungamana na utamaduni wa jamii. Kila jamii au kundi la watu huwa na mambo fulani wanayothamini na hivyo huwa na njia ya kisitiari ya kuyarejelea. Kwa mfano ''mwanamke ni nguo''. Sitiari hii inamaanisha kwamba mwanamke yeyote akipambwa kwa nguo nzuri ata kuwa wa kupendeza au mrembo. Mfano mwingine ni kama elimu ni ngao, kumaanisha ukiwa na elimu una kinga ya maisha kwani unaweza kuajiriwa na kuwa na mali pia unaweza kutumia elimu kujikinga kwa kujieleza. Aghalabu, wanasiasa hupenda kurejelea sitiari ya kikaida kufafanua mambo ya maendeleo katika jamii yao na pia kulaumu wapinzani wao kwa kukaidi tamaduni zao au kutofanya maendeleo.

Aina ya saba ni Sitiari hisimseto. Kulingana na Mutiso (1996), aina hii ya sitiari hutumika kuhamisha hisia za kitu kimoja kwa kitu kingine. Kwa mfano 'Ujumbe Mzito' kumaanisha ujumbe aliobeba ama unaopatikana katika matini fulani una maudhui muhimu. Mifano mingine ni kama 'sauti nyororo' sauti inapewa sifa za wepesi na kuvutia, 'baridi kali', 'upepo mwanana' na kadhalika. Mutiso (1996:123) anaelezea kuwa kawaida 'giza' linahusishwa na uoga, kushindwa, upweke, msiba, mashetani, mizuka, wanyama wala watu, uchawi, ujinga miongoni mwa mambo mengine hasi. Kwa upande mwingine moto unahusishwa na hatari na maangamizo. Nayo baridi inahusihwa na upweke na ukosefu wa furaha.

Aina ya mwisho katika uchambuzi huu ni Sitiari mseto. Huu ni mchanganyiko wa sitiari zaidi ya moja. Sitiari kadha zinaweza kutumiwa pamoja ili kurejelea hali moja. Sitiari hizi huwa tofauti lakini huwa zinachimuza sifa fulani ya pamoja kuhusu kinacholinganishwa kwa mfano: 'Tabia njema ni mzizi mkuu wa fadhila. Unapotaka kutafuta mchumba wa kuoa kumbuka mapenzi ni kikohozi na pia ni majani huota popote. Angalia sana tabia kabla ya kuposa kwani kuingia ni rahisi kutoka ni ngumu'. Katika mfano huu maneno hayo matatu yamelinganishwa ingawa ni tofauti yaani tabia njema, mapenzi kama kikohozi na pia majani. Mathalani mapenzi yamelinganishwa na kikohozi na pia majani. Mke anayechaguliwa anatakiwa kuwa na tabia njema na pia mwenye mapenzi ya wazi ambayo hayafichiki na yanaweza kuota mahali popote na wakati wowote. Kwa hivyo achunge asihadaiwe na mapenzi na kusahau kuangalia tabia.

Niliteua sitiari chakavu kuongoza utafiti wangu kwa sababu, kwenye siasa, wanasiasa wengi hutumia sitiari chakavu kujisifu, kueleza jinsi makabila yao yamepuuzwa au kudunishwa kwa muda mrefu katika ugavi wa rasilimali pamoja na uteuzi wa nyadhifa mbalimbali ya serikali. Vilevile, wanasiasa wengine hutumia sitiari chakavu kudunisha wapinzani wao. Kwa mfano, mara nyingi wanasiasa nchini Kenya wametumia sitiari chakavu; 'Nyani haoni kundule' kueleza wanaowakosoa kwamba hao pia wana dosari zaidi.

### 2.2. Aina ya vitendo usemi

VU huanishwa kutegemea sifa zao, maana zao au muktadha (Wairima, 2009). Kwa mujibu wa Auston, Vu huwa na sehemu tatu- lokusheni, ilokusheni na palokusheni.

#### 2.2.1. Lokusheni

Hili ni tendo la kimsingi la kutamka (unatiki). Lokusheni huwa na vijisehemu vitatu: Kwanza, tendo la kifoni linalohusu utamkaji sauti. Pili, tendo la kifati, linalohusu utamkaji wa sauti za lugha mahususi zinazozingatia sarufi. Sauti zinapochunguzwa kwa mtazamo huu huitwa femu. Tatu ni tendo la kireti, linalohusu kutumia sauti kurejelea na fahiwa fulani. Ni utendaji wa kitendo cha kifoni kwa namna inayokipa kitendo chenyewe maana, ambapo maana hubainika ikiwa kinachosemwa hutibithishwa. Sauti katika mtazamo huu huitwa reme. (Malmkjær, 1995:563; Istomine, 2010:26).

Kuzungumza, kama utoaji sauti unaotawaliwa na kanuni, ni aina ya utendaji. Hata hivyo, lokusheni hazijisimamii. Licha ya kuwa matamko, lokusheni zinatumiwa kuwasilisha nia. Nia hizi huandamana na nguvu ilokusheni (NI), kwa kuwa zinashawishi uelewa wa msikilizaji kuhusu kile msemaji anataka kutekeleza. Utambuzi huu huwezekana kwa sababu ya kuwepo kwa kanuni za kijumla zinazofahamika na wanaohusika wote. Iwapo msikizaji anaelewa anavyopasa kutenda au kujibu, hiyo kauli basi ina MP na NI (Littlejohn, 2009:918). Lokusheni hujumuisha tendo la tamko na tendo la proposisheni.

#### 2.2.2. Ilokusheni

Msemaji anapotamka chochote, huwa ana lengo fulani akilini mwake. Lengo hili ndilo hurejelewa kama ilokusheni. Hii ina maana kwamba ilokusheni ni aina ya jukumu msemaji

analenga kutimiza kupitia tamko lake, linabainikalo kupitia kaida za kijamii (Capone 2009:1015). Majukumu haya huitwa NI au kiini ilokusheni cha tamko. Asemavyo Dijk (1977) ni muhimu kutambua jinsi muundo wa ndani wa utendaji 'wa ilokusheni ulivyo kwa kurejelea ukweli fulani, kwa kulenga proposisheni fulani, kwa kutaja kirai au sentensi fulani, mfuatano wa mofu au fonimu, kwa kutekeleza kitendo fulani cha kifonetiki. Vitendo changamano vilivyomo ndani ya ilokusheni huweza kufaulu ikiwa tamko ni tunu inayokubalika ya aina ya tamko lililolengwa. Hata hivyo, aina hii ya ufanisi ni ya upande mmoja, na sehemu tu ya tendo la mawasiliano: msemaji huwa na majukumu. Yaani hutaka matamko yake yawe na athari mahususi. Athari hizi huhusu msikilizaji kuirekebisha seti yake ya maarifa: msikilizaji hujua kwamba msemaji anatamka /a/, anatamka mofu {kalamu}, n.k. Anajua kwamba msemaji ana maana kwamba kitabu kimepotea 'hivyo basi kurejelea kitabu mahususi, chenye sifa maalum, wakati wa kutamka. Hivyo basi, katika kila kiwango cha kutenda, msemaji ana majukumu yanayowiana na kile msemewa anakitambua. Athari hizi ambazo zinadhamiriwa, katika hali ya kawaida zitaweza kutekelezwa kutokana na hali ya kimawasiliano ya matendo yanayohusika pamoja ya ukaida wa vipashio, kategoria na kanuni za tokeo la tamko lililotekelezwa kikamilifu. Kwa hivyo, tendo la lugha hufanikiwa ikiwa msikilizaji atatambua maana/ urejelezi unaokusudiwa, na ikiwa msemaji alilenga msemewa atambue hivyo.

Wataalamu mbalimbali wameainisha ilokusheni kwa kuzingatia viathiriwa tofauti tofauti. Baadhi huzingatia sifa, wengine maana na sifa huku wengine ikizingatia yote matatu (Wairima, 2009). Msisitiza ambao umetiliwa kwenye ilokusheni umeishia kutumia ilokusheni kama kisawe cha VU. Katika sehemu hii nilijadili baadhi ya mifumo ya uainishaji huo. Nitakaowaangazia ni pamoja na Austin (1962), Searle (1969; 1971; 1975; 1983; 1985). Bach na Hanish (1979), Kreidler (1998), Allan (2000) na Bach (2004).

Akizingatia vitenzi vya kiilokusheni, Austin (1962: 150-163) ameainisha Vu kuwa maamuzi, amri, ahadi, hisia na vifunuzi.

Vendler (1972) ameainisha Vu kwa msingi unaokaribiana na ule wa Austin kwa kuwa Vendler anatofautisha aina mbili ya amri (vidahili na amri za kweli) pamoja na aina mbili za maamuzi (viendeshi na maamuzi ya kweli), uainishaji wake una makundi saba.

Mfumo wa Searle (1969), tunaoweza kuurejelea kama wa usasa- Austin unazingatia mambo manne kuvianisha VU- kitovu cha kiilokusheni; mwelekeo wa ufaafu baina ya maneno na ulimwengu; hali ya kisaikolojia ya msemaji inayojitokeza na; maana ya kiproposisheni. Kwa kuyazingatia, Searle anaibuka na makundi matano ya VU.

### 2.2.3. Vitendo Usemi Elekezi (VUE)

Hivi ni VU ambavyo msemaji hujaribu kumfanya msemewa kutenda jambo kwa kutaja kile anachokitaka msemaji. Mifano ni pamoja na kuamuru, kushurutisha, kushawishi, kuomba, kurai, kusihi, kukaribisha, kuuliza (kujaribu kumfanya msikilizaji kujibu), bembeja, sairi, kunasihi, sisitiza, pendekeza, ruhusu na chachawiza. Ili VUE kufaulu sharti tendo liwe la hiari na la kutendwa wakati ujao. Kwa mfano—Ninakuamuru uondoke jana" au —ninakushurutisha ukue uwe mrefu" ni amri zisizo fasaha. Mwelekeo wake wa ufaafu huwa ulimwengu-kwa-neno. Mfano wa sentensi ni kama vile; *ingia darasani.* Katika VUE, proposisheni au NI huweza kukanushwa. Kila umbo lililokanushwa hurejelewa kwa namna tofauti tofauti ilivyoonyeshwa hapa (alama ya wimbi inawakilisha kukanusha).

| | |
|---|---|
| Amri | NI (Prop) ninakuamuru upige kura |
| Kataza, zuia, kanya | NI (~Prop) ninakuamuru/nimekukataza usiipige kura. |
| Ruhusu | ~ NI (Prop) sikuamuru upige kura |
| | ~ NI (~Prop) sikuamuru usiipige kura = unaweza kupiga. |

### 2.2.4. Vitendo Usemi Ahadi (VUA)

VUA humdiriki msemaji kwa utendaji wa wakati ujao wa jambo lililomo kwenye proposisheni ya tamko lake (Bussmann, 1996). Huonyesha nia ya msemaji kutenda jambo fulani. Katika aina hii ya VU, msemaji hujihusisha na utendaji wa kitendo. Mifano ya VUA ni pamoja na ahadi, apa, dhamini, tisha, kubali, kiri, kataa, ruhusu. VUA, kama VUE, huwa vya hiari na vya wakati ujao. Hisia ambayo huwasilishwa ni ya msemaji kuwa na nia ya kutenda jambo fulani. Mfano ni kauli Sitakununulia gari nyingine

### 2.2.5. Vitendo Usemi Taarifa (VUT)

Haya na matamko yawasilishayo hali ilivyo. Kwa hivyo, huonyesha imani ya msemaji kuhusu tamkolake. Katika kutoa tamko la aina hii, msemaji huwakilisha ulimwengu kwa namna anavyoamini ulivyo. Kwa njia hii, anayafanya maneno yake kuoana na ulimwengu wake wa imani. Hii ina maana kwamba mwelekeo wa ufaafu wa VUT huwa neno-kwa-ulimwengu, kwa kuwa maelezo hulengwa yawiane na hali ilivyo ulimwenguni. Mifano ya VUT ni arifu, fahamisha, sadikisha, thibitisha, eleza, taja, fafanua, pambanua, sisistiza, ambia, kadiria, dai, taja, radidi na bashiri. VUT humfungamanisha msemaji kwenye ukweli wa proposisheni inayowasilishwa. Msemaji huonyesha hisia ya imani, ingawa kiwango cha imani cha msemaji chaweza kuwa tofauti. Kwa mfano, kiwango cha kuthibitisha huwa cha juu huku cha kubashiri huwa cha muda tu. Ufuatao ni mfano kwa kitendo taarifa Vita vya pili vya dunia vilisababisha maafa.

### 2.2.6. Vitendo Usemi Hisia (VUH)

Katika aina hii ya VU, msemaji huwasilisha hali yake kisaikolojia kupitia proposisheni. Mifano ni shukrani, msamaha, kufariji, pongeza, salimu, na kusikitika. MP ni jambo linalowaathiri msemaji au msikilizaji. Si kawaida kusema "ninakufariji kwa msiba uliokupata ama ninakupongeza kwa kujaliwa mwana wa kiume", iwapo jambo linalohusika limemwathiri msikilizaji. VUH havina mwelekeo wa ufaafu wa upande wowote kwa sababu proposisheni hujitokeza kwa uchukuliaji wala haitangazwi. Mfano wa kitendo hisia ni kama vile: Hongera kwa hii tasnifu nzuri uliyoiandika.

### 2.2.7. (Vitendo Usemi Maamuzi (VUM)

Ni aina ya kitendo usemi ambacho, ikiwa kitafaulu kutendwa, matokeo yake ni upatikanaji wa proposisheni iliyotamkwa kama athari ya kutamkwa kwake tu, kwa mfano ninaufungua mkutano huu rasmi, ikitamkwa na mtu anayefaa, wakati unaofaa na mahali panapostahili (Bussmann, 1996). VUM ndivyo hurejelewa kama VU halisi. Kwa kutamka msemaji husababisha mabadiliko katika ulimwengu kwa kutamka. Mifano ni kutangaza hali hatari, kutangaza vita, kuunga mkono kumbukumbu za mkutano, kuahirisha kikao, kuachisha mwajiriwa kazi, kuteua, kupa jina, kubatiza, kumpata mshtakiwa na kosa, kuweka dau, kupa talaka, kubatiza, kutia nguvuni na

kujiuzulu. Kwa misingi hii, Elam (1980) anauona usemi kama nguvu ya kimahusiano baina ya watu katika ulimwengu halisi ambao huipa lugha uwezo wa kutekeleza matendo ya kijamii kama kuoa, kubatiza na kuhukumu. Kawaida, sharti msemaji awe na cheo fulani nje ya asasi ya kiisimu ili kitendo usemi cha maamuzi kuweza kutokea. Mwelekeo wa ufaafu wa VM huwa wa pande zote mbili kwa kuwa msemaji huwakilisha hali ya mambo na wakati huohuo kuisababisha hali hiyo. Hakuna hisia zozote ambazo huwasilishwa; kwa mfano rais anaweza kutangaza hali ya hatari ama kulivunja bunge pasi kutegemea hisia zake kuhusu tangazo hilo. Mfano wa kitendo maamuzi ni; ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kajwang'. Uainishaji wa Searle wa taarifa, vielekezi, ahadi, hisia na maamuzi una uwiano wa karibu na ule wa Austin (1962: 150-163) wenye vikundi vitano; vifunuzi, amri, ahadi, hisia na maamuzi.

Tofauti muhimu kati ya uainishaji wa Searle na ule wa Austin ni kuwa, Searle ametenganisha dhana ya kitendo usemi kutoka kwa kitenzi cha kitendo usemi. Kulingana naye kitenzi cha kitendo usemi si kigezo faafu cha kutumiwa kuainisha VU (Mey, 2001: 117; Degand, 2009: 1013).

Bach na Harnish (1979), Wakilenga kuleta pamoja mawazo ya Austin na Searle kwa upande mmoja, na yale ya Grice kwa upande mwingine, wanaibuka na makundi sita. Manne katika ya hayo sita (taarifa, vielekezi, ahadi na pongezi) huwiana na vifunuzi, vitumizi, ahadi na hisia kwa usanjari huo katika uainishaji wa Austin wa taarifa, vielekezi, ahadi na hisia wa Searle (Uk. 40-41). Makundi hayo mengine mawili, maamuzi na vielekezi, yanawiana na kile Searle anaita "Maamuzi" Uainishaji wao unaelekea kutegemea mtazamo wa Grice wa uelewa rejelevu wa dhamira ya kimawasiliano ya msemaji kuliko mtazamo wa Austin na Searle ambao huchukulia VU kama vinavyotendwa kulingana na kanuni. Baada ya kuleta pamoja mawazo ya wataalamu hawa na kuongeza yao wanaibuka na makundi sita (Tazama Jedwali 1).

Kwa kutumia kigezo cha kutathmini cha W, Allan (1994: 4125; 1998: 10-11) amebainisha aina nne za VU. Taarifa hujumuisha VU kama vile ripoti, kukanusha na ubashiri (taarifa za Searle). Mialiko ni kijisehemu katika vielekezi vya Searle kinachojumuisha ombi, mapendekezo, onyo na nasaha. Vielekezi vinginevyo vya Searle vimewekwa pamoja na maamuzi anaviita 'amri'. Hatimaye hisia hujumuisha salamu, shukrani, pongeza na udhuru. Naye Kreidler (1998)

ameainisha VU hadi makundi saba ambapo anaongeza vitenda na fati kwa vikundi vitano vya Searle. Katika jedwali 1 tunalinganisha hii mitazamo mbalimbali ya uainishaji.

**Jedwali 1: Aina mbalimbali ya uainishaji wa vitendo usemi**

| Austin (1962) | Vendler (1972) | Searle (1975) | Bach & Harnish (1979) | Allan (1994) | Kreidler (1998) |
|---|---|---|---|---|---|
| Vifunuzi | Vifunuzi | Taarifa | Taarifa | Kauli | Taarifa |
| Ahadi | Ahadi | Ahadi | Ahadi | | Ahadi |
| Vitumizi | Vidahili | Vielekezi | Vielekezi | Mwaliko | Vielekezi |
| | Vitumizi | | | Amri | Amri |
| Maamuzi | Viendeshi | Maamuzi | Viendeshi | | |
| | Maamuzi | | Maamuzi | | Maamuzi |
| Hulka | Hulka | Hisia | Pongezi | Hisia | Hisia |
| | | | | | Fati |

**2.2.8. Palokusheni**

Tamko hufanikisha nia ya msemaji kama matokeo ya kudhihirisha nia ya msemaji kufanya jambo fulani (Capone, 2009:1015). Palokusheni huhusu athari ambayo tamko linaweza kuwa nayo kwa msemewa. Palokusheni hufafanua jinsi ilokusheni huathiri msemewa. Yaani matokeo ya kuzungumza. Palokusheni ni mwitikio wa lokusheni ya msemaji inayoathiri tabia, imani na hisia za msemewa. Hii ina maana kwamba palokusheni ni ufasiri wa malengo ya ilokusheni aufanyao msemewa. Mifano ya palokusheni ni kushtuka, kukerwa kushawishika, kukasirika, kuchochewa au kuridhika. Ili kuhakikisha kwamba mawasiliano yamekamilika, ni muhimu msemewa atambue aina ya VU vinavyotendwa na kuitikia ipasavyo. Kwa jinsi hii, hali huweza kubadilishwa kwa upande wa msemewa. Hii ndiyo inayorejelewa kama AP (Blakemore 1992 katika Wairima 2009). Kutokana na umuhimu wa NI kwenye nadharia ya VU, kwenye sehemu inayofuata niliaangazia dhana hii.

## 2.3. Kanuni za ufasaha

VU huweza kueleweka kwa sababu vinapatana na kanuni fulani fulani. Kanuni hizi huhusu masuala ambayo hufaulisha utendaji wa ilokusheni (NI + MP). Masuala haya ndiyo huunda maana ya tamko. Kwa kuwa tamko ndilo kipasho cha kimsingi, kanuni hizi huwa muhimu kwa msilikizaji kwa kuwa zinamfaa katika kupata fasiri kamili ya tamko. Kanuni za ufasaha zinaweza kutambuliwa kwa urahisi kwenye muktadha wa mawasiliano kwa kuwa msemewa yupo, hivyo msemaji anaweza kuyarekebisha matamko yake kulingana na nia yake.

Kuna makundi mawili ya kanuni ambayo hudhibiti utendaji na uelewekaji wa VU – jumuishi na sawazishi. Kanuni jumuishi hutambua jinsi kitendo kitakavyokuwa. Watu hutambua ahadi pindi tu wanaposikia ikitamkwa kwa kuwa wanaelewa kanuni zake. Ahadi hutofautishwa kutoka kwa amri kutokana na tofauti zao kwenye kanuni za kile kila tamko hujumlisha. Seale anatumia mfano wa ahadi kuonyesha hizi kanuni jumuishi akisema kwamba huwa na kanuni tano: (1) Itangaze kwamba msemaji atafanya kitendo Fulani wakati ujao; (2) sharti kiwe kitendo ambacho msikilizaji angependa msemaji kukitenda; (3) kitendo hicho kiwe kile ambacho katika hali ya kawaida, msemaji hangekitenda; (4) msemaji kwa kweli awe na nia ya kukitenda; na (5) msemaji na msemewa wachukulie kauli hiyo kama wajibu wa kutekelezwa (Littlejohn, 2009:919).

VU hutolewa kwa njia ya moja kwa moja, ambapo kanuni zote jumuishi huzingatiwa kwa njia ya moja kwa moja. Hata hivyo mara nyingi, wanaowasiliana hutoa VU kwa njia isiyo ya moja kwa moja, wakichukulia kuwa vipashio kwenye kitendo ni wazi kutoka kwa muktadha, ama huwa vimemaanishwa wala haviko wazi. Upo uwezekano wa kuwa na VU visivyo vya moja kwa moja kwa kuwa wanaohusika wana habari za awali wanazozifahamu. Grice (1957) ansema kwamba kanuni za kitendo usemi huvunjwa kimakusudi, si kwa lengo la kuhadaa, bali kutajirisha usemi na kuupatia mvuto wa kipekee. Ukiushi wa kanuni pia huwawezesha wasemaji kutamka kauli zinazowaingilia wasikilizaji lakini kwa upole, na kumpa msikilizaji uwezo wa kuwa mshiriki mtendaji unapojishughulisha kufasiri matamko kwa kiwango cha muktadha pana. Watu wanapotoa VU kwa njia isiyo ya moja kwa moja, au kukiuka kanuni kwa njia moja au nyingine, huwa wanategemea mifichamo ya kitawasiliano, au fasiri ambazo wasemewa wanapaswa kufanya. Mtu anaposema *"nina njaa"* anategemea uwezo razini wa msemewa kufasiri nia yake ya kuomba chakula.

VU pia huhitaji kanuni sawazishi. Kanuni hizi hutaja utaratibu wa utendaji wenyewe na kuelekeza namna wasikilizaji wanavyomjibu msemaji. Kitendo usemi hakitakuwa kimetekelezwa hadi pale nia zake za kiilokusheni na za kipalokusheni zimeeleweka na msemewa kuitikia ipasavyo. Sharti ahadi ikubalike kama ahadi, la sivyo, iwe batili, ombi likubaliwe au lisikubaliwe, vinginevyo halitakuwa ombi. Kanuni jumuishi hutuonyesha nia inayowasilishwa na kitendo usemi; nayo kanuni sawazishi hutuonyesha jinsi ya kuitikia ili kukamilisha kitendo hicho. Mahitaji haya yanarejelewa na Searle (1983) kama kanuni za uridhishaji (Littlejohn, 2009: 919). Searle (1969) anataja kanuni nne kuu ambazo sharti ziwepo kitendo usemi kuweze kufaulu.

### 2.3.1. Kanuni ya maana ya kiproposisheni

MP ni kile kinachodaiwa katika kauli, huku NI ikiwa nia inayowasilishwa. Kwa mfano MP *"ninahisi njaa"* ina NI ya kuomba chakula. Proposisheni huwasilisha jambo ambalo masemaji anaamini ni la kweli au angependa msemewa achukulie kuwa ni la kweli, lakini proposisheni hiyo hutolewa kwa lengo kwamba, kwa sababu ya NI za tamko hilo, wengine wataitambua (Littlejohn, 2009: 918). Kwa mujibu wa falsafa changanuzi, proposisheni huhakikiwa kwa msingi wa uhalali. Ikiwa inazingatia viwango fulani vya ukweli kama vile ushahidi na mantiki, basi inafaa.

Kwa upande mwingine, VU uhakikiwa kwa kuzingatia kanuni za ufasaha. Kwa hakika chanzo cha kutoelewana mara nyingi huwa ni kushindwa kufahamu nia ya msemaji (Littlejohn, 2009: 919), yaani NI yake.

Kanuni hii kimsingi huhusu kile kitendo usemi hushughulikia. Huweka sheria kwenye MP ya baadhi ya ilokusheni. Hii ina maana kwamba, inahusu kutambua mipaka inayowekwa kwenye dhamira ambayo huwa *"kiini"* cha tamko, baada ya kuondolewa kwa sehemu ya kitendo cha kiilokusheni kutoka kwa tamko hilo. Hii ni kanuni sawazishi.

### 2.3.2. Kanuni za matayarisho

Ni lazima msemaji awe na idhini kutekeleza kitendo kinachohusika. Kwa mfano awe na kibali kikatiba kutangaza hali ya hatari nchini au kutoa hukumu kortini; awe na ithibati kwa yale anayoyasema; asiwe na ufahamu wa kile anachokiuliza n.k. kanuni hii hutaja mahitaji

yanayopaswa kuwepo ili kitendo usemi kifaulu. Kama kanuni ya MP, hii pia ni kanuni sawazishi.

### 2.3.3. Kanuni za uaminifu

Kanuni za uaminifu hufafanua hali ya kisaikolojia ya msemaji. Msemaji anapaswa kuwa mkweli na mwaminifu kwa kila anachokisema; kwa hakika anahitaji anachokiomba; awe mwenye shukrani ya dhati. Msemaji hunuia kusema anachokisema. Sharti kanuni hii itoshelezwe, ikiwa kitendo kitafanywa kwa uaminifu. Wakati wa kuahidi, sharti anayeahidi awe na nia ya dhati kutekeleza ahadi. Ikiwa kanuni hii haizingatiwi, bado kitendo kitatendeka, lakini patajitokeza matumizi mabaya ya nia au cheo. Kama zilivyo kanuni za kwanza mbili, hizi pia huwa kanuni sawazishi.

### 2.3.4. Kanuni za msingi

Kanuni za kimsingi, hueleza kile kitendo kinajumuisha. Msemaji afungwe na ahadi ya kutekeleza tendo lililopo; ajitolee kwenye taarifa anayoitoa. Tamko humfunga msemaji kuwajibikia tamko lake. Kanuni hii hudai kwamba msemaji huwa na nia kwamba tamko lake litachukuliwa kama kitendo na nia yake kutambuliwa na wasemewa. Kanuni hii inapokosa ina maana kwamba kitendo kinachohusika hakifanyijki. Hi ni kanuni jumuishi.

Searle pia anazungumzia *"kanuni ya ujielezaji,"* ambayo ndiyo kanuni ya pekee inayoruhusu uchanganuzi wa (kimsingi wa) kipragmatiki wa VU. Hii ni kinyume na uchanganuzi wa kisemantiki wa kauli. Kutokana na mawazo haya nilibainisha mikabala miwili katika uchanganuzi wa VU. Wa kwanza ni wa kisemantiki ambao huruhusu uchanganuzi wa sifa za VU huku mkabala wa pili, ukiwa wa kipragmatiki, ukisisitiza michakato ya mawasiliano katika kushughulikia VU. Kwa kuwa VU vyote ni tendaji, ingawa vinatofautiana kwenye viwango vya utendaji, kwenye sehemu ifuatayo niliangazia kitenda nikikilinganisha na kitaarifu.

## 2.4. Kitenda na kitaarifu

Lugha inaweza kuwa ya kutaarifu au ya kitenda. Kwa kusema lugha kutaarifu ina maana inafafanua ukweli au uwongo kuhusu kitu. Kwa upande mwingine lugha ya kitenda huwa haisemi tu, pia hufanya kitu fulani wakati huohuo. Wasemavyo Bennett na Royle (1995), lugha

isingekuwa na uwezo huo wa kutenda ndoa haingewezekana kufanyika au mikutano kukamilika. Kitenda ni kauli ambayo, licha ya kueleza kitendo, wakati huohuo hukitenda hicho kitendo (Bennett na Royle, 1995: 234; Huang 2009: 1000).

Kwenye mihadhara yake ya baadaye, Austin alitupilia mbali uainishaji wa kitenda kitaarifu kwa msingi kwamba hata kiraarifu huwa na kigezo cha kutenda (kupitia kutamka) hivyo akadai kwamba hata kitaarifu ni ilokusheni. Alichukua hatua hii kutokana na sababu tatu. Kwanza, ukosefu wa mfumo wa kisarufi wa kuvitenga vitenzi vitenda kutoka kwa vitenzi vinginevyo. Pili, ukweli kwamba kuwepo kwa kitenzi kitenda si ithibati ya kutendwa kwa tendo. Tatu, kuwepo kwa njia badala za '*kitenda vitu kwa maneno*' ambazo hazihusishi matumizi ya kitenzi kitendi (Thomas, 1995). Bussmann (1996) anasema kwamba kinyume na vitenda ambavyo ni vibeba matukio, vitaarifu huwa vibeba ukweli. Katika sehemu inayofuata niliangazia dhana ya proposisheni ambayo maana hujitokeza.

## 2.5 Proposisheni

Proposisheni kwa mujibu wa Larson (1984) ndicho kipashio kidogo kabisa cha mawasiliano. Dhana huwa na maana kwa sababu zinarejelea vitu, matukio, sifa au mahusiano. Hadi pale dhana inapojitokeza na dhana nyinginezo ndipo pana mawasiliano kamili. Iwapo muungano wa dhana una maana ndipo mawasiliano yatafanikiwa. Proposisheni moja huwa na tukio moja. Hii ina maana kwamba proposisheni moja ni sana na sentensi sahili. Kwa mantiki hii, sentensi ni tungo kamili yenye jukumu la kiilokusheni.

Proposisheni ni habari inayowasilishwa na tamko pasi kuzingatia jinsi habari yenyewe imewasilishwa (Kreidler, 1998). Hii in maana kwamba habari inaweza kuwasilishwa kwa njia tofauti tofauti lakini ujumbe ukabaki kuwa ule ule.

Maana ya tamko hujumuisha kipanuzi, kitu au sifa halisi inayorejelewa, pamoja na dhamiri, nduni ambazo hutumiwa kukitofautisha kitu hicho kutoka kwa vitu vinginevyo (Chapman, 2000). Ikiwa ni sentensi, kipanuzi chake si kitu au sifa ama hali ya mambo bali ni thamani-ukweli wake, yaani ana ukweli au uwongo. Hii ina maana kwamba katika lugha, kauli huwa na upanuzi wa ama ukweli au uwongo.

Uchanganuzi wa tofauti za kimaana kati ya sentensi mbili za kweli huhusisha maana ya kidhamira. Chapman (2000:44) akimnukuu Frege anasema thamani-ukweli ya sentensi ndiyo hujumuisha maana ya sentensi hiyo. Yaani, maana ni urejeleaji au kipanuzi ambacho hufaa kueleweka kama maana ya wazo linalowasilishwa. Hii ndiyo proposisheni. Katika isimu na falsafa, proposisheni huhusishwa na dhana, fikra, kauli, madai, tetesi na Imani. Wakati mwingine proposisheni hutangulizwa kwa virai "kwamba ...." au "kuwa ......." Kwa mfano unaamini kwamna mwanasiasa Obita, jirani yako anayeishi mlango nambari 4, ni mzuri, basi proposisheni kwamba mwanasiasa Obita ni mzuri ndiyo maana ya imani ya msemaji na inaweza kuwasilishwa kwa namna mbalimbali zifuatazo:

a) Mwanasiasa Obita ni mzuri
b) Jirani yangu ni mzuri

Sentensi *a* – *b* kwa hakika si visawa lakini zinawasilisha proposisheni ile ile. Hii ina maana kwamba *a* na *b* zinafanana kidhamira. Ukweli wa kauli hizi, unahitaji kupata ukweli wa hii proposisheni moja. Ikiwa mwanasiasa Obita ni mzuri, basi Imani (na hivyo sentensi zote zilizotumiwa kuwasilisha) zitakuwa za kweli. Hii huathiri ukweli na uwongo wa sentensi zinazowasilisha.

Kiini cha maana ya kiisimu ni ishara zinazowakilishwa na ishara ya kiisimu iliyotumiwa (Devitt na Sterelny, 1991). Kwa mantiki hii ninaweza kusema kwamba, kiini cha maana ya msemaji ni proposisheni za tamko la msemaji. Proposisheni hujitokeza ndani ya matamko, na matamko huwa ndiyo VU. Hivyo basi kipashio cha maana si neno bali ni kitendo usemi.

Larson (1984) anaonyesha kwamba proposisheni ni kundi la dhana lijengalo kipashio cha mawasiliano. Anasema hiki ni "kipashio cha kisemantiki chenye dhana ambazo kwazo moja ya dhana hizo huwa kiini huku zile nyinginezo zikihusiana nayo moja kwa moja." (Uk, 190). Dhana anazozitaja Larson ni vitu, matukio na sifa. Iwapo dhana kiini ni tukio kwa mfano, proposisheni iliyomo huwa ni proposisheni tukio. Dhana Mohammed, Kuria na piga zinaweza kuunganishwa kuunda proposisheni. Kitendo piga ndicho kiini (dhana tukio). Kitakachowasilishwa na proposisheni hutegemea uhusiano wa hizo dhana nyinginezo na dhana tukio piga. Iwapo Mohammed atatenda upigaji na Kuria ndiye atapigwa, basi proposisheni

itakuwa Mohammed alimpiga Kuria. Iwapo Mohammed ndiye alipigwa, proposisheni ni Kuria alimpiga Mohammed au Mohammed alipigwa na Kuria.

Larson ametaja aina mbili za proposisheni-tukio na hali. Proposisheni tukio huwa na angalau dhana moja ya tukio pamoja na dhana ya kitu. Tukio linaweza kurejelea tendo, mchakato au mapitikio. Mifano ya matukio ni kama *kimbia*, *kula* na *pokea*; mapitio ni kama *fahamu*, *elewa*, *sikia* na *ona*, na; michakato ni kama vile kolea, chakachua, chachua, na yeyuka. Michakato ni matendo yanayohusisha fahiwa tano za *kuona*, *kusikia*, *kugusa*, *kuonja* na *kunusa* huku mapitikio yakihusu mabadiliko katika hali.

Proposisheni hali hazina tukio lisilo la kimsingi. Proposisheni za aina hii hujumuisha dhana za vitu na sifa ambazo huhusiana kwa kigezo cha hali. Huwa na sehemu mbili- mada na maoni. Mada ni dhana inayorejelewa huku maoni yakijumuisha kitu au sifa inayotumiwa kufafanua mada pamoja na uhusiano hali unaojitokeza. Kwa mfano katika sentensi *Hiki chama ni cha Odinga*, mada ni "*hiki chama,*" na inahusiana na dhana kiini 'Odinga' kupitia uhusiano wa umiliki (sifa). Hivyo basi maana ni kwamba chama kinamilikiwa na Odinga.

Ni muhimu kuchunguza proposisheni kwa mkabala wa hali zinamotumika ili kubainisha nia ya msemaji. Pengine anauliza swali au kutoa amri. Haya yatajitokeza ikiwa tutajaribu kuelewa kile msemaji anajaribu kuifanyia proposisheni yake. Hii ni kwa sababu, maana rejelezi inaweza kuwa ile ile lakini matumizi yakawa tofauti kadiri proposisheni inavyobadilika. Tazama mifano ifuatayo;

| **Maana rejelezi** | **Mfano** |
|---|---|
| Kauli | Mwita alipiga kura |
| Swali | Mwita alipiga kura? |
| Mshangao | Mwita alipiga kura! |

Hizi tofauti za kimaana, kinyume na maana rejelezi huitwa maana muktadha. Proposisheni tukio na proposisheni hali zinaweza kujitokeza pamoja na hizi maana muktadha. Katika mazingira haya, hizi proposisheni huitwa NI. Proposisheni huwa tu na maana rejelezi hadi itakapoongezewa NI. Mawasiliano hayawezi kukamilishwa ikiwa hizi maana za kimuktadha

hazitajumuishwa. Asemavyo Larson (1984: 196) "Upo uwezekano wa kuzifahamu dhana zinazounda proposisheni na mahusiano yaliyopo baina ya dhana hizo, lakini bado mtu asijue maana ya msemaji." Kwa mfano, kuna tukio kula, mtendwa kuku na mtenda kicheche, lakini huenda tusifahamu maana ya msemaji kama ni kutoa taarifa (kicheche alimla kuku) au kuuliza (kicheche alimla kuku?) au kushangaza (kicheche alimla kuku!) Hii ina maana kwamba nia ya msemaji huwa muhimu katika mawasiliano. Nia hii ambayo tumeirejelea kama NI, hudhihirika katika lugha mbalimbali kwa njia tofauti tofauti kama vile matumizi ya alama za uakifishi, mpangilio wa maneno, kiimbo, faridipeke au kuitaja waziwazi (Hickey, 1998).

Proposisheni ni vibeba ukweli, maana ya kisemantiki ya sentensi na kile wasemacho, wanachoamini na kukijua wasemaji (Soames 2010: 109).

Katika sehemu hii nimeonyesha kwamba proposisheni huathiri maana. Hii inaonyesha kwamba proposisheni ni sehemu ya maana (Hurford n.w, 2007). Maana ya tamko katika ukamilifu wake hujumuisha MP na NI. Hivyo basi ni muhimu kuchunguza NI katika sehemu inayofuata. Kwa kuwa kile kinachopatiwa uzito ni maana.

## 2.6. Nguvu ilokusheni

Muundo wa kisemantiki wa VU hujumuisha nguvu zake za kiilokusheni (NI) na maana yake ya kiproposisheni (MP). NI ni namna proposisheni inapaswa kuchukuliwa. NI hujitokeza kupitia kwa vitenzi vitenda, aina ya sentensi, mpangilio wa maneno, mkazo, kiimbo, uakifishaji, au dhamira.

Searle na Vanderveken (1985) wanatofautisha NI zinazotumiwa na jamii-lugha mahususi kutoka kwa seti ya kijumla ya NI zinazoweza kujitokeza (tuiite seti bia ya NI). Wanaelekea kuamini kwamba seti hizi hazina kikomo, ingawa zina maana yenye ukomo. Searle na Vanderveken wanapiga hatua Zaidi na kutaja vipengele saba vya NI. Vipengele hivi ni;

i) kitovi cha kiilokusheni: hii ni lengo bainifu la bila aina ya kitendo usemi. Kwa mfano. Lengo bainifu la taarifa ni kueleza jinsi vitu, mambo au hali ilivyo; lengo bainifu la ahadi ni kumfunga msemaji kwenye tukio lijalo.

ii) Kiwango cha uwezo wa kitovu cha kiilokusheni: ilokusheni mbili zinaweza kuwa na kitovu kimoja lakini zikatofautiana katika uwezo wao. Kwa mfano kuomba na

kushurutisha msemewa afanye jambo fulani huwa na kitovu kimoja cha kumtaka msemewa kufanya jambo linalorejelewa. Hata hivyo, uwezo huu unaweza kuwa wa kiwango cha juu kwa mfano kushurutisha huwa mkubwa kuliko ule wa kuomba.

iii) Namna ya kufaulisha: Hii ni njia maalum ya kufanikisha kitendo usemi. Kitovu cha ushuhuda na cha taarifa huwa kueleza jinsi mambo yalivyo; hata hivyo, ushuhuda huhitaji amri ya msemaji kama shahidi ilhali sivyo ilivyo katika taarifa. Kutoa ushuhuda kuna maana ya kusema kwamba anayetoa ushuhuda anaweza kuwa shahidi. Mfano mwingine ni amri na ombo ambavyo ni VU vinavyomtaka msemewa afanye jambo fulani, hata hivyo, ni yule tu anayeamuru pekee, ndiye hutumia mamlaka yake kama mwenye cheo fulani kufaulisha ilokusheni yake.

iv) Kanuni zinazodhibiti MP: baadhi ya ilokusheni huweza kufaulu zinapoambatanishwa MP inayofaa. Kwa mfano, ninaweza tu kuahidi jambo la wakati ujao na ninalolidhibiti. Ninaweza kuomba msamaha kwa kile kimekwishatendeka na ninaudhibiti kwacho. Kwa sababu hii, ahadi inaweza kukataa kauli kama "jua halitaangaza jana" kwa kuwa hili haliwezekani; pia huwezi kuomba msamaha kuhusu ukweli wa kanuni upole ya Grice.

v) Kanuni tayarishi: hujumuisha kanuni nyinginezo ambazo sharti ziwepo ili kitendo usemi kisitibuke. Kanuni hisi huhusu hadhi ya wanaohusika. Kwa mfano, mtu hawezi kuhalifu mwenzake kitu ikiwa hana umiliki wa kitu hicho, ama hana mamlaka kisheria; mtu hawezi kufungisha ndoa ikiwa hana mamlaka ya kikatiba kufanya hivyo.

vi) Kanuni za uaminifu: karibu VU vyote hudhihirisha hali ya kisaikolojia ya msemaji. Taarifa huashiria imani; msamaha huonyesha majuto na; ahadi inaashiria nia ya kutekeleza. Kitendo usemi huaminika ikiwa msemaji atadhihirisha hali ya kisaikolojia iliyomo kwenye kitendo usemi kinachohusika.

vii) Kiwango cha uwezo wa kanuni za uaminifu: Vu viwili vinaweza kufanana kwenye vigezo hivyo vingine lakini vikatofautiana kwenye uwezo. Kila kimoja kikidhihirisha uwezo kisaikolojia. Kuomba na kusihi hudhihirisha tamani, japo VU hivi vinafanana katika vipengele sita vya hapo juu, kusihi kuna uwezo zaidi kuliko kuomba. Ufuatao ni muhtasari wa vipengele hivi kwenye uainishaji wa Searle.

| Kitovu cha kiilokusheni/ aina | Mwelekeo wa ufaafu | Hali ya kisaikolojia |
|---|---|---|
| Taarifa | Maneno-kwa-ulimwengu | Imani |
| Kielekezi | Ulimwengu-kwa-maneno | Tamani |
| Ahadi | Ulimwengu-kwa-maneno | Nia |
| Hisia | Hakuna | Hubadilikabadilika |
| Maamuzi | Pande zote mbili | Hakuna |

## 2.7 Hitimisho

Hadi hapa mjadala wangu umeonyesha maana mbalimbali za sitiari na aina zake kulingana na wasomi mbalimbali. Isitoshe, nimefafanua dhana za kimsingi za VU na umuhimu wao katika mawasiliano. Pia niliteua sitiari chakavu kuongoza utafiti wangu kwa sababu kwenye siasa, wanasiasa wengi hutumia sitiari chakavu kujisifu, kueleza jinsi makabila yao yamepuuzwa au kudunishwa kwa muda mrefu katika ugavi wa rasilimali pamoja na uteuzi wa nyadhifa mbalimbali ya serikali. Vilevile, wanasiasa wengine hutumia sitiari chakavu kudunisha wapinzani wao. Kwa mfano, mara nyingi wanasiasa nchini Kenya wametumia sitiari chakavu; 'Nyani haoni kundule' kueleza wanaowakosoa kwamba hao pia wana dosari zaidi. Katika kuchunguza jinsi nadharia hii inaweza kufanikisha mawasiliano, kwenye sura inayofuata, nimeitumia nadharia hii katika kutambua na kuainisha VU mbalimbali vilivyomo kwenye sitiari za Kiswahili nilizoziteua kabla ya kuonyesha jinsi zilivyoendeleza kauli ya kichochezi nchini Kenya.

# SURA YA TATU

# VITENDO USEMI KATIKA SITIARI ZA KISWAHILI ZINAZOTUMIKA KATIKA SIASA NCHINI KENYA

## 3.0 Utangulizi

Matumizi ya lugha kuwasilisha nia ya msemaji ndiyo yamerejelewa kama VU. Nimeshughulikia masuala ya nadharia yanayoongoza utafiti huu. Nimefafanua misingi, mihimili pamoja na masuala mengineyo muhimu. Katika sura ya pili nimefafanua dhana za kimsingi za VU na umuhimu wao katika mawasiliano. Kutokana na kuwepo mikabala na mitazamo kadhaa ya kuvianisha VU, kwenye sura hii niliangazia uainishaji wa Searle (1975) kuelekeza uchunguzi wangu. Data zilizokusanywa zimechanganuliwa kwa msingi wa nadharia ya vitendo usemi kama ifuatavyo:

George Aladwa akizungumza na wafuasi wa ODM katika eneo bunge la Kibra mnamo tarehe 14/1/2017 alisema*"...... Raila hakupeleka Ruto ICC, waache maombi ya uongo. Ruto ana mawakili, akishinda sawa na akibaki sawa. 2017 imefika na sisi kaka watu wa ODM tumebaki na risasi moja. Mimi ninamwambia party leader Raila Amollo Odinga, This time round the outcome of elections ikiwa tumeshinda na watunyanganye, wacha kiumane."*

*"Wacha kiumane"* ni aina ya sitiari inayopatikana katika Vitendo Usemi Maamuzi (VUM) kwa vile ni aina ya kitendo usemi ambacho, ikiwa kitafaulu kutendwa, matokeo yake ni upatikanaji wa proposisheni iliyotamkwa kama athari ya kutamkwa kwake tu; *"This time round the outcome of elections ikiwa tumeshinda na watunyanganye, wacha kiumane."*. Kwa kutamka maneno *"Wacha kiumane"*, msemaji husababisha mabadiliko katika ulimwengu. Kwa mifano, sitiari *"Wacha kiumane"* inatangaza hali ya hatari, kutangaza vita, kuahirisha kikao, kuteua, kupa jina, kubatiza, kumpata mshtakiwa na kosa, kuweka dau, kutia nguvuni na kujiuzulu. Kwa misingi hii, Elam (1980) anauona usemi kama nguvu ya kimahusiano baina ya watu katika ulimwengu halisi ambao huipa lugha uwezo wa kutekeleza matendo ya kijamii kama kuoa, kubatiza na kuhukumu. Kawaida, sharti msemaji awe na cheo fulani nje ya asasi ya kiisimu ili kitendo usemi cha maamuzi kuweza kutokea. Katika muktadha huu, sitiari *"Wacha kiumane"* hutumika na wanasiasa ambao wako na ushawishi mkubwa kwa wafuasi wao hivyo basi kuwachochea dhidi

ya jamii lengwa. Mwelekeo wa ufaafu wa VUM huwa wa pande zote mbili kwa kuwa msemaji huwakilisha hali ya mambo na wakati huohuo kuisababisha hali hiyo. Hakuna hisia zozote ambazo huwasilishwa; kwa mfano rais anaweza kutangaza hali ya hatari ama kulivunja bunge pasi kutegemea hisia zake kuhusu tangazo hilo. "*Sisi kama watu wa ODM, tumebaki na risasi moja*", ni sitiari ambayo imetumika katika usemi huu kuashiria kwamba wafuasi wanaolengwa wanashauriwa kujitokeza ili kumsaidia mgombea wao ili ashinde katika uchaguzi kwani hatakuwa na uwezo tena wa kuwania kiti cha urais ikiwa ameshindwa.

Mbunge wa Suna Mashariki Junet Mohamed, akizungumza na wafuasi wa ODM mjini Homabay mnamo tarehe 15/7/2017 alisema "....... *sisi ndio jeshi la Raila na tutakufa kabla ya yeye. Wasipotangaza Raila kama Rais wa Kenya kwa njia ya haki na ukweli wataona. Ile ya 2007 itakuwa ya kitoto.*"

Usemi "Ile *ya 2007 itakuwa ya kitoto.*" ni Vitendo Usemi Ahadi (VUA) kwa vile unaashiria msemaji kuwa na nia ya utendaji wa wakati ujao wa jambo lililomo kwenye proposisheni ya tamko lake; "*Ile ya 2007 itakuwa ya kitoto.*" (Bussmann, 1996). Huonyesha nia ya msemaji kutenda jambo fulani. Katika aina hii ya VUA, msemaji amejihusisha na utendaji wa kitendo. Hii ni kwa sababu Usemi huu una Vitendo Usemi kama vile ahadi, apa, dhamini, tisha, kubali, kiri, kataa, ruhusu. VUA huwa ni vya hiari na vya wakati ujao. Hisia ambayo huwasilishwa ni ya msemaji kuwa na nia ya kutenda jambo fulani. "*Ile ya 2007 itakuwa ya kitoto.*" ni sitiari ambayo imetumika katika usemi huu kwa lengo la kuonya kuwa ikiwa matokeo ya uchaguzi hayatakuwa ya haki na ukweli basi wajitayarishe kwa vita vikali zaidi ya vita vya 2007. Wanaohusika na uchaguzi wanatahadharishwa ili kufanya uchaguzi kwa njia ya ukweli bila ubaguzi wowote.

*"Tutaondoa madoadoa katikati yetu"*

Sitiari "*Tutaondoa madoadoa katikati yetu",* ni aina ya Vitendo Usemi Elekezi (VUE). Hii ni kwa sababu wanaoitumia kuchochea wengine katika siasa hujaribu kumfanya msemewa kutenda jambo kwa kutaja kile anachokitaka; *"tutaondoa madoadoa".* Kwa mfano, msemaji anajaribu kuamuru, kushurutisha, kushawishi, kuomba, kurai, kuuliza bembeja, sairi, kunasihi, sisitiza, pendekeza, ruhusu na chachawiza. Uwanja wa siasa nchini Kenya kuitaja jamii nyingine kama 'madoadoa' ni jambo linalojulikana. Kutumia sitiari kurejelea kundi la watu kama 'madoadoa'

Mbunge wa Suna Mashariki Junet Mohamed akizungumza katika uwanja wa Manispaa wa Homabay mnamo tarehe 15/7/2017 alisema *"Hao watu wa Jubilee wakija Homabay wachapwe viboko na wapigwe na mawe."*

*"Hao watu wa Jubilee wakija Homabay wachapwe viboko na wapigwe na mawe."* ni sitiari inayoweza kupatikana katika aina mbili za Vitendo Usemi; Vitendo Usemi Maamuzi (VUM) na Vitendo Usemi Elekezi (VUE). Ni aina ya VUM kwa vile ni aina ya kitendo usemi ambacho, ikiwa kitafaulu kutendwa, matokeo yake ni upatikanaji wa proposisheni iliyotamkwa kama athari ya kutamkwa kwake tu "wachapwe viboko na wapigwe na mawe". Kwa kutamka maneno haya, msemaji husababisha mabadiliko katika ulimwengu kwa kutamka. Kwa mifano, sitiari hii inatangaza hali ya hatari, kutangaza vita, kuahirisha kikao, kuteua, kupa jina, kubatiza, kumpata mshtakiwa na kosa, kuweka dau, kutia nguvuni na kujiuzulu. Kwa misingi hii, Elam (1980) anauona usemi kama nguvu ya kimahusiano baina ya watu katika ulimwengu halisi ambao huipa lugha uwezo wa kutekeleza matendo ya kijamii kama kuoa, kubatiza na kuhukumu. Kawaida, sharti msemaji awe na cheo fulani nje ya asasi ya kiisimu ili kitendo usemi cha maamuzi kuweza kutokea. Katika muktadha huu, sitiari hii imetumika na wanasiasa ambao wako na ushawishi mkubwa kwa wafuasi wao hivyo basi kuwachochea dhidi ya jamii lengwa.

Mwelekeo wa ufaafu wa VUM huwa wa pande zote mbili kwa kuwa msemaji huwakilisha hali ya mambo na wakati huohuo kuisababisha hali hiyo. Hakuna hisia zozote ambazo huwasilishwa; kwa mfano rais anaweza kutangaza hali ya hatari ama kulivunja bunge pasi kutegemea hisia zake kuhusu tangazo hilo.

Vilevile, ni aina ya VUE kwa vile msemaji anajaribu kumfanya msemewa kutenda jambo kwa kutaja kile anachokitaka msemaji "wachapwe viboko na wapigwe na mawe". Mifano ni pamoja na kuamuru, kushurutisha, kushawishi, kuomba, kurai, kusihi, kukaribisha, kuuliza (kujaribu kumfanya msikilizaji kujibu), bembeja, sairi, kunasihi, sisitiza, pendekeza, ruhusu na chachawiza. Ili VUE kufaulu sharti tendo liwe la hiari na la kutendwa wakati ujao.

Msemaji wa tungo hili anawachochea wafuasi wao kutoka Homabay kuwa wapinzani wao wakija katika eneo hilo basi washughulikiwe kwa kupigwa kwa mawe na kuchapwa. Matamshi

haya, *"Hao watu wa Jubilee wakija Homabay wachapwe viboko na wapigwe na mawe,"* hutumiwa kiuchochezi kati ya pande mbili zinazong'ang'ania umaarufu katika ngome zao.

Mbunge wa Gatundu Moses Kuria akizungumza katika kituo cha ununuzi wa Ithekahuno Tetu mnamo tarehe 6/6/2017 alisema *"Jitu linaloitwa Raila linapaswa kupigwa kwa kichwa liuawe ili lisiharibu serikali ya Uhuru."*

Sitiari *"Jitu linaloitwa Raila linapaswa kupigwa kwa kichwa liuawe ili lisiharibu serikali ya Uhuru"* inaweza kuelezwa kwa njia mbili; Vitendo Usemi Taarifa (VUT) na Vitendo Usemi Elekezi (VUE). Ni VUT kwa vile msemaji anajaribu kueleza jinsi serikali ya Uhuru inaharibiwa na Raila. VUT in aina ya sitiari ambayo matamko yanawasilisha hali ilivyo. Kwa hivyo, huonyesha imani ya msemaji kuhusu tamko lake. Katika kutoa tamko la aina hii, msemaji huwakilisha ulimwengu kwa namna anavyoamini ulivyo. Msemaji anaamini kuwa Raila akipigwa kwa kichwa basi serikali ya Uhuru itabaki imara. Kwa njia hii, anayafanya maneno yake kuoana na ulimwengu wake wa imani. Hii ina maana kwamba mwelekeo wa ufaafu wa VUT huwa neno-kwa-ulimwengu, kwa kuwa maelezo hulengwa yawiane na hali ilivyo ulimwenguni. Mifano ya VUT ni arifu, fahamisha, sadikisha, thibitisha, eleza, taja, fafanua, pambanua, sisistiza, ambia, kadiria, dai, taja, radidi na bashiri. VUT humfungamanisha msemaji kwenye ukweli wa proposisheni inayowasilishwa. Msemaji huonyesha hisia ya imani, ingawa kiwango cha imani cha msemaji chaweza kuwa tofauti. Kwa mfano, kiwango cha kuthibitisha huwa cha juu huku cha kubashiri huwa cha muda tu.

Vilevile, sitiari *"Jitu linaloitwa Raila linapaswa kupigwa kwa kichwa liuawe ili lisiharibu serikali ya Uhuru,"* ni aina ya Vitendo Usemi Elekezi (VUE) kwa vile msemaji anajaribu kumfanya msemewa kutenda jambo kwa kutaja kile anachokitaka msemaji. Anawaambia wafuasi wake kupiga Raila kwa kichwa. Mifano mingine ni pamoja na kuamuru, kushurutisha, kushawishi, kuomba, kurai, kusihi, kukaribisha, kuuliza (kujaribu kumfanya msikilizaji kujibu), bembeja, sairi, kunasihi, sisitiza, pendekeza, ruhusu na chachawiza. Ili VUE kufaulu sharti tendo liwe la hiari na la kutendwa wakati ujao. Mwelekeo wake wa ufaafu huwa ulimwengu-kwa-neno.

Sitiari *"Jitu"* limetumiwa katika usemi huu kumrejelea mwanasiasa Raila. Kulingana na msemaji, Raila ni jitu ambalo ni baya, lililo sura mbaya na mharibifu ambalo likiachwa likiwa

hai basi huenda likaporomosha serikali yao. Msemaji anawachochea wasikilizaji wake ambao ni wafuasi wake dhidi ya mwanasiasa huyo kwa kudhihirisha sifa alizo nazo na ambazo ni hatari kwa serikali yao. Usemi huu, *"Jitu linaloitwa Raila linapaswa kupigwa kwa kichwa liuawe ili lisiharibu serikali ya Uhuru,"* *uhimiza wasikilizaji lengwa na kuwapotosha ili wachukuwe mtazamo uo* huo wa kutaka kusababisha mauaji.

William Wambugu mshauri wa Mukaru ward akizungumza mjini Tetu mnamo tarehe 12/7/2017 alisema *"Tunapaswa kumshinda mnyama huyu anayeitwa Raila ambaye anatuzuia kupata uongozi tena."*

Sitiari *"Tunapaswa kumshinda mnyama huyu anayeitwa Raila ambaye anatuzuia kupata uongozi tena,"* ni aina ya Vitendo Usemi Taarifa (VUT) kwa vile msemaji anajaribu kueleza jinsi Raila anawazuia kupata uongozi tena. VUT in aina ya sitiari ambayo matamko yanawasilisha hali ilivyo. Kwa hivyo, huonyesha imani ya msemaji kuhusu tamko lake. Katika kutoa tamko la aina hii, msemaji huwakilisha ulimwengu kwa namna anavyoamini ulivyo. Msemaji anaamini kuwa Raila akishindwa basi watapata uongozi. Kwa njia hii, anayafanya maneno yake kuoana na ulimwengu wake wa imani. Hii ina maana kwamba mwelekeo wa ufaafu wa VUT huwa neno-kwa-ulimwengu, kwa kuwa maelezo hulengwa yawiane na hali ilivyo ulimwenguni. Mifano ya VUT ni arifu, fahamisha, sadikisha, thibitisha, eleza, taja, fafanua, pambanua, sisistiza, ambia, kadiria, dai, taja, radidi na bashiri.VUT humfungamanisha msemaji kwenye ukweli wa proposisheni inayowasilishwa. Msemaji huonyesha hisia ya imani, ingawa kiwango cha imani cha msemaji chaweza kuwa tofauti. Kwa mfano, kiwango cha kuthibitisha huwa cha juu huku cha kubashiri huwa cha muda tu.

Sitiari ya kumwita mtu mnyama, imetumika katika usemi huu kumrejelea Raila kama kizingiti kikubwa kwa jamii hii cha kupata wanachokistahili ambacho ni uongozi. Msemaji anataka wamshinde mwanasiasa huyu ambaye ana msimamo tofauti nao. Hivyo basi, anawahimiza wafuasi wake wote wajitokeze ili wamshinde Raila katika uchaguzi mkuu wa 2017. Kulingana na msemaji, msimamo wa Raila ni kikwazo kwao cha kupata uongozi. Sitiari kama hii ya kuwadunisha wengine kwa kuwaita wanyama hutumika na wanasiasa wengi ili kujipatia kura dhidi ya wapinzani wao kwani mtu anapohusishwa na mnyama ni ishara tosha kwa wasikilizaji

kuwa mtu huyo hana sifa zinazostahili kuwa kiongozi. Kwa hivyo, kwa kuwalinganisha wapinzani wao na wanyama huwa wanawachochea wafuasi wao kutowapigia kura.

Mwakilishi wa wanawake wa Kaunti ya Homabay Gladys Wanga akiwahutubia wafuasi wao katika uwanja wa Musinde Muliro mjini Kakamega mnamo 24/6/2017 alisema *"Nyanza na Western inapaswa kuwa katika mstari wa mbele katika kampeni wa Nasa, na yeyote anayetoka katika miji hii miwili na anapinga atashughulikiwa vilivyo, yeyote anayetaka kuwa na tabia ya kupinga atakunjwa. Hatuna wakati wa kuvumilia mashetani ambao kazi yao ni kushikiana na maadui wetu."*

Usemi *"atakunjwa na hatuna wakati wa kuvumilia mashetani ambao kazi yao ni kushikiana na maadui wetu,"* unaweza kuchambuliwa kwa njia mbili; njia ya kwanza, kama Kitendo Usemi Elekezi na ya pili, kama Kitendo Usemi Taarifa. Kama Vitendo Usemi Elekezi (VUE), usemi huu unaonyesha wasemaji kama wanaojaribu kuwafanya wasemeo kutenda jambo kwa kutaja kile wanachokitaka wasemaji; "*na yeyote atakayepinga msimamo huu atashughulikiwa vilivyo*". *Yeyote anayetaka kuwa na tabia ya kupinga anapaswa kukunjwa*". Mifano ni pamoja na kuamuru, kushurutisha, kushawishi, kuomba, kurai, kusihi, kukaribisha, kuuliza (kujaribu kumfanya msikilizaji kujibu), bembeja, sairi, kunasihi, sisitiza, pendekeza, ruhusu na chachawiza. Ili VUE kufaulu sharti tendo liwe la hiari na la kutendwa wakati ujao.

Vilevile, sitiari *"atakunjwa na hatuna wakati wa kuvumilia mashetani ambao kazi yao ni kushirikiana na maadui wetu,"* ni aina ya Vitendo Usemi Taarifa (VUT) kwa vile wasemaji wanajaribu kueleza jinsi maeneo ya Nyanza na Western yanafaa kuwa ngome ya kampeni ya muungano wa Nasa na hawana "wakati wa kuvumilia mashetani ambao kazi yao ni kushirikiana na maadui wao wa kisiasa". VUT in aina ya sitiari ambayo matamko yanawasilisha hali ilivyo. Kwa hivyo, huonyesha imani ya msemaji kuhusu tamko lake. Katika kutoa tamko la aina hii, msemaji huwakilisha ulimwengu kwa namna anavyoamini ulivyo. Wasemaji wanaamini kuwa wakishughulikia yeyote anayepinga msimamo wa muungano wa Nasa basi utaratibu wa vitu vilivyopangwa utasalia. Kwa njia hii, wanayafanya maneno yao kuoana na ulimwengu wao wa imani. Hii ina maana kwamba mwelekeo wa ufaafu wa VUT huwa neno-kwa-ulimwengu, kwa kuwa maelezo hulengwa yawiane na hali ilivyo ulimwenguni. Mifano ya VUT ni arifu, fahamisha, sadikisha, thibitisha, eleza, taja, fafanua, pambanua, sisistiza, ambia, kadiria, dai, taja,

radidi na bashiri. VUT humfungamanisha msemaji kwenye ukweli wa proposisheni inayowasilishwa. Msemaji huonyesha hisia ya imani, ingawa kiwango cha imani cha msemaji chaweza kuwa tofauti. Kwa mfano, kiwango cha kuthibitisha huwa cha juu huku cha kubashiri huwa cha muda tu.

Katika kifungu hiki, walio na mtazamo tofauti na wasemaji wamelinganishwa kisitiari na mashetani. Kulingana na wasemaji hawa mashetani hawapaswi kupewa nafasi katika eneo hili kwani nia yao kuu ni kuharibu mpango uliokubaliwa ufuatwe. Kwa hivyo wasemaji wanawaonya wale ambao wanaweza kuwa na msimamo tofauti wajihadhari kwani wakipatikana watashughulikiwa vilivyo. Wanawachochea wafuasi wao kujitokeza ili kuwapiga na kuwanyamazisha wanaoweza kuwa katika kikundi cha chama cha Jubilee na ambacho hakitakikani katika maeneo hayo. Wanasiasa mara nyingi huwaita wanasiasa wenzao walio na umahiri mkubwa dhidi yao mashetani kwa lengo la kuwapa sifa mbaya zisizostahiliwa na jamii ili wapate ushindi katika uchaguzi wowote ule.

*'Majitu kutoka Magharibi'*

Sitiari *'Majitu kutoka Magharibi'* ni aina ya Vitendo Usemi Hisia (VUH) kwa vile katika aina hii ya Vitendo Usemi, msemaji huwasilisha hali yake kisaikolojia kupitia proposisheni. Mifano ni shukrani, msamaha, kufariji, pongeza, salimu, na kusikitika. Maana ya proposisheni ni jambo linalomwathiri msemaji au msikilizaji. Mwanasiasa huyu anataja watu wanaolengwa kama 'majitu' kuonyesha jinsi anavyowadunisha na kuwadharau. Si kawaida kusema "ninakufariji kwa msiba uliokupata ama ninakupongeza kwa kujaliwa mwana wa kiume", iwapo jambo linalohusika limemwathiri msikilizaji. VUH havina mwelekeo wa ufaafu wa upande wowote kwa sababu proposisheni hujitokeza kwa uchukuliaji wala haitangazwi. Mfano wa kitendo hisia ni kama vile: Hongera kwa hii tasnifu nzuri uliyoiandika.

Wakati wa uchaguzi mkuu wa 2017, wanasiasa kama Moses Kuria kutoka jamii ya Kikuyu walizoea kuwaita wafuasi wa Raila kutoka jamii ya Luo "*Majitu kutoka Magharibi*". Walitumia sitiari hii ili kuonyesha kuwa wafuasi wa mwanasiasa huyu ni wabaya, wenye kiburi na walio na mienendo hasi. Lengo lao lilikuwa kumhusisha mwanasiasa huyu na tabia hizi zisizofaa kwa mtu anayetaka kuchaguliwa kama kiongozi wa taifa. Kwa hivyo, madhumuni yao yalikuwa

kumnyima Raila kura hasa kutoka Mkoa wa Kati. Aghalabu wanasiasa hutumia sitiari kama hii kuwachochea wafuasi wao dhidi ya wapinzani wao kwa manufaa yao wenyewe.

Gavana wa Uasian Gishu bwana Mandago akizungumuza katika uwanja wa 64 mjini Eldoret mnamo tarehe 18/2/2017 alisema *"Watu wa maziwa tokeni nje ili kuondoa magugu yaliyo nyasini"*

Usemi *"Watu wa maziwa tokeni nje ili kuondoa magugu yaliyo nyasini"* ni aina ya sitiari ya Vitendo Usemi Elekezi (VUE) kwa vile msemaji anajaribu kumfanya msemewa kutenda jambo kwa kutaja kile anachokitaka msemaji *"watu wa maziwa tokeni nje ili kuondoa magugu..."* Kutokana na mila na utamaduni wao wa ufugaji, wanasiasa kutoka jamii ya Wakalenjin walitumia sitiari "watu wa maziwa," kujitambulisha. Hivyo basi waliwataka wafuasi wao kutoka maeneo yao watoke nje ili kuwafukuza watu kutoka makabila yaliyopinga chama cha Jubilee katika Mkoa huo wa Bonde la Ufa. Kauli hii ilieleweka kabisa na wafugaji Wakalenjin. *"Nyasi,"* zilirejelea makabila mengine yaliyoishi katika ardhi ya Wakalenjin. Wito wa viongozi hawa wa chama cha Jubilee kwa wafuasi wao *"wakate magugu nyasini"* ulikuwa uchochezi ulionekana wazi wa kuwashambulia waliotazamwa kama maadui ndani ya Mkoa wa Bonde la Ufa. Matumizi ya sitiari "kuondoa magugu nyasini" yalikuwa na maana ya kuwaua watu hao au kuwafukuza kutoka katika ardhi zilizokuwa za Wakalenjin kwa sababu za tofauti zao za kisiasa.

Aliyekuwa Gavana wa Kaunti ya Nyeri bwana Gakuru akiongea na wafuasi wa Jubilee mjini Nyeri mnamo tarehe 13/5/2017 alisema *"Kwanza apashwe tohara" (yaani Raila lazima atahiriwe)*

Sitiari *"Kwanza apashwe tohara" (yaani Raila lazima atahiriwe)* ni aina ya Vitendo Usemi Maamuzi (VUM) kwa vile ni usemi ambao ukifaulu kutendwa, matokeo yake ni upatikanaji wa proposisheni iliyotamkwa; yaani baada ya Raila *"Kupashwa tohara kwanza"* ndipo anaweza kuwa kiongozi. Sitiari *"kwanza apashwe tohara,"* hutumiwa na wanasiasa wengine ili kudunisha jamii ambazo hazishiriki mila na utamaduni huu wa kuitahiri jamaa zake. Jamii zinazoamini kuhusu mila na utamaduni huu, huwachukuwa watu wasiotahiriwa kuwa *"wajinga, waoga na walio na upungufu wa maarifa"*. Kwa hivyo, kulingana nao, watu kama hawa hawapaswi kuchaguliwa ili kuongoza taifa kwa wadhifa wa urais. Masharti ya kuchaguliwa kwao ni

kwamba wapashwe tohara kwanza ndipo wawe na hekima ya uongozi. Wasikilizaji wa kauli hii hivyo basi huchochewa kutomchagua *"ambaye hajatahiriwa,"* kutokana na imani potovu kuwa hana maarifa na uwezo wa kuongoza.

*"Ondoa mizizi"*

Usemi *"Ondoa mizizi"* ni aina ya sitiari ya Vitendo Usemi Elekezi (VUE) kwa vile msemaji anajaribu kumfanya msemewa kutenda jambo kwa kutaja kile anachokitaka msemaji; yaani *"ondoa mizizi"*. Diwani kutoka jamii ya Wakalenjin aliripotia watu kwenye kampeni iliyofanyika katika mji wa Soi kuwa akichaguliwa, chama cha Jubilee *"kitaondoa mizizi"* ya jamii iliyopinga chama hicho katika eneo hilo na hivyo basi kutakuwepo tu na kabila moja hapo. Matumizi ya sitiari hii inamaanisha wazi kuwa viongozi wa chama hiki walikuwa na nia ya kuwachochea wafuasi wao katika eneo hili kuwafukuza Waliowapinga na kuwaua ili wabaki wakizungumza kwa lugha moja kuhusu masuala ya kisiasa.

William Wambugu mshauri wa Mukaru ward akiongea mjini Tetu mnamo tarehe 12/7/2017 alisema *"Tuna nyoka ambaye tunapaswa kumwondoa"*

Usemi *"Tuna nyoka ambaye tunapaswa kumwondoa"* ni sitiari ya Vitendo Usemi Maamuzi (VUM) kwa vile msemaji anaashiria kuwa kuna nyoka wamegundua yupo miongoni mwao na suluhisho ni kumwondoa. Kwa kutamka msemaji husababisha mabadiliko katika ulimwengu kwa kutamka. Mifano mengine ni kutangaza hali hatari, kutangaza vita, kuunga mkono kumbukumbu za mkutano, kuahirisha kikao, kuachisha mwajiriwa kazi, kuteua, kupa jina, kubatiza, kumpata mshtakiwa na kosa, kuweka dau, kupa talaka, kubatiza, kutia nguvuni na kujiuzulu. Wanasiasa wengine wa chama cha Jubilee walisikika wakisema kuwa wana *"nyoka"* ambaye wanafaa kumwondoa. Hii ilikuwa sitiari ya kumrejelea kiongozi wa upinzani Raila na jamii yake. Nia kuu ya wanasiasa hawa ilikuwa ni kuwachochea wafuasi wao dhidi ya Wajaluo waliokuwa wakitazamwa kama mahasidi ambao hawakutakikana katika ngome za wanasiasa hawa. Kwa hivyo matumizi ya sitiari hii na wanasiasa hawa ilikuwa ni kuwahimiza wafuasi wao kuwafukuza Wajaluo katika ngome zao kupitia vita kwani *"nyoka"* huondolewa mahali kwa kupigwa.

Mbunge wa Gatundu bwana Moses Kuria akiongea katika kituo cha ununuzi wa Ithekahuno mjini Tetu tarehe 6/6/2017 alisema *"Njoo na usimame hapa ili unionyeshe ikiwa umetahiriwa na nyinyi njooni na panga ili kumwonyesha mtu huyu kuwa panga hazitumiwi tu kukata nyasi"*

Usemi "*nyinyi njooni na panga ili kumwonyesha mtu huyu kuwa panga hazitumiwi tu kukata nyasi"* ni sitiari ya Vitendo Usemi Elekezi (VUE) kwa vile msemaji anajaribu kumfanya msemewa kutenda jambo kwa kutaja kile anachokitaka msemaji *"Nyinyi njooni na panga ili kumwonyesha mtu huyu kuwa panga hazitumiwi tu kukata nyasi*". Msemaji wa usemi huu anawachochea wasikilizaji wake dhidi ya wajaluo ambao hawapashi tohara jamaa zake. Anatumia neno panga kisitiari ili kuwaeleza wasikilizaji wake kuwa watu kama hawa wanastahili kuawa. Kulingana na msemaji watu ambao hawajatahiriwa wanastahili kushambuliwa kwa panga au kutaabishwa. Maelezo ya msemaji yanatokana na msimamo wa kisiasa wa jamii lengwa ambao unatofautiana na wao. Kwa hivyo, mtazamo wake ni kuwa jamii lengwa hutofautiana nao kisiasa kwa kuwa hawajatahiriwa.

Aliyekuwa Gavana wa Kaunti ya Kiambu akizungumza mjini Thika mnamo tarehe 3/6/2017 alisema *"Una mazoea ya kumtusi Uhuru na ukijaribu tena nitakuja hadi kwa nyumba ya mama yako kukupata. Unatuma picha zake hata kwa mtandao wa kijamii huna hata maadili. Mwambie Raila aache upuuzi na huwa ninawaeleza kuwa mwache kutangamana na mtu ambaye hajatahiriwa kwa sababu akili zake huwa pale pale"*

Usemi "*mwache kutangamana na mtu ambaye hajatahiriwa kwa sababu akili zake huwa pale pale" ni* sitiari ya Vitendo Usemi Ahadi (VUA) na sitiari ya Vitendo Usemi Hisia (VUH). Ni sitiari VUA kwa vile msemaji anaahidi anayelengwa kuwa akijaribu kumtusi Uhuru tena atamkujia hadi kwa nyumba ya mama yake. VUA humdiriki msemaji kwa utendaji wa wakati ujao wa jambo lililomo kwenye proposisheni ya tamko lake (Bussmann, 1996). Huonyesha nia ya msemaji kutenda jambo fulani. Katika aina hii ya VU, msemaji hujihusisha na utendaji wa kitendo.

Vilevile, ni sitiari ya VUH kwa vile msemaji anajaribu kutoa hisia yake kuhusu watu ambao hawajatahiri; *"...huwa ninawaeleza kuwa mwache kutangamana na mtu ambaye hajatahiriwa kwa sababu akili zake huwa pale pale"*

Kulingana na msemaji, mtu ambaye hajatahiriwa ni mjinga, hana busara na ana fikra hasi. Msemaji anatumia usemi *"mtu ambaye hajatahiriwa"* kisitiari kurejelea jamii isiyotahiri jamaa zake(wajaluo). Hivyo basi anawaambia wasikilizaji wake kutotangamana na hawa watu kwani ni *"wajinga na wana fikra hasi"* kutokana na kutotahiriwa. Msemaji anawachochea wasikilizaji wake dhidi ya jamii lengwa kwa sababu ya msimamo wa mwakilishi wao ambao unatofautiana na wao. Kwa hivyo, maoni ya msemaji ni kuwa, mwakilishi wa jamii lengwa ana fikra hasi kwa sababu hajapashwa tohara.

Katika rekodi ya YouTube mwanasiasa mmoja aliyekuwa akiwania kiti cha udiwani Joab Omino mnamo tarehe 4/3/2017 ameripotiwa kusema *"Bungoma hata jina ni yetu. Kule Trans nzoia ni kwetu. Na vile wanasema Trans nzoia ni ya kimataifa, sisi tunawaambia watu wa Trans Nzoia kura ikipita, funga virago mwende kwenu. Wale wako Bungoma Jubilee ikishinda, wafunge viraka waende kwao "*

*"Funga virago mwende kwenu"* ni sitiari ya Vitendo Usemi Elekezi (VUE) maana wanaolengwa wanaamrishwa *"kufunga virago waende kwao."* Uchaguzi wa neno virago au matambara ni uamuzi unaoweza kuwa na athari ya kubadili neno lisilo na chuki katika hotuba kuwa ya chuki. Hii ni kwa sababu maneno haya huzungumzwa kwa dharau kwa watu wote wa kundi linalolengwa. Pia ni ujumbe mkali unaotumwa na msemaji kwa jamii zilizolengwa kwamba hazijakaribishwa kuishi miongoni mwao na tena wasiporudi makwao watajutia yatakayojiri.

*"Tunawaambia"*

*"Tunawaambia"* ni sitiari ya Vitendo Usemi Maamuzi (VUM) maana msemaji anatangaza vita ama hali ya hatari anapoanza kwa kusema "*tunawaambia.*" Haya ni matamshi ya *umoja 'sisi, wao, hao na yetu'.* Kwa kusema 'tunawaambia' msemaji anaonyesha kwamba anaongea kwa niaba ya watu wengine. Inaonekana pia kwamba ameweka mazungumzo yake kwa wasikilizaji wake wakati huo na pia kwa wasikilizaji wanaomsikia kutoka mahali pengine. Kwa kawaida msemaji hujenga 'SISI' dhidi ya 'WALE' na 'SISI' kama watu wema na 'WALE' kama wabaya. Mwelekeo wa wasiwasi wa msemaji kuelekea 'jamii nyingine' pia umetambulishwa katika maelekezo ya sitiari- *'tunawaambia'.* Mwongozo huu una athari ya kumtia na wote

anaowawakilisha katika nafasi bora zaidi na kudhalilisha wale wanaolengwa na hii ndiyo msingi wa tabia yao ya kudharau wengine.

*"Bungoma hata jina ni yetu. Kule Trans-Nzoia ni kwetu. Na vile wanasema Trans-Nzoia is cosmopolitan, sisi tunaambia watu wa Trans-Nzoia kura ikipita, funga viraka mwende kwenu. Wale wako Bungoma Jubilee ikishinda, wafunge viraka waende kwao".*

Usemi huu kwa jumla ni sitiari ya Vitendo Usemi Maamuzi (VUM) kwa vile ni aina ya kitendo usemi ambacho, ikiwa kitafaulu kutendwa, matokeo yake ni upatikanaji wa proposisheni iliyotamkwa kama athari ya kutamkwa kwake tu. Kwa kutamka maneno haya, msemaji husababisha mabadiliko katika ulimwengu kwa kutamka. Kwa mfano, sitiari hii inatangaza hali ya hatari na kutangaza vita *"funga viraka muende kwenu".*

Sitiari zilizotumika katika hotuba hii ni zifuatazo:

*"Funga viraka mwende kwenu"*

Kauli hii inaeleza wazi kuwa jamii lengwa(Wakikuyu) inaambiwa kuwa wajitayarishe kuchukuwa vitu vyao vyote kuondoka katika eneo hilo baada ya uchaguzi kumalizika. Pia ni ujumbe mzito unaowasilishwa na msemaji kwa watu wa jamii lengwa kuwa hawatakikani kabisa katika eneo hilo na ikiwa hawataondoka basi wajitayarishe kutaabika. Hii inatokana na sababu kuwa msimamo wa kisiasa uliochukuliwa na jamii lengwa ni tofauti na ya msemaji na wafuasi wake katika eneo hili.

*"Funga viraka"*

*"Funga viraka"* ina maana ya kuanza safari kwa lugha ya Kiswahili. Katika hotuba ya kisiasa, wasemaji wanatumia usemi huu kuzijulisha jamii zilizolengwa kwamba zinapaswa kuondoka kwenye ardhi za wenyeji kabla ya kushambuliwa. Ni aina ya kauli ya kichochezi inayotarajiwa kuhamasisha jamii ya wenyeji dhidi ya jamii nyingine na kuwaogopesha jamii ndogo ili kukimbia wakati wa kupiga kura ili kutopiga kura dhidi ya jamii ya wenyeji. Maneno *"funga viraka"* wakati yanatumiwa na msemaji, yanaonyesha kwamba jamii zilizolengwa hazitakikani tena na lazima zirejee kwenye ardhi za mababu zao.

Mbuge wa Mbita Bi Millie Odhiambo akizungumza na waandishi wa habari bungeni alisema "*Uhuru Kenyatta ni fisi na ni mwizi and we don't care about him and we don't respect him. This is not a police state; he can not intimidate us.*"

Sitiari *'Uhuru Kenyatta ni fisi na ni mwizi'* ni aina ya Vitendo Usemi Hisia (VUH) kwa vile katika aina hii ya Vitendo Usemi, msemaji huwasilisha hali yake kisaikolojia kupitia proposisheni. Mifano ni shukrani, msamaha, kufariji, pongeza, salimu, na kusikitika. Maana ya proposisheni ni jambo linalomwathiri msemaji au msikilizaji. Mwanasiasa huyu anataja Rais kama '*fisi na mwizi*' kuonyesha jinsi anavyomdunisha na kumdharau.

Wakati wabunge wa Jubilee walipaswa kupitisha sheria bungeni inayoruhusu Tume ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) kutotumia njia ya kielektroniki, Mbunge wa Mbita alimrejelea Rais kama '*fisi na mwizi*' ili kuonyesha jinsi anavyomdharau na kumdunisha. Lengo lake lilikuwa kumhusisha rais na tabia zisizofaa kwa mtu anayetaka kuchaguliwa kama kiongozi wa taifa. Kwa hivyo, madhumuni yake yalikuwa kuonyesha wapiga kura na wafuasi wao katika muungano wa NASA kuwa Rais hakushinda uchaguzi wa mwaka wa 2013 kwa vile Tume ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) haikuanda uchaguzi wa ukweli na wa haki.

Sitiari *JUBILEE ni chama cha maendeleo na kwamba wao ni nyani* ni aina ya Vitendo Usemi Hisia (VUH) kwa vile katika aina hii ya Vitendo Usemi, msemaji huwasilisha hali yake kisaikolojia kupitia proposisheni. Kupendekeza chama cha Jubilee na kuita vyama vingine Nyani, msemaji anatoa hisia zake kuhusu msimamo wake wa kisiasa. Vile vile, anaonyesha hali ya kudharau watu wengine walioko kwenye vyama vingine.

Gavana wa Homabay bwana Cyprian Awiti akiongea mjini Homabay mnamo tarehe 3/6/2017 alisema "*Naambia Rege alete hao chokoraa wa Jubilee HomaBay ndio ajue kwa nini punda hakuna mapembe*". Usemi huu kwa jumla ni sitiari ya Vitendo Usemi Maamuzi (VUM) kwa vile ni aina ya kitendo usemi ambacho, ikiwa kitafaulu kutendwa, matokeo yake ni upatikanaji wa proposisheni iliyotamkwa kama athari ya kutamkwa kwake tu. Msemaji hapa anatangaza hali ya hatari kwa wanaolengwa kwamba wakithubutu kufika HomaBay watatendewa vibaya.

Aliyekuwa seneta wa Mombasa bwana Hassan Omar akiongea mjini Mombasa mnamo tarehe 6/6/2017 alisema "*Joho, si mume kamili, hana elimu na ni kiroboto*" Usemi huu ni sitiari ya

Vitendo Usemi Hisia (VUH) kwa vile msemaji anatoa matamshi ya matusi dhidi ya mwanasiasa Joho. Isitoshe, anawaambia wasikilizaji wake kuwa mwanasiasa huyo amekosa uwezo wa kuongoza kielimu na kimaadili na hivyo basi anawatahadharisha dhidi yake.

### 3.1 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia uchanganuzi wa data kuhusu semi za sitiari za Kiswahili zilizotumiwa na wanasiasa katika kampeni na jinsi zinavyochangia kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya. Jinsi ilivyofafanuliwa katika sura ya kwanza kwamba msingi wa kinadharia uliotumiwa katika utafiti huu ni wa vitendo usemi. Nadharia ya vitendo usemi imetumiwa katika utafiti huu kulingana na Austin (1962) na kufafanuliwa kwa kina na Kent (2014). Tumechambua jinsi sitiari za Kiswahili zinatumika na wanasiasa katika hotuba zao za kisiasa na jinsi zimechangia kuleta chuki dhidi ya jamii nyingine. Uchambuzi zaidi wa sitiari kulingana na malengo ya utafiti huu umefanyika katika sura ya nne.

# SURA YA NNE

# JINSI LUGHA YA KISWAHILI NA MATUMIZI YA SITIARI ZA KISWAHILI YANAVYOCHANGIA KUENEA KWA KAULI YA CHUKI KATIKA SIASA NCHINI KENYA

## 4.0 Utangulizi.

Sura hii inazungumzia matokeo kutoka kwa uchanganuzi wa data katika sura ya 3. Mjadala utazingatia malengo ya utafiti huu.

## 4.1 Jinsi lugha ya Kiswahili inachangia kuenea kwa kauli ya chuki katika siasa nchini Kenya

Wanasiasa wa Kenya wamekuwa wakitumia masuala ya ndani kwa kawaida ili kuweka uhasama dhidi ya jamii zinazoishi pamoja kwa kutumia lugha iliyopangwa kuhamasisha na kuwashambulia wapinzani wao. Katika kipindi cha uhuru hadi mwaka wa 1991, Kenya ilikuwa nchi iliyotawaliwa na chama kimoja hali iliyofanya vyombo vya habari kutokuwa na uwezo wa kuripoti wazi na ambayo wanasiasa walio na mamlaka walikuwa na uhuru wa kuvamia wapinzani au wakosoaji wao kimabavu au hata kwa maneno. Wakati shinikizo liliwekwa kubuniwa kwa siasa ya vyama vingi, lugha ya mazungumzo ya kisiasa yaliyotokea kwanza kutoka kwa Rais Moi na wafuasi wake ndani ya KANU na kisha kuenea katika wasomi wa kisiasa wenye mashindano ilikuwa ni ya matusi, tishio na mashtaka. Hali hii pia ilishuhudia ufisadi, uadui wa kikabila, utakaso wa kikabila, mauaji na makosa ya jinai.

Kenya ina makabila zaidi ya 42 yanayoishi pamoja kote nchini. Mengi ya makundi haya ya kikabila yana lugha zao ambazo yanatumia kuzungumza. Katika hali ambayo sasa iko Kenya, Kiingereza ni lugha ya kifahari, ambayo ustadi wake ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kiswahili, kwa upande wake, kama lugha ya kitaifa ya Kenya na sasa lugha rasmi pamoja na Kiingereza, hutumiwa kwa mawasiliano kati ya watu wa makabila mbalimbali, katika mahakama, katika shule ya msingi, na katika maeneo kama soko, majirani, sekta ya usafiri na kazini. Zile lugha nyingine za kiasili za Kenya isipokuwa lugha ya Kiswahili, hutumiwa katika familia, jamii ya ndani, shule ya chekechea, kozi za kufunza watu wazima, kanisa, vyombo vya habari, na mahali pa kazi. Mara nyingi, wagombea wa viti mbalimbali vya kisiasa wamekuwa

wakitumia tofauti hizo katika lugha ili kugawanya wananchi kwa kutumia hotuba za kichochezi au za madharau ili kubadilisha jamii zao dhidi ya wapinzani kutoka kwa jamii nyingine za kikabila (Oddsdottir, 2014).

Kutoka kwenye data iliyotolewa katika sura ya tatu, ni dhahiri kwamba baadhi ya wanasiasa hutumia lugha ya Kiswahili kuchochea vurugu ili wapate umaarufu kisiasa. Kwa mujibu wa Odiwuor (2002), lugha ya kiswahili na hasa utumiaji wa sitiari za kiswahili ni silaha yenye nguvu ambayo inaweza kutumiwa na kikundi kimoja ili kuonyesha ubabe wao au kuendeleza mitindo ya uongozi fulani kwa nia ya kuimarisha umaarufu wao. Uteuzi wa maneno unaweza kutumika kwa ufasaha kuibadilisha tabia, matendo na mtazamo wa watu. Kwa kufanya hivyo, misamiati hiyo inaweza kutumika kudhalilisha au kuboresha hali ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Viongozi wa kisiasa wana ushawishi mkubwa kwa jamii na wengi wa wafuasi wao wanaamini kile wanachosema. Hii inaonekana wazi kwenye matokeo ya vitendo fulani vinavyotokana na maneno fulani yanayohusiana nao na ambayo huunda msingi wa imani yao ya kisiasa ambayo hayabadiliki.

Katika nchi ya Kenya, lugha kama mahitaji ya kimsingi huacha maswali mengi bila ya majibu - hususan katika mikusanyiko ya kisiasa. Wanasiasa wengi kwa jitihada za kuhalalisha nafasi zao huacha ujumbe wao kutegemea mtazamo wa msikilizaji ambaye mara nyingi hana la kufanya au kuamua. Matamshi ya kisiasa hutumiwa kwa namna ya kunyima wasikilizaji haki ya kujielewa wenyewe na mazingira yao. Katika ulingo wa kisiasa ambao uamuzi unapaswa kuwa jambo muhimu, wengi wa wasikilizaji (ambao wengine hawajui kusoma kabisa na wengine wanajua kidogo tu kusoma na kuandika) wanaachwa bila uamuzi isipokuwa kuchukua kile kinachosemwa kwa maana yake halisi. Kwa mfano, baada ya kufunguliwa kwa Sehemu ya 2 (A) ya katiba ya Kenya ya kitambo ambayo iliruhusu demokrasia ya vyama vingi, maneno yafuatayo ya kisiasa yalitumiwa na viongozi wa kisiasa (Yamewekwa katika Kiswahili na Kiingereza).

| Neno | Maana kisiasa |
|---|---|
| Vyama vingi (Multi-party) | Ukabila (Tribalism) |
| Siasa mbaya (Bad politics) | Maisha mabaya (Bad life) |
| Siasa nzuri (Good politics) | Maisha mazuri (Good life) |
| Maadamano (Demostrations) | Umwagikaji damu/vita (Blood shed//war) |

Aina ya tafsiri na maana zinazohusiana na sitiari hizi za kisiasa haziruhusu mtu mwenye upungufu kwa mambo ya siasa na mifumo ya kisiasa kufanya chaguo lolote na kwa hiyo kuchukua mwelekeo tofauti na yanayotarajiwa. Kufafanua kwamba vyama vingi humaanisha ukabila ni kuweka vikwazo kwa maana na hutumika kwa njia ya kuwaweka wale wasioelewa operesheni hii ya siasa mbali na kukubali au kufanya uchaguzi kati ya vyama vingi na mfumo mwingine wowote. Ukabila unaweza kuwa tu matokeo ya vyama vingi kulingana na jinsi vyama hivyo vinavyotumika. Pili, maandamano hayana maana ya umwagikaji wa damu au vita. Ingekuwa rahisi kuelezewa kwamba ni njia ya watu kuonyesha maoni yao kwa kuunga mkono au kupinga mswada fulani.

Njia wazi ya kuelezea maana ya maneno haya yamezuiliwa kwa makusudi na isiyoelezewa kwa nia ya kushikilia nafasi fulani za kisiasa na viongozi. Sitiari za kisiasa nchini Kenya kwa muda mrefu zimekuwa zikitumika kunyima watu haki yao ya kutumia lugha kama chombo cha kujielewa wenyewe pamoja na mazingira yao na utangamano wa kisiasa. Huenda labda hii ndiyo sababu mpito wa kisiasa nchini Kenya unakabiliwa na ukabila.

### 4.2 Mchango wa sitiari za Kiswahili katika kuenea kwa kauli za chuki katika siasa nchini Kenya

Kama ilivyoelezwa katika sura ya tatu, lugha ya siasa za Kenya imetambuliwa na sitiari, methali na nyanja nyingine za msamiati. Kulingana na ufafanuzi wa Lakoff na Johnson (1980) kwamba sitiari ni "kuelewa na kushughulikia kitu kimoja kwa kutumia kitu kingine", inamaanisha kwamba sitiari inaweza pia kutazamiwa kama "dhana au 'mtazamo'. Kulingana na Hart (2010), sitiari ina viwango vitatu vya ufafanuzi tofauti wakati unatumika katika hotuba; Lugha, ufahamu,

na kiwango cha kuelewa vitu kikawaida. Katika ngazi ya lugha, sitiari inamaanisha neno au maneno ambayo husababisha mvutano wa semantiki kwa njia ya upatanisho au kujidhihirisha.

Kikundi muhimu kwa ajili ya utafiti huu ni kile kinachoonyesha sitiari za Kiswahili zinazopatikana katika hotuba ya kisiasa. Katika kikundi hiki, hebu tujadili mwelekeo unaojulikana ndani ya mazingira ya kisiasa ya Kenya kama ilivyoonyeshwa na takwimu zilizokusanywa, yaani, *'majitu, funga virago mwende kwenu'*na kutaja jamii nyingine kama *madoadoa.* Mifano hii itatusaidia kuonyesha jinsi sitiari za Kiswahilizinatumiwa nchini Kenya kueneza hotuba ya chuki katika siasa. Katika duru za kisiasa za Kenya, kutajwa kwa jamii fulani kama 'madoadoa' kunajulikana sana. Kutaja watu wa jamii fulani kutumia sitiari aina hizi zimetajwa hapo juu ni mchakato wa kupunguza wanadamu kuwa 'vitu' au vyombo visivyo na uhai. Matamshi kama haya yana uhusiano wa karibu na jinsi wasikilizaji wa kauli hizo wanavyowatendea wale wanaoitwa 'madoadoa'. Pili, dhana ya doa au uchafu pia inathibitisha wazo la alama fulani zisizohitajika (kitu ambacho hakitakikani mahali) ambacho kinahitaji kuondolewa. Kwa kugawa watu wa jamii moja kama madoadoa, wale wanaojulishwa na msemaji wanakuwa na mtazamo wa kuondolewa kwa doa kama kitu sahihi cha kufanya. Vilevile, dhana hii huelekea kuhalalisha vitendo vya vurugu dhidi ya jamii nyingine. Kwa vile hao ni madoadoa ambayo yanazuia picha au utaratibu mzuri.

Mfano wa onyo kwa jamii fulani *'wafunge virago waende kwao'* ni kati ya mifano inayojulikana zaidi ya matamshi ya chuki katika siasa nchini Kenya. Kwa vyovyote sitiari hizi zinaibua maana sawa, na zinaweza kufasiriwa kwa njia sawa. Usemi 'funga virago' unaweza kumaanisha kuwa watu wa jamii inayolengwa wanahatarishwa na hawana haki yoyote. Vile vile, msemaji anasema kwamba atakayekataa kufuata amri zake atajuta mwenyewe kutokana na athari zitakazotokea.

Kwa hivyo, kutaja au kuwaita watu wa jamii inayolengwa kama nyani, magugu, au madoadoa na kuhitaji wengine 'wafunge virago warudi kwao', inaonyesha kuwa watu wa jamii nyingine hawana haki yoyote. Hatimaye, maneno hayo yataonekana kuwa ni kauli ya chuki. Kwa mtazamo wa mifano hii ya wazi ya sitiari kama inavyotumiwa katika hotuba ya kisiasa nchini Kenya, ni dhahiri kwamba sitiari za Kiswahili huchangia sana katika kueneza kauli ya chuki katika siasa nchini Kenya. Matumizi ya sitiari za Kiswahili na wanasiasa katika hotuba za chuki

zinaweza kusemwa ni njia ya kuepuka mashtaka kama vile wengi wao wameonyesha wakati wa kupelekwa mahakamani kuwa wamechukuliwa nje ya muktadha.

### 4.3 Jinsi lugha ya Kiswahili inaweza kutumika kama chombo katika kuleta umoja wa kijamii nchini Kenya

Lugha ni moja ya vitu vinavyofafanua tabia ya mwanadamu. Thamani yake ya kuwasiliana katika mazingira tofauti inaelezea kikamilifu nia na matendo ya mtumiaji. Katika jamii nyingi, lugha hutumiwa kuzungumza, kuhifadhi mila na utamaduni wa kitamaduni, na kusambaza mila kutoka kwa kizazi moja hadi kingine. Lugha inaweza kutumika kuunganisha watu, hasa wale wanaotoka kwa kikundi kimoja lakini pia inaweza kutumika kugawanya watu kwa misingi ya kikabila ikiwa itatumika vibaya. Kenya ni nchi tajiri katika lugha mbalimbali za kikabila. Hata hivyo, lugha za Kenya zimewekwa katika vikundi vitatu: lugha za kiasili, Kiingereza na Kiswahili.

#### Jukumu la lugha za kiasili za Kenya

Hivi sasa, lugha za asili za Kenya zinabaki imara na kutumika katika familia na katika kijiji na kuendelea kuhifadhi nafasi kama "lugha ya kibanda au mtaa", kukopa maneno kutoka Breton (1991). Lugha za kiasili hutumiwa katika ngazi ya kijiji na wazazi, watu wakongwe na jamaa nyingine kijijini; hutumiwa kwa utani na kama ishara za utambulisho wa kawaida au wa karibu (Breton 1991, pp.171-172). Katika miji mikubwa kama vile Nairobi, sherehe za kitamaduni hutoa furaha ya upishi, muziki na ngoma kutoka kwa makundi mbalimbali ya kikabila na inakuwa njia maarufu ya kukumbusha wenyeji wa miji ya urithi wao wa kitamaduni na lugha. (Ingawa kwa baadhi yao ni mila tu ya wazazi wao).

Kwa kuongezea, vituo vya redio havitangazi tu katika lugha mbalimbali za asili (Gikuyu, Dholuo, Kikamba, Kiluhya, nk) lakini pia, kwa kushirikiana na kampuni ya Safaricom (mtoa huduma ya simu ya mkononi nchini Kenya) inayoandaa maonyesho barabarani kutoka kwa eneo moja hadi jingine, wakati wanahabari pamoja na wanamuziki huburudisha watu kwakutumia lugha za kiasili.

Zaidi ya hayo, ingawa mfumo wa kisheria wa Kenya hauna nafasi ya mkalimani wa mahakama rasmi, lugha za kiasili hutumiwa sana katika mahakama, hivyo zinahitaji matumizi ya mkalimani

asiye rasmi. Wakati wa kesi za kisheria, mtuhumiwa, au hata shahidi, anaweza kutumia lugha ya asili ili kutoa ushahidi au kushuhudia. Kwa kawaida ni bora kupata karani wa mahakama ambaye anaongea lugha asili kutafsiri hata wakati hakimu anayeongoza anaelewa lugha ya shahidi au mtuhumiwa.

Mwisho, baadhi ya lugha za asili za Kenya zinaonekana kuwa zimeanza kujisisitiza katika vitabu. Katika uhusiano huu, Webb na Kembo-Sure (2000, pp. 46-52) ilibainisha kuongezeka kwa machapisho katika Gikuyu, Dholuo na Luhya. Hata hivyo, wakati wa kutambua matukio hayo ya matumizi ya lugha za asili, inapaswa pia kuongezwa kuwa kwa sababu ya mchakato wa miji, lugha hizi zimeendelea kusukumwa zaidi kwa Kiswahili na Kiingereza kwa maeneo ya jamii kijijini.

**Jukumu la Kiingereza nchini Kenya**

Katika Kenya, Kiingereza ni lugha ya utawala, biashara ya kimataifa, diplomasia, biashara, na mafundisho katika mfumo wa shule hadi chuo kikuu (isipokuwa kwa miaka mitatu ya kwanza ya shule ya msingi katika maeneo ya vijijini nchini). Imekuwa lugha rasmi ya Kenya tangu uhuru wa nchi mwaka wa 1963, na hali yake maalum iliyothibitishwa katika Katiba. Kwa mfano, kwa mujibu wa Katiba ya Kale ya Kenya ya mwaka 1983 (ambayo ilikuwa imara hadi mwisho wa Agosti 2010) pamoja na Kiswahili, Kiingereza kilikuwa lugha ya Bunge na kilitambuliwa na kila Mjumbe wa Bunge.

Lakini hata Katiba ya sasa (iliyoadhimishwa tarehe 27 Agosti 2010), wakati wa kutambua Kiswahili (katika kifungu cha 7) kama lugha ya kitaifa na, pamoja na Kiingereza, kama lugha nyingine rasmi ya Kenya, bado inaweka Kiingereza katika nafasi ya kifahari zaidi kuliko ile ya lugha nyingine zote zinazotumiwa nchini Kenya. Katika kifungu chake 259 (2), inasema hivi: "Ikiwa kuna mgongano kati ya tafsiri tofauti ya lugha ya Katiba hii, tafsiri ya lugha ya Kiingereza itazingatiwa".

Pamoja na lugha ya Kiingereza kuwa lugha ya kipekee nchini Kenya, bado ni lugha ndogo, ambayo hueleweka na idadi ndogo tu ya watu wa nchi na hutumiwa hasa kwa mandhari ambayo hayapatikani na tamaduni za jadi za Kenya. Kwa mfano, sherehe za ushirika wa jadi (kama vile harusi), sherehe za kutahiriwa na ibada za jadi za mazishi haziwezi kufanywa kwa ufanisi kwa

kutumia Kiingereza. Ikiwa sherehe ya ushirikiano wa jadi inafanyika kwa Kiingereza, basi hii inafanywa tu ili kumtumikia mkwe au bibi na familia zao, ambao hawawezi kushirikiana na utamaduni huo. Kwa sherehe kama vile kutahiriwa na kuzikwa, kutumia Kiingereza ni nje ya swali, kwa sababu lugha ya asili hufanya sehemu muhimu ya sherehe. Hata hivyo, ni lazima tukubali kwamba idadi ya wasemaji wa Kiingereza imeongezeka kwa kasi, kutokana na tukio moja muhimu: kukomesha ada za shule kwa shule nzima ya msingi mwaka 2003. Hii imesababisha kuongezeka kwa idadi mpya ya usajili katika shule, ambayo iliongezeka "kutoka milioni 5.9 mwaka 2002 hadi milioni 8.8 (wavulana milioni 4.5 na wasichana milioni 4.3) mwaka 2009" (Kenya Private Sector Alliance 2011, p.21). Hii inaweza kumaanisha kwamba idadi ya wasemaji wa Kiingereza nchini Kenya imeongezeka kwa kasi.

Umuhimu wa ongezeko hili kwa namba liko katika ukweli kwamba nchini Kenya, Kiingereza ni somo mahususi,hata ingawa sio jumuishi, hufunzwa shuleni. Hali hii pia inaweza kuambatanishwa na Kiswahili, ambayo, ingawa hufundishwa rasmi shuleni, pia inachukua zaidi mawasiliano ya kila siku kwenye barabara na katika taasisi za uzalishaji (kazi) na biashara (soko) kuliko shule. Kwa hiyo, wakati Kiingereza mara nyingi hutumiwa katika hali rasmi, Kiswahili mara nyingi hutumiwa kwa wasio rasmi.

**Jukumu la Kiswahili nchini Kenya na jinsi inaweza kutumiwa kuleta uwiano**

Nchini Kenya, lugha ya Kiswahili hutumika kama lugha rasmi na lugha ya kitaifa. Hii ina maana ya kuwa Kiswahili kinachangia pakubwa katika mawasiliano ya kila siku nchini Kenya. Katika jamii ambazo zimeundwa kwa vikundi vingi vidogo vya kikabila kama vile Kenya, wanasiasa wana mazoea ya kutumia lugha ya Kiswahili kama mojawapo za lugha ambazo zinaeleweka na watu wengi nchini kuwavutia jamii zao kuwapigia kura au kusaidia ajenda zao za kisiasa.

Kama lugha ya pili rasmi na lugha ya kitaifa ya Kenya, kiswahili kina jukumu tofauti na ile ya lugha zingine za asili nchini licha ya kuzungumzwa na wachache wa wakenya kama lugha ya kwanza. Kama lugha ya kitaifa na lugha rasmi, kiswahili ni lugha ya kwanza kabisa kutumika kama lugha kati ya watu wa makabila mbalimbali. Lakini pia hutumiwa katika mahakama na kama lugha ya elimu ya chini ya shule ya msingi katika maeneo mengine ya ulimwengu, na katika maeneo ya kawaida kama vile soko, jirani, usafiri, sekta, kazi, nk (Reh, 1981).

Leo, kiwango cha juu cha kiswahili kipo pamoja na aina nyingine zisizo sanifu. Aina mbalimbali hupewa hasa shule kama lugha ya pili. Wakati huo huo, aina tofauti ya Kiswahili huzungumzwa kando ya pwani ya Kenya na visiwa vya karibu kama lugha ya mama. Lakini pia kuna aina tofauti za kiswahili zisizo sanifu, zinazotumiwa na jamii nyingi katika maeneo ya kisiwani ya Kenya. Kwa sababu hii, mtu anawezapata kuwa katika miji mikubwa ya Kenya, watu ambao lugha yao ya kwanza ni moja ya aina hizi zisizo za kiswahili sanifu.

Kulingana na uchambuzi wa makundi ya lugha zilizopo Kenya na jinsi zinazotumiwa katika ushirikiano wa kila siku kati ya wananchi, inaonyesha kwamba serikali inaweza kutegemea na kutumia lugha ya Kiswahili ili kukuza umoja kati ya jamii zinazoishi Kenya. Hii ni kwa sababu Kiswahili ndicho lugha ya kiasili nchini Kenya ambayo imetambulika na katiba kama lugha ya taifa ambayo kila jamii inatumia kuzungumza. Kiswahili kinajulikana na wengi nchini Kenya. Uwiano huu kwa kutumia lugha ya Kiswahili, unaweza kupatikana kwa njia ya kupitishwa kwa sera za ushirikiano wa kijamii na utangamano ambao unakubali tofauti zetu za kiutamaduni na lugha wakati tunakubaliana na mambo ambayo yanatuleta pamoja kama taifa. Kufundisha lugha ya Kiswahili shuleni ni sera moja ambayo inaweza kuhakikisha kila jamii inaweza kuwa na mazungumzo kwa lugha ya Kiswahili pamoja na kutangamana kila siku na kushirikiana. Kujifunza lugha ya Kiswahili ni hali bora ambayo inaweza kufanya jamii kuishi nchini Kenya kwa amani na kwa usawa.

### 4.4 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili matokeo ya data iliyokusanywa kuhusiana na mchango wa sitiari za Kiswahili katika kauli ya kichochezi katika siasa nchini Kenya. Data hizi zimechanganuliwa katika sura ya tatu. Hasa, uchambuzi huu umefafanua matokeo yafuatayo:

a) Lugha ni sehemu muhimu katika hotuba ya kisiasa na hivyo huchangia sana kuenea kwa hotuba ya chuki katika siasa nchini Kenya. Matamshi yote ya kisiasa yameunganishwa kwa lugha na hivyo matumizi ya lugha yanaweza kuchangia sana kuenea kwa hotuba ya chuki katika siasa.

b) Sitiari za kiswahili zimebainishwa kueneza hotuba ya chuki nchini Kenya kwa njia mbili. Njia ya kwanza inahusiana na sitiari ya kielelezo inayopatikana katika mazungumzo ya wanasiasa ambayo yanajumuisha maneno kama *nyani na fisi.*

**c)** Kenya inaweza kutumia lugha ya Kiswahili kuhubiri amani, umoja na kuleta ushirikiano wa kijamii. Kwa kuiga mawasiliano mazuri na kupinga hotuba ya chuki katika hotuba ya kisiasa, Kenya inaweza kufikia ushirikiano wa kijamii kupitia lugha.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii ya mwisho tunatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho, mapendekezo na matarajio kwa ajili ya utafiti zaidi juu ya mada ya kauli ya chuki katika siasa nchini Kenya.

## 5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulikuwa unashughulikia mchango wa sitiari za Kiswahili katika kauli ya chuki katika siasa nchini Kenya.

Madhumuni yalikuwa: Kubainisha jinsi lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya taifa na lugha rasmi huchangia kueneza kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya; kuchunguza mchango wa sitiari za Kiswahili katika kueneza kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya; kuchunguza jinsi lugha ya Kiswahili inaweza kutumiwa kama chombo cha kuleta uwiano wa kijamii nchini Kenya

Yafuatayo ni makisio: lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya taifa na lugha rasmi huchangia kueneza kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya. Sitiari za Kiswahili katika kueneza kauli za kichochezi katika siasa nchini Kenya. Lugha ya Kiswahili inaweza kutumiwa kama chombo cha kuleta uwiano wa kijamii nchini Kenya.

Madhumuni ya utafiti umebainisha kuwa lugha ya Kiswahili inachangia sana kuenezwa kwa hotuba ya chuki nchini Kenya kwa vile jamii tofauti zina misamiati za Kiswahili ambayo inachochea chuki ikitumiwa dhidi ya jamii nyingine inayochukiwa. Kwa mfano, kila wakati watu wa jamii wanapotaka kuhimiza watu wao kuinuka dhidi ya changamoto fulani au kukidhi matarajio ya jamii, wanawazungumzia kwa kutumia maneno ya kidharau ambayo ni kiasi cha kuchukiza, hasa wakati unaelekezwa kwa jamii nyingine. Utafiti umethibitisha kwamba sitiari za Kiswahili zina mchango mkubwa katika hotuba ya chuki kwenye siasa nchini Kenya. Hii ni kwa sababu matumizi ya misemo kama 'funga virago mrudi kwenu' na maneno kama 'madoadoa' yamekuwa kwenye mazungumzo ya kisiasa nchini Kenya tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi mwaka wa 1992. Matumizi ya sitiari na maneno kama hayo yamekuwa yakitumiwa

kuchochea jamii nyingi kwa faida ya kisiasa. Vilevile, utafiti umebainisha kuwa lugha ya Kiswahili ni chombo chenye nguvu ambacho kinaweza kutumika katika kuleta watu pamoja na kukuza ushirikiano wa kijamii ndani ya nchi. Hatimaye, utafiti umefafanua kwamba kuna changamoto kadhaa zinazoathiri utekelezaji wa sera na sheria za hotuba za chuki. Changamoto hizo ni pamoja na ufafanuzi usio wazi wa kisheria wa hotuba za chuki, kuchelewa kwa kutoa uamuzi katika kesi za hotuba ya chuki mahakamani kwa miaka mingi, adhabu nyepesi kutolewa kwa wenye wako na hatia ya hotuba za chuki, na kuachwa kwa kesi za chuki kutokana na uchunguzi duni, ufisadi, au mfumo wa kisheria usiofaa katika mashtaka ya kesi za hotuba za chuki.

## 5.2 Hitimisho

Ikiwa kuna jambo ambalo historia imetufundisha nchini Kenya ni kwamba hotuba ya chuki inakuja na gharama kubwa ya kulipwa. Kutoka kwa mapigano ya kikabila ya 1992 yaliyosababisha vifo vya watu 5,000 na watu 75,000 kufurushwa makwao, mvutano wa kikabila wa 1997 kati ya Luo, Kikuyu na Kalenjin, na unyanyasaji wa baada ya uchaguzi wa 2007-2008 pia ulisababisha madhara makubwa kwa vile angalau watu 1500 waliuawa na kati ya watu 180,000 na 600,000 walihamishwa. Migogoro hii yote inafuata mfumo mmoja na njia moja ya kichochezi; wanasiasa, wasomi wa jamii na vyombo vya habari vimechangia kuleta mvutano kwa njia ya sitiari ya kuchochea na kusababisha vurugu. Matamshi kama haya yanatoka kwa upeperushaji wa ujumbe wa simu (SMS) na uchochezi kutoka kwa wanasiasa.

Sitiari za Kiswahili zimebainishwa kueneza hotuba ya chuki nchini Kenya kwa njia mbili. Njia ya kwanza inahusiana na sitiari ya kielelezo inayopatikana katika mazungumzo ya kikabila ambayo yanajumuisha sitiari za wanyama zenye maneno kama *Nyani, fisi, magugu, kunguru, mwizi, watu wa maziwa* kati ya mengine. Maneno haya yanatukana, hudunisha na wakati yanapotumiwa dhidi ya jamii nyingine huwa ni ya chuki. Njia ya pili inahusiana na sitiari inayopatikana katika hotuba ya kisiasa. Katika kikundi hiki, vielelezo viwili vinavyojulikana ndani ya mazingira ya kisiasa ya Kenya kama yalivyoonyeshwa na takwimu zilizokusanywa ni pamoja na 'wafunge virago warudi kwao ' na kutajwa kwa jamii nyingine kama 'madoadoa'. Matamshi haya yanaposemwa hasa yanapotumiwa dhidi ya jamii nyingine yanakuwa ni ya chuki.

Vile vile, kama ilivyoonyeshwa na takwimu zilizokusanywa, lugha ni sehemu muhimu katika hotuba ya kisiasa na hivyo huchangia sana kuenea kwa hotuba ya chuki katika siasa nchini Kenya. Matamshi yote ya kisiasa yameunganishwa kwa lugha na hivyo matumizi ya lugha yanaweza kuchangia sana kuenea kwa hotuba ya chuki katika siasa. Hatimaye, jinsi tu imebainika kwamba lugha nyingi inaweza kusababisha kuenea kwa hotuba ya chuki, utafiti huu pia umetambua kwamba Kenya inaweza kutumia makundi yake matatu ya lugha, yaani, lugha za asili, Kiingereza na Kiswahili kuhubiri amani, umoja na kuleta ushirikiano wa kijamii. Kwa kuiga mawasiliano mazuri na kupinga hotuba ya chuki katika hotuba ya kisiasa, Kenya inaweza kufikia ushirikiano wa kijamii kupitia lugha.

Hata hivyo, hatua mbaya zinaonekana kuwa zimechukuliwa kushughulikia suala hili licha ya kuwa na Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano (NCIC). Tume hii ilibuniwa kwa kutambua kuwa amani ya muda mrefu, maendeleo na ushirikiano wa usawa kati ya wakenya unahitaji mchakato wa kuimarisha taasisi na mtazamo wa kujenga taifa, ushirikiano wa kitaifa na utangamano. Inasikitisha kutambua kuwa Kenya ina rekodi mbaya ya hotuba ya chuki, si ajabu jitihada za kupambana na hotuba ya chuki bado hazijafaulu. Kama vile Katiba yetu inayolinda uhuru wa kujieleza wa kila mmoja, Katiba yetu pia iko wazi sana juu ya kile kinachotajwa kama hotuba ya chuki. Watuhumiwa wengi wa kesi za hotuba ya chuki wameweza kushuhudia kesi zao zikichukuwa miaka mingi mahakamani, wengine wameweza kupata adhabu nyepesi au kesi zao kutupiliwa mbali kwa kukosa ushahidi wa kutosha.

### 5.3 Mapendekezo

Kulingana na matokeo ya utafiti huu kuhusu mchango wa sitiari za Kiswahili katika kueneza hotuba ya chuki katika siasa nchini Kenya, ushawishi wa lugha ya Kiswahili kwa kuenea kwa hotuba ya chuki katika siasa nchini Kenya, jinsi lugha ya Kiswahili inaweza kutumika kama zana katika kuleta ushirikiano wa kijamii nchini Kenya, na changamoto zinazohusiana na utekelezaji wa sera na sheria za ushirikiano wa kijamii nchini Kenya, zifuatazo ni baadhi ya mapendekezo muhimu yanayohitajika:

a) Uhamasisho unafaa ufanywe juu ya haki za kisiasa, kijamii na utamaduni wa watu binafsi na vikundi, ikiwa ni pamoja na uhuru wa kuzungumza, majukumu ya jamii, na matokeo

ambayo huja kupitia uhuru wa vyombo vya habari. Jamii inaonekana haijui madhara ya hotuba ya chuki. Jinsi umma ilivyoshangilia mbunge wa Gatundu Moses Kuria hivi karibuni akitoa hotuba ya chuki ni dhihirisho tosha ya madai haya. Kuna haja ya umma kutambua athari mbaya ya hotuba ya uchochezi na jinsi viongozi wanaweza kuchochea umma kwa kufanya vitendo vya ukatili. Vyama vya kisiasa lazima vihamasishe wananchi kuhusu hotuba iliyo sawa na yenye siyo sawa. Wakenya wote wana haki ya kuishi bila hofu na vitisho; hii ina maana ya kuwa sheria ni lazima ilinde haki za wengine na kuhakikisha utaratibu wa umma unaendana na kufuata demokrasia.

b) Waandishi wa habari wanapaswa kuwa na ujuzi na ufahamu wa kutambua hotuba ya chuki. Katika mikusanyiko mingi ya kisiasa, ni waandishi wa habari wanaofika kutoa ripoti juu ya mazungumzo ya kisiasa. Katika suala hili, ushahidi unaowasilishwa na vyombo vya habari wanaporipoti kauli ya chuki kwenye mkutano wa kisiasa unafaa kuruhusiwa mahakamani kusaidia kesi dhidi ya hotuba ya chuki kufaulu kortini.

c) Asasi za serikali zinapaswa kusimama na kuunga mkono vita dhidi ya hotuba ya chuki. Serikali, hasa mahakama, inapaswa kuweka sera na taratibu ambazo zitaharakisha mchakato wa utekelezaji wa hukumu dhidi ya kauli ya chuki. Polisi, DPP na Mahakama zinapaswa kufanya kazi pamoja ili kuchunguza, kukamata, kuhakikisha faini zimelipwa na kuthibitishwa kwa hatia ya washtakiwa ili iwe funzo kwa wenye tabia kama hizi. Kama ilivyobainika, mahakama imekuwa kizuizi katika shughuli nzima ya kushughulikia kesi za kauli za chuki. Vile vile kuna upungufu wa watu wa kufuatilia na kuchunguza hotuba ya chuki na hivyo kunyamazisha ndimi za wanasiasa wanaoeneza kauli ya chuki imekuwa changamoto kubwa.

d) Teknolojia ya kisasa inapaswa kukubaliwa na kutumiwa katika mchakato wa kuzuia na kufuru kesi za chuki nchini Kenya. Hivi karibuni, DPP iliiomba Bunge kuhalalisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika mahakama, ikiwa ni pamoja na kupokea ushahidi kupitia video, na upekuzi wa hali ya juu ya kiteknolojia. Kupitishwa kwa teknolojia ya

kisasa kutasaidia kuwezesha kupokea kwa ushahidi na kukamatwa kwa wale wanaofanya hotuba ya chuki katika siasa nchini Kenya.

e) Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano (NCIC), kama taasisi inayo jukumu na wajibu wa kuhakikisha umoja wa kijamii na ushirikiano nchini Kenya inapaswa kuunda mkakati wake vizuri katika kupigana na hotuba ya chuki kwa kubuni na kutekeleza sera ambazo zinalenga kuleta wakenya wote pamoja bila kujali sera, ushirikiano wa kisiasa, kabila, dini, au jinsia.

### 5.4. Mapendekezo ya utafiti zaidi

Bado kuna pengo kubwa la elimu katika mada ya hotuba ya chuki, hasa katika kesi ya Kenya. Watafiti wa baadaye wanaweza kufikiria kuchunguza mada zifuatazo: Mchango wa hotuba ya chuki katika kuhujumu demokrasia nchini Kenya; Athari za sitiari katika kukomesha hotuba ya chuki nchini Kenya; na mchango wa Kiswahili katika kuimarisha ushirikiano wa kijamii nchini Kenya.

## MAREJELEO


Abrahams M.H. (1957) *Glossary of Literary Terms: Toleo la tatu*, New York: Holt, Reinehart and Winston Inc.

Agoya-Wotsuna, Catherine (2012). The Role of Indigenous Languages in Kenya: A Case for Using Them as Languages of Instruction Throughout Primary School. *The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics, Vol. 2.* Retrieved from: http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/76813/Wotsuna_The%20role%20of%20indigenous%20languages%20in%20Kenya.pdf?sequence=2

Austin, J. L. (!962). *How to Do Things with Words*. London: OUP.

Bach, K., na Harnish, R. M. (1979). *Linguistic Communication and Speech Acts*. Massachussets: MIT Press.

Bekoe, Dorina (2010) Trends in Electoral Violence in Sub-Saharan Africa, *United States Institute of peace, Peace Brief 13.*

Bell, Jeannine (2009). Restraining the heartless: racist speech and minority rights. *Indiana Law Journal.* 84: 963–979.

Bennett, A. na Royle, N (1995). *An Introduction to Literature, Criticism and Theory*. London: Longman.

Bougher, L.D (2012). *The case of metaphor in political reasoning and cognition.* Political Psychology, 33, 145-163

Briggs, B. R. (2003). *Getting Involved: Speech Acts and Biblical Interpretation*. ANVIL Volume 20 No 1, 25 -34.

Bunt, H. C. (2000). Dialogue Pragmatics and Context Specification. Katika H. C. Bunt, na W. J. Black, Abduction, *Belief and Context in Dialogue Studies in Computational Pragmatics* (uk. 81 -150). Amsterdam: Benjamins.

Bussmann, H. (1996). *Routledge Dictionary of Language and Linguistics (2nd Ed).* London: Routledge

Calvert, Clay (1997). Hate Speech and its Harms: A Communication Theory Perspective. *Journal of Communication.* 47: 4–19. Cambridge: Cambridge University Press.

Capone, A. (2009). *Speech Acts, Classification and Definition. Katika J. L. Mey, The Concise Encyclopedia of Pragmatics* (uk. 1015 -1017). London: Elsevier Ltd.

Chapman, S. (2000). *Philosophy for Linguists: An Introduction*. London: Routledge

Clark, H. H., na Carlson, T. B. (1982). *Hearers and Speech Acts.* Language 58(2), 332-373.

Devitt, M., na Sterenly, K., (1991). *Language and Reality: An Introduction to the Philosophy of Language.* Massachussets: Blackwell.

Djik, T. A. (1977). *Text and Context: Explorations in the Semantics and Pragmatics of Discourse.* London: Longman.

Elam, K. (1980). *The Semiotics of Theatre and Drama*. Routledge: London

Emmanuel, S. na Kembo, S. (2017). Mwanga wa lugha. *Jarida la idara ya Kiswahili na lugha nyingine za kiafrika katika chuo kikuu cha Moi*, Eldoret Kenya

Esterhammer, A. (1993). Speech Acts and World-Creation: The Dual Function of the Performative. *Canadian Review of Comparative Literature* 20, 285-304.

Galvan, José L. (2015). *Writing Literature Reviews: A Guide for Students of the Social and Behavioral Sciences* (6th ed.). Pyrczak Publishing.ff

Gorman, D. (1999). *Use and Abuse of Speech - Act Theory in Criticism*. Poetics Today 20(1), 93 -119.

Hartman, T.K. (2012). *Toll booths on the information superhighway? Policy metaphors in the case of net neutrality*. Political Communication, 29, 278-298

Herz M and Peter M (2012). *The content and context of hate speech*. Cambridge University Press.

Holdcroft, D. (1978). *Words and Deeds: Problems in the Theory of Speech Acts*. Oxford: Clarendon Press.

Hornsby, J. (1994). *Illocution and its significance. Katika S. L. Tsohatzidis (Mha), Foundations of Speech Act theory: Philosophical and Linguistic Perspectives (uk. 187-207)*. New York: Routledge.

Istomine, V. (2010). Interpreting and Speech Acts Theory. Quality and Qualifications in Translation and Interpreting: proceeding of the IV International scientific conference Grodno, 8-9 October 2009 (pp. 25-29). *Grodno: Grodno State University*.

Kalmoe, Nathan (2014). *Fueling the Fire: Violent Rhetoric, Trait Aggression, and Support for Political Violence*, School of Media and Public Affairs, George Washington University.

Kissine, M. (2009). *Illocutionary Forces and What is said*. Mind and Language 24(1), 122-138.

KNHCR (2009). "Behaving Badly: The Referendum Report". Nairobi.

Kreidler, C.W., (1998). *Introducing English Semantics*. London: Routledge

Landau, M.J., Meier, & L.A. Keefer (2010). A metaphor-enriched social cognition. *Psychological Bulletin*, 136, 1045-1067.

Larson M.L., (1984). *Meaning Based Traslation, A Guide to cross- Language Equivalence*. New York; University Press of America.

Littlejohn, S. W. (2009). *Language and Communication. Katika S. W. Littlejohn, na K. A. Foss (Wah), Encyclopedia of Communication Theory (uk. 585 -589)*. London: SAGE Publications Ltd.

Lugwiri P.L.O (2009) Sitiari, Taashira na Tashibiha katika uwasilishaji wa dhamira katika Utenzi wa Tambuka. *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (MA) katika Kiswahili*, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Malmkjær, K. (1995). *Speech Acts. Katika K. Malmkjær (Mha), Linguistics Encyclopedia (uk. 560 -570)*. London: Routledge.

Masaki, Y. (2004). *Critique of JL Austin's Speech Act Theory: Decentralization of the Speaker-Centered Meaning in Communication*. Kyusha Communication Studies 2, 27-43.

Murray P. (1978) *Literary Criticism*. Harlow Essex, Longman Group.

NCIC (2010) Guidelines for Monitoring Hate Speech: Monitoring Hate Speech in the Electronic Media in Kenya. Nairobi

Oddsdottir, Freyja (2014). Peaceful or Violent? Online Hate Speech During Kenya's General Elections 2013, *Paper Presented at 'Perspectives on Conflict' Conference, June 6th 2014, Glasgow*

Oduori R.W (2002) Language and Politics in Kenya: Restricted and Elaborated Codes. Journal of Language and Linguistics. Retrieved from: http://webspace.buckingham.ac.uk/kbernhardt/journal/1_4/oduori1_4.htm

Olang', Tom (2010). Of hate think and hate speech in Kenya's political landscape. *Pambazuka News*. Retrieved from: http://www.pambazuka.org/land-environment/hate-think-and-hate-speech-kenya%E2%80%99s-political-landscape

Oyeniyi, Adeleye (2011) *Conflict and Violence in Africa: Causes, Sources and Types*. Africa.
Petrey, S. (1990). *Speech Acts and Literary Theory*.New York: Routledge.
Searle, J. R. (1975). *Indirect Speech Acts. Katika P. Cole, na J. Morgan (Wah), Syntax and Semantics 3 (uk. 59 -82).* New York: Academic Press.
Sharon, A.D (2013). A Web of Hate: European, U.S. Laws Clash on Defining and Policing Online Anti-Semitism. *Algemeiner Journal*.
Soames, S. (2010). *Phisolophy of Language*. New Jersey: Princeton University Press
Thomas, J. (1995). *Meaning in Interaction: An Introduction to Pragmatics*. England: Longman.
Tulkens, Françoise (2013). *The hate factor in political speech. Where do responsibilities lie* Programme of the Warsaw Conference of 18-19 September 2013
Umar, Ahmed (2015). Language and Control in the Campaigns for 2015 Elections. *Daily Trust*
USHMM (2015). *HATE SPEECH AND GROUP-TARGETED VIOLENCE- The Role of Speech in Violent Conflicts.* Raoul Wallenberg Place, SW Washington, DC
Venice Commission (2008). "Analysis of the Domestic Law Concerning Blasphemy, Religious Insult and Inciting Religious Hatred in Albania, Austria, Belgium, Denmark, France, Greece, Ireland, Netherlands, Poland, Romania, Turkey, United Kingdom on the Basis of Replies to a Questionnaire" (PDF). *Council of Europe*.
Verhey, A. (2007). *Scripture as Script and as Scripted: The Beatitudes. Katika V. A. Brawley (Mha), Character Ethics and the New Testament: Moral Dimensions of Scripture (uk. 19 -34).* Louisville: Westminster John Knox Press.
Wairima, M. L. (2009). *Explicit and Implicit Speech Acts in Gikuyu.* Tasnifu ya Uzamili iliyotolewa katika Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.
Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus.
Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi Misingi ya uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi Videmua Publihsers Ltd.

## KIAMBATISHO 1: Mpangilio wa muda uliotumika

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Aprili 2017, wiki ya 1 | Uteuzi wa tatizo |
| 2 | Mei- Juni 2017, wiki ya 2, 3, & 4 | Ujenzi wa pendekezo na uwasilishaji |
| 3 | Julai 2017, wiki ya 5, 6 & 7 | Ukusanyaji wa data |
| 4 | Oktoba 2017, wiki ya 8, 9 & 10 | Uchanganuzi wa data, kuandika na kuwasilisha tasnifu |

## KIAMBATISHO 2: Bajeti

| | Mahitaji | Gharama (KSH) |
|---|---|---|
| 1 | Kupiga taipu | 400 |
| 2 | Uchapishaji | 400 |
| 3 | Gharama za ukusanyaji wa data | 1500 |
| 4 | Usafiri | 500 |
| 5 | Nyenzo | 500 |
| 6 | Mahitaji mengine | 500 |
| | **JUMLA** | **3800** |

## KIAMBATISHO 3: Sitiari zingine

| Jamii | Msamiati ya chuki | Maana yake | Jamii lengwa |
|---|---|---|---|
| Wanga | Omurende | | Watu wote wasiozungumza lugha ya waluhya |
| Maragoli | Omukivala | | Wasioongea kimaragoli |
| Maragoli | Ababo | | Luo |
| Maragoli | Bidugudi | Wale wasioongea vizuri au wasioeleweka wakiongea | Kalenjin |
| Kisa | Abasebe | | Kikuyu |
| Pokot | Kaure | Walafi- wanaopenda kula sana | Luhya |
| Keiyo | Lamindet/Chepl amindet | | Wasioongea Kikalenjin |
| Keiyo | Lemek | | Lugha chafu ya kutaja wasio wakalenjin |
| Bukusu | Omusinde | Wasiotahiriwa | Luo |
| Kikuyu | Kihii | Wasiotahiriwa | Luo |
| Luo | Jo Rabuon | Wakulima wa viazi | Kikuyu |
| Bukusu | Banyolo | Waoga- wasiotahiri | Luo |
| Luo | Jo Got | Wanaoishi mlimani | Kissi |
| Kikuyu | Mode wa Nyuba | Mtu kutoka kabila letu | Wasioongea Kikuyu |
| Luo | Ja Dhot | Mtu kutoka kabila letu | Luo |
| Luo | Ja Tol | Mwenye Kamba | Kamba |
| Luo | Bimbe | Nyani | Kikuyu |
| Kissi | Ekenyambi | Magugu makaidi | Wasioongea kwa lugha ya Ekegusi |
| Swahili | Madoadoa | Alama ambazo hazitakikani na zinapaswa kuondolewa | Wale wasiotoka kwenye jamii iliyoanza kuishi mahali kitambo au wanaotoka kwa kabila lingine. |
| Kalenjin | Kekoyok | Ukoo au jamaa wa mbali | Kikuyu |
| Luo | Onagi | Waliong'olea meno | Luo |
| Kalenjin | Kaamama | Kazaliwa na mjomba | Kikuyu |
| Meru | Kiiji | Mvulana ambaye hajatahiri | Luo |

## KIAMBATISHO 4: Aina Mbalimbali ya Uainishaji wa Vitendo Usemi

| **Austin (1962)** | **Vendler (1972)** | **Searle (1975)** | **Bach & Harnish (1979)** | **Allan (1994)** | **Kreidler (1998)** |
|---|---|---|---|---|---|
| Vifunuzi | Vifunuzi | Taarifa | Taarifa | Kauli | Taarifa |
| Ahadi | Ahadi | Ahadi | Ahadi | Kauli | Ahadi |
| Vitumizi | Vidahili | Vielekezi | Vielekezi | Mwaliko | Vielekezi |
| Maamuzi | Viendeshi | Maamuzi | Viendeshi | Amri | Amri |
| Hulka | Hulka | Hisia | Pongezi | Hisia | Hisia |

## KIAMBATISHO 5: Kauli za kichochezi zilizochambuliwa

1. *".... Raila hakupeleka Ruto ICC, waache maombi ya uongo. Ruto ana mawakili, akishinda sawa na akibaki sawa. 2017 imekaribia na sisi kaka watu wa ODM tumebaki na risasi moja. Mimi ninamwambia party leader Raila Amollo Odinga, This time round the outcome of elections ikiwa tumeshinda na watunyanganye, wacha kiumane."*

2. *"... sisi ndio jeshi la Raila na tutakufa kabla ya yeye. Wasipotangaza Raila kama Rais wa Kenya kwa njia ya haki na ukweli wataona. Ile ya 2007 itakuwa ya kitoto."*

3. *"Tutaondoa madoadoa katikati yetu"*

4. *"Wale hawajatahiri peleka jandoni kwani kitu hiyo inapaswa kukatwa kwa sababu inadhoofisha uwezo wa kufikiri. Je! Tuko pamoja?"*

5. *"Hao watu wa Jubilee wakija Homabay wachapwe viboko na wapigwe na mawe."*

6. *"Jitu linaloitwa Raila linapaswa kupigwa kwa kichwa liuawe ili lisiharibu serikali ya Uhuru."*

7. *"Tunapaswa kumshinda mnyama huyu anayeitwa Raila ambaye anatuzuia kupata uongozi tena."*

8. *"Nyanza na Western inapaswa kuwa katika mstari wa mbele katika kampeni wa Nasa, na yeyote anayetoka katika miji hii miwili na anapinga atashughulikiwa vilivyo, yeyote anayetaka kuwa na tabia ya kupinga atakunjwa. Hatuna wakati wa kuvumilia mashetani ambao kazi yao ni kushikiana na maadui wetu."*

9. *"Watu wa maziwa tokeni nje ili kuondoa magugu yaliyo nyasini"*

10. *"Kwanza apashwe tohara" (yaani Raila lazima atahiriwe)*

11. *"Tuna nyoka ambaye tunapaswa kumwondoa"*

12. *"Njoo na usimame hapa ili unionyeshe ikiwa umetahiriwa na nyinyi njooni na panga ili kumwonyesha mtu huyu kuwa panga hazitumiwi tu kukata nyasi"*

13.*"Una mazoea ya kumtusi Uhuru na ukijaribu tena nitakuja hadi kwa nyumba ya mama yako kukupata. Unatuma picha zake hata kwa mtandao wa kijamii huna hata maadili. Mwambie Raila aache upuuzi na huwa ninawaeleza kuwa mwache kutangamana na mtu ambaye hajatahiriwa kwa sababu akili zake huwa pale pale"*

14.*"Bungoma hata jina ni yetu. Kule Trans nzoia ni kwetu. Na vile wanasema Trans nzoia ni ya kimataifa, sisi tunawaambia watu wa Trans Nzoia kura ikipita, funga virago mwende kwenu. Wale wako Bungoma Jubilee ikishinda, wafunge viraka waende kwao "*

15. "*Uhuru Kenyatta ni fisi na ni mwizi and we don't care about him and we don't respect him. This is not a police state; he can not intimidate us.*"

16.*"Naambia Rege alete hao chokoraa wa Jubilee HomaBay ndio ajue kwa nini punda hakuna mapembe*".

17.*"Joho, si mume kamili, hana elimu na ni kiroboto"*